ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID - SPIKA

1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe.Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais

17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais
19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake
28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe.Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil	-	Uteuzi wa Rais
33. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
34. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
35. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
36. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
37. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
38. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa

39. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Jimbo la Chambani

40. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake

41. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi

42. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake

43. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo

44. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo

45. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake

46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni

47. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje

48. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe

49. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini

50. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo

51. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani

52. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando

53. Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu

54. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni

55. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile

56. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae

57. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini

58. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini

59. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake

60. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole

61. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani

62. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

63. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake

64. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani

65. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy - Jimbo la Chaani

66. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni

67. Mhe. Omar Seif Abeid	-	Jimbo la Konde
68. Mhe. Panya Ali Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
69. Mhe. Rashid Makame Shamsi	-	Jimbo la Magomeni
70. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	-	Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
72. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
73. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
75. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
76. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
77. Mhe. Sira Ubwa Mamboya	-	Uteuzi wa Rais
78. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
79. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
80. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
82. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
85. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
86. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Thelathini – Tarehe 19 Juni, 2017

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma Dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Naomba kwanza nimwite Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko ili majibu ya maandishi aliyoahidi kuyaleta Barazani kwa Mhe. Nadir.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, wakati ninajibu swali Nam. 140 linalohusu Kiwanda cha Makuta kilichopo eneo la Buyu, liliulizwa swali la nyongeza na Mhe. Nadir Abdul-latif aliyetaka kujua kuna viwanda vingapi hivi sasa vinafanya kazi na vingapi havifanyi kazi na pia ni sababu gani zilizopelekea viwanda hivyo vikashindwa kufanya kazi.

Mhe. Spika, kabla ya kujibu swali la msingi la Mhe. Nadir Abdul-latif Mwakilishi wa Jimbo la Chaani, napenda kwanza nitoe maelezo machache kuhusu mgawanyiko wa sekta ya viwanda kwa mujibu wa sera ya ujasiri amali ya Zanzibar ya mwaka 2006 na sera ya viwanda ya Zanzibar ya mwaka 1998.

Kwa mujibu wa sera hizo, viwanda vyote nchini vimegawika katika makundi manne:

1. Viwanda vidogo sana (*Micro*) ambavyo vimeajiri watu wasiozidi wanne (1 – 4)
2. Viwanda vidogo vidogo ambavyo vimeajiri kati ya watu watano hadi kumi na tisa (5 – 19)
3. Viwanda vya kati ambavyo vimeajiri kati ya watu ishirini hadi tisini na tisa (20-99)
4. Viwanda vya kati ambavyo vimeajiri watu kuanzia mia moja na kuendelea (100 na ziada)

Kwa mujibu wa Sensa ya Viwanda ya mwaka 2012, Zanzibar kuna jumla ya viwanda 2,201 ambavyo vimeajiri watu 10,427. Kati ya hivyo, viwanda 235 vimeajiri kuanzia watu kumi na kuendelea kila kimoja. Viwanda 19 kati ya hivyo 235 ni vya upigaji matofali na usagaji wa kokoto (*Mining and quarrying*) na viwanda 216 ni vya uzalishaji (*Manufacturing*) ambavyo husarifu mazao ya kilimo (*Ago-processing*) kama kiwanda cha *ZANTO* na *ZATEPA*. Viwanda vyengine vinazalisha sabuni za kukogea, mafuta ya mwili (*Body lotion*), *shampoo* pamoja na sabuni ya kusafishia sakafu na vyombo vya jikoni kama vile INAYA, ZAYDAT, MKIPIMILIKI na kadhalika.

Pia viko viwanda vikubwa vya uzalishaji (*Manufacturing*) ambavyo vimeajiri watu wengi. Viwanda hivyo ni kiwanda cha maziwa (*Azam Milling Corporation*–Mtoni), Kiwanda cha Sukari (*Zanzibar Sugar Factory Limited* – Mahonda), Kiwanda cha Makonyo na Arki za mimea (*Pemba Essential Oil Distilleries* –Wawi Pemba) Viwanda vya Maji na vinywaji baridi (*Zainab Bottlers Limited*- Mombasa), *Drop of Zanzibar* – Jendele , *Super pure*–Amaan *Industrial Park, Skycola* – Tunguu na *Aqua blue* – Hanyegwa Mchana. Pia vipo viwanda vya ushoni wa nguo kama vile

Zanzibar Fashion LTD. Na *Zanzibar Quality Tailoring* – Amaan *Industrial Park*. Viwanda vyote hivi vinaendelea na uzalishaji wa bidhaa kama kawaida.

Kwa upande mwengine, viwanda vilivyositisha uzalishaji kwa miaka ya hivi karibuni ni kiwanda cha kutengeneza kaseti *Amaan Industrial Park* kilichofungwa kutokana na kubadilika kwa teknolojia ya kaseti kwenda CD, na Kiwanda cha Soda (Coca- Cola Maruhubi) kilichositisha uzalishaji kutokana na sababu zifuatazo:-

1. Kuathirika kwa mauzo ya soda kutokana na ushindani wa bei za soda za vibati zinazotoka nje ya nchi.
2. Kuongezeka kwa gharama za uzalishaji kutokana na uchakavu wa mitambo iliyokuwemo kiasi cha kupelekea kiwanda kuzalisha kwa hasara katika miaka miwili kabla ya kusitisha uzalishaji
3. Mitambo iliyokuwapo na ambayo ilikwishachakaa ilikuwa ni kwa uzalishaji wa soda za chupa za vigae ambazo zimepitwa na wakati, gharama inayohitajika kuwekeza mitambo ya uzalishaji wa soda za chupa za plastiki au vibati ilikadiriwa kufikia USD milioni tano, ambazo kampuni iliona ni kubwa kwa wakati ule.

Mhe. Spika, pamoja na maelezo haya wizara itafanya utaratibu wa kupitia viwanda vyote nchini na kujua idadi yake na shughuli wanazozifanya ili kufanya sensa ya uhakika. Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa.

Mhe. Spika: Ahsante sana sasa naomba nimwite Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira na yeye atoe taarifa.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako wakati najibu swali la nyongeza Nam. 113 Mhe. Naibu Waziri alivyokuwa akijibu aliulizwa swali na Mhe. Machano Othman Said aliomba kupatiwa fedha za miradi ya maji zilizotumika kuanzia mwaka 2000/2017.

Mhe. Spika, naomba kutoa ufafanuzi wa fedha ambazo zimetumika katika kipindi hicho mwaka 2000/2017. Jumla ya bilioni 178,251,400,000 zimetumika kwa miradi ya maendeleo kwa maji safi na salama nchini, kati ya fedha hizo bilioni 17,553,000,000 ni mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na bilioni 160,668,400,000 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 176
Idadi ya Skuli za Elimu Mjumuisho

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Zanzibar imepiga hatua kiasi katika maendeleo ya elimu kwa watu wenye ulemavu, na hivi karibuni kumekuwa na mpango wa kujumuisha wenzetu wenye ulemavu katika skuli za kawaida.

(a) Je, kuna skuli ngapi za elimu mjumuisho kwa Unguja na Pemba.

(b) Je, ni vipi serikali inazipa msaada skuli hizi kwa upande wa wataalamu, vifaa na mbinu za usomeshaji.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 176 lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Dhana ya elimu mjumuisho ni kuwa watoto wote wenye mahitaji maalum na wasio na mahitaji maalum kusoma pamoja katika darasa moja ili kuweza kusaidiana na kuondoa kujihisi kutengwa kwa watoto wenye mahitaji maalum. Skuli zote za Unguja na Pemba zinatakiwa zitayarishwe ili kuweza kutoa elimu kwa kuzingatia hali hii. Hii ni kusema kuwa hakuna skuli maalum zinazotoa elimu mjumuisho. Wizara ina jumla ya skuli 148 (skuli 89 Pemba na 59 Unguja) katika ngazi zote za elimu: Maandalizi, Msingi na Sekondari.

(b) Wizara inazisaidia skuli zote zenye wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa kuwapelekea walimu waliopatiwa mafunzo ya elimu mjumuisho, inazipatia vifaa mbali mbali vya kusomeshea na kujifunzia kama vile vile *Embosser, Perkin brailler, Voice recorder, photocopy machine, Dux bury Braille translator software, laptop computer desktop*, chaki, penseli, na vitabu. Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru washirika wetu wa maendeleo kwa misaada yao iliyofanikisha hili. Wahisani hawa ni pamoja na *Global Partnership for Education* (*GPE*), *Milele Zanzibar Foundation* na Shirika la *UNICEF*. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza kwa dhati Mhe. Naibu Waziri kwa kujibu swali la msingi. Baada ya kumpongeza naomba kumuuliza maswali mawili madogo sana ya nyongeza yenye (a) na (b).

a) Je, ni sababu gani zilizopelekea kuhamishwa kwa walimu wataalamu wa elimu mjumuisho ambayo wanafunzi wameshawazoea na huku kuhamisha walimu si kuwachanganya wanafunzi hao.

b) Vifaa kama ulivyovitaja katika mwaka jana skuli gani mlizozisaidia.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Ni kwamba uhamisho katika idara za serikali ni jambo la kawaida na mara zote uhamisho unapofanywa huwa unafanywa kutokana na sababu, zinawezekana ni sababu za kiufundi, inawezekana ni sababu za kinidhamu, inawezekana kutokana na sababu za kimahitaji. Kwa hivyo, walimu waliohamishwa kwa kweli wamehamishwa kutokana na sababu za kiufundi kwenda sehemu nyengine ili kutoa mchango wao kama walioutoa hapo sehemu ambazo walikuwepo.

b) Vifaa hivi vilisambazwa katika skuli maalum hasa hizi ambazo zina mahitaji maalum, na vilikuwa vingi vyenye thamani kama milioni mia moja na tisiini. Ahsante.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza napenda nichukue fursa hii kuipongeza sana wizara kwa uamuzi wake muafaka wa kuwajumuisha wenzetu wenye ulemavu katika skuli za kawaida. Lakini swali langu je, ni utaratibu gani ambao unatumika katika kuwawezesha walimu kukabiliana na wanafunzi hao wenye mahitaji maalum wakati wapo katika darasa moja na wale wengine wa kawaida ambapo wao wanahitaji msaada zaidi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:

Ni kwamba huu ni utaratibu ambao ni wa muda mrefu, hii dhana ya mjumuisho si dhana mpya kama tulivyoifafanua. Kwa hivyo, ili kuwasaidia walimu wetu kuweza kukabiliana na changamoto hizi za kuwasomesha wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa pamoja basi hupatiwa mafunzo mbali mbali. Kuna mafunzo ya muda mrefu, vyeti, diploma na hata *degree* lakini huwa kuna mafunzo mafupi kwa njia ya semina, pia kuna mafunzo mengine ambayo hutolewa na vituo vya walimu TC. Hizo ni baadhi ya njia ambazo huwa tunatumia wizara.

Mhe. Spika, lakini jengine ambalo wizara huwa inatumia ni kwamba kwa walimu wetu haya ni mazingira mapya, kwa hivyo pia huwa kuna mafunzo fulani ya kisaikolojia ili kuwakubali na kuwazoea wanafunzi wa namna hiyo. Ahsante.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii nikauliza swali dogo la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kama alivyotueleza katika swali lake mama kwamba wanafunzi hawa wa elimu mjumuisho wanawachanganyisha na wanafunzi wa kawaida. Nilikuwa nataka kujua ni wanafunzi wangapi hawa wenye mahitaji maalum walioweza kufaulu katika mitihani ya kitaifa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi ingekuwa vizuri zaidi akatufafanulia angetaka kujua mwaka gani na gani na gani ili kuweza kumpa takwimu hizo, miaka mitano, sita, saba au mwaka uliopita. Kwa hivyo, hatujui tutoe takwimu ya mwaka gani.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, nilikuwa nataka nipate takwimu za miaka mitano iliyopita.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kwa kuwa swali hili linataka takwimu na takwimu hatuwezi kuwa nazo hapa, naomba swali hili tulijibu kwa maandishi.

Nam. 184

Ongezeko la Wanafunzi wa Darasa la Kwanza na Uhaba wa Madarasa ya Kusomea

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Uandikishwaji wa wanafunzi wanaoanza darasa la kwanza umekuwa ukiongezeka kila mwaka lakini ongezeko hilo haliendani na uimarishwaji wa miundombinu ya madarasa ya kuwaweka watoto hao. Zipo skuli ambazo darasa moja lina wanafunzi mia moja na zaidi hali ambayo haileti matokeo bora katika ufundishaji.

Je, serikali imejipangaje kuhakikisha kuwa ongezeko la uandikishaji linakwenda sambamba na kuimarisha miundombinu ya kusomea kama madarasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 184 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, uandikishaji wa wanafunzi wanaoanza darasa la kwanza umekuwa ukiongezeka kila mwaka, lakini ongezeko hilo haliendani na uimarishaji wa miundombinu ya madara ya kuweka watoto hao. Zipo skuli ambazo darasa moja lina wanafunzi mia moja na zaidi, hali ambayo haileti matokeo bora katika ufundishaji.

Mhe. Spika, sasa naomba nimjibu kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, ni kweli kuwa uandikishaji wa watoto ni mkubwa kulinganisha na nafasi zilizopo. Kiwango cha idadi ya watoto wanaotakiwa kuwemo katika darasa moja ni 45. Hata hivyo, kutokana na upungufu wa madarasa, idadi ya wanafunzi kwa darasa kwa baadhi ya skuli inapindukia wanafunzi 100 hali ambayo inaathiri jitihada za upatikanaji wa elimu ubora.

Jitihada mbali mbali zinaendelea kuchukuliwa katika kuhakikisha tunaimarisha mazingira ya mtoto kujisomea. Miongoni mwa jitihada hizo ni kuhamasisha jamii kupitia kamati za skuli kusaidia ujenzi wa madarasa. Napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza jamii kwa muitikio wao. Jumla ya madarasa 285 yamejengwa na jamii mpaka katika ngazi ya gebo na kukabidhiwa wizara kuyamaliza.

Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, wizara yangu imeweza kukamilisha madarasa 32 yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi katika skuli 9 za Unguja na Pemba. Pia wizara imejenga mashirikiano mazuri na wahisani mbali mbali wa ndani na nje ya nchi, wakiwemo *Zanzibar Milele Foundation*, *Good Neighbors*, Serikali ya Watu wa China na Shirika la Misaada la Sweden (*SIDA*) katika kusaidia kutatua changamoto hii. Kupitia mashirikiano hayo ukarabati wa paa kwa skuli 16 unaendelea kufanyika kwa Unguja na Pemba, kuanza ujenzi wa skuli ya msingi Fuoni-Pangawe na ujenzi wa Skuli ya Kwarara Msingi unatarajiwa kuanza hivi karibuni.

Aidha, katika mwaka wa fedha wa 2017/2018, wizara imetengewa jumla ya TSh 2,000,000,000/- za serikali na TSh. 2,000,000,000/- za wahisani katika kasma ya uendelezaji wa miundombinu. Fedha hizo zitatumika kukamilisha jumla ya madarasa 200 yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi. Natoa wito kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa nafasi zao wasaidie kujenga madarasa na kufanya ukarabati wa skuli ziliopo kwenye majimbo yao ili kuwawekea mazingira mazuri kwa watoto kujifunzia.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana niendelee kumpongeza tena kwa mara ya pili Mhe. Naibu Waziri na mtu atapofanya kweli atasifiwa tu kwa ukweli wake, na atakapokuwa hakujibu swali la msingi ataelezwa tu ukweli wake. Umejibu tena kwa mara ya pili wali la msingi nikupongeze tena Mhe. Naibu na nitaomba nikuulize maswali madogo sana ya nyongeza. Na hili nafikiri litamuhusu Waziri wa Fedha na Mipango huenda akanyanyuka yeye ili kukusaidia.

a) Je, serikali haioni haja kuwa na mpango wa kuwashikirisha wawekezaji binafsi katika skuli na kutokana na kukiri kuwa darasa moja kuwa na wanafunzi mia moja kuwapunguzia kodi au kuwaondoshea kodi haipo haja hiyo na hili ningemuomba Waziri wa Fedha na Mipango akainuka ili akakusaidia, maana yake wawekezaji wako tayari kodi zimekuwa kubwa katika serikali.

b) La pili ni kwamba uliahidi katika Baraza hili kama miundombinu Skuli ya Bwejuu akanyanyuka waziri kutoka Ikulu Mhe. Issa Haji Gavu akasema kuna mfuko wa jimbo kule utajenga vyoo mpaka leo hakuna dalili baada ya shilingi elfu thalathini zilizotoka pale kufunika turubali. Na uliniahidi utakwenda ile safari ulikwenda lini ili wananchi wa Bwejuu wakusikie.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi maswali yake mawili kama ifuatavyo:

a) Mpaka sasa ukamilishaji wa majengo ya skuli uko ndani ya uwezo wa serikali, kwa hivyo mpaka sasa serikali haioni haja ya kuwashirikisha katika suala hili.

b) Skuli ya Bwejuu nimehakikishiwa na Mbunge kwamba ameahidi kukarabati vyoo vyote karibuni na atafanya hivyo kwa maandishi ametwambia hivyo.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipatia na mimi nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Spika, kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri na ya ufasaha, lakini ningependa nimuulize swali dogo la nyongeza. Kwa vile tunafahamu kwamba skuli karibu ya zote sasa hivi zina asilimia kubwa ya wanafunzi kujaa ndani ya madarasa kuliko uwezo uliopo ndani ya madarasa yale, madarasa yana wanafunzi 100 mpaka 190.

Je, serikali kwa sasa kwa vile bado suala hili la ujengaji wa madarasa linaendelea, ina mpango gani wa kuweza kudhibiti ile hali iliyopo mule ndani ya madarasa yale kwa walimu ambao wanasomesha, ili waweze kuondokana na ile changamoto ya uvumbikaji wa wanafunzi wengi ndani ya darasa moja na walimu wake kuweza kusomesha kwa ufanisi zaidi na kwa uelewa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ahsante sana kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Hidaya Ali Makame swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Ni kweli katika baadhi ya skuli wanafunzi ni wengi na kwa maana hiyo, imeweza kuleta changamoto kwa pande zote mbili, kwa walimu na kwa wanafunzi. Kwa upande wa walimu tumejaribu kuwapa mafunzo fulani ya kuweza kudhibiti madarasa makubwa (*teaching large class),* tumewapa mafunzo ili kuweza kuyabeba. Lakini kwa upande mwengine suala hili linafahamika na serikali na ndio kuna juhudi maalum ambazo zinachukuliwa na serikali katika mwaka huu wa fedha ili kuliondoa kabisa suala hili.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante Mhe. Spika, na mimi asubuhi hii kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza swali Mhe. Naibu Waziri wa Elimu. Mheshimiwa zamani kulikuwa kuna utaratibu maskulini wanafunzi tunapochelewa ilikuwa tunapigwa mikwaju au tunapewa adhabu ya kusafisha, lakini leo baadhi ya maskuli Zanzibar kuna utaratibu wa wanafunzi wanapochelewa wanalipishwa pesa. Naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri kwamba je, hii ni kanuni au sera, na pesa hizo zinakwenda wapi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Hassan Khamis Hafidh swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Suala hilo si sera wala kanuni wala mazowea. Kwa maana hiyo wizara inalipiga vita suala hili na imekuwa ikitoa maelekezo mara kwa mara, kwamba hakuna adhabu ya kulipisha fedha katika skuli, ni kwamba sasa hivi wizara imekuja na utaratibu mpya ambao tunauita 'heshima endelevu', ambayo inachukua nafasi ya adhabu mbadala na hiyo tunaifanyia kazi na itaondosha masuala haya ya kulipishana fedha na adhabu nyengine ambazo ni za vitisho na kuhatarisha maisha ya mwanafunzi. Ahsante.

Nam. 40

Fidia kwa Wananchi wa Jang'ombe Kufuatia Ujenzi wa Mtaro

Mhe. Abdalla Maulid Diwani - Aliuliza:-

Pamoja na kuipongeza SMZ katika kutatua shida za wananchi katika kipindi cha mvua na kupelekea kuchimbwa mitaro mikubwa katika sehemu mbalimbali za Manispaa ya Mji wa Zanzibar, ili kuondoa tatizo la kutuama kwa maji na kuhatarisha shughuli mbalimbali za wananchi katika maeneo yao.

(a) Je, serikali inatoa tamko gani kwa wakaazi wa Jang'ombe Urusi ambao nyumba zao zimependekezwa kuvunjwa na hivyo zimeshawekwa alama za X.

(b) Ni lini kazi hiyo ya kuvunjwa nyumba hizo itaanza na wakaazi hao kulipwa fidia ya nyumba zao hizo.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 40 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, serikali imekuwa ikichukua hatua za kuimarisha ubora wa maeneo ya makaazi kwa maana ya kuweka viwango bora vya kuishi katika maeneo hayo, ikiwemo ya kujenga miundombinu ya kupitisha maji ya mvua katika maeneo mbalimbali ya mji wa Zanzibar na vitongoji vyake. Mwishoni mwa miaka ya 2000, kwa msaada wa Serikali ya Ujerumani kupitia Benki yake ya Maendeleo, (*KFW),* iliandaa Mpango wa Ujenzi wa Misingi ya Maji ya Mvua katika maeneo tofuati ya Mji na kuigawa kama ifuatavyo:-

i) Mfumo A na B kwa ajili ya maeneo ya Mji Mkongwe;
ii) Mfumo C kwa eneo la Magogoni, Nyerere, Sebleni, Mikunguni, Saateni hadi Kinazini.
iii) Mfumo D – Maeneo ya Kijangwani na Kibandamaiti;
iv) Mfumo E – Magomeni kwa Mtumwajeni, Mpendae, kwa binti Amrani, barabara ya Jang'ombe Urusi, Migombani hadi Kilimani;
v) Mfumo F – eneo la Mnazimmoja; na
vi) Mfumo G – Mtopepo na karakana.

Mhe. Spika, kwa msaada wa *GTZ* mifumo A na B iliimarishwa kipindi hicho na kubakisha mifumo mingine niliyoitaja, ambayo hatimae imepata ufadhili wa mkopo nafuu wa Benki ya Dunia chini ya Mradi wa Uimarishaji wa Huduma za Mijini (*ZUSP*). Utekelezaji wa mradi huo unaendelela kupitia kwa Mkandarasi, Kampuni ya *CRJE* kutoka China. Kwa upande wa Mfumo E ambao Mhe. Mwakilishi ameulizia, tayari wananchi wote watakaothirika katika maeneo ya Magomeni, Meya, Jang'ombe Urusi, Kilimani na Migombani wameshalipwa fidia. Maeneo yaliyobakia ambayo hayajalipwa fidia ni Mpendae barabara ya Jang'ombe hadi Skuli ya Jang'ombe.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, sasa namjibu kama ifuatavyo:-

(a) Kama ilivyokuwa kwa wananchi wa maeneo mengine, serikali italipa fidia kwa wananchi wote wakaazi wa Jang'ombe watakaoathirika kufanikisha ujenzi huo.

(b) Malipo ya fidia yanatarajiwa kukamilika ndani ya mwezi wa Juni na Julai. Wananchi wataombwa kuvunja nyumba zao na kuchukua vitu vyao vyote mara tu watakapolipwa fidia ili kupisha maendeleo hayo muhimu kwa nchi yetu na wananchi wote katika maeneo hayo.

Mhe. Abdalla Maulud Diwani: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mubashara ya Mhe. Waziri wa Fedha na kutia matumaini kwa wakaazi wangu wa Jimbo la Jang'ombe nina maswali ya nyongeza (a) na (b).

(a) Mhe. Waziri ni utaratibu gani uliotumika hapo mwanzo wakati wa kutathmini walipiga X nyumba nzima, lakini mara baada ya majadiliano ya muda mrefu wakabadilisha ule muundo wakaja wakapiga nusu nyumba.

(b) Je, hawa watu waliopata kadhia hii watalipwa katika mfumo gani, ni mvumo ule wa nyumba nzima kama ilivokuwa mwanzo au huu mfumo wa pili wa nusu nyuma.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, tarifa niliyonayo kwamba mfumo uliotumika ni mfumo wa kuweka X kwenye nyumba na sio nusu nyumba. Hadi sasa kwa eneo alilolitaja Mhe. Mwakilishi ambalo lilikuwa na nyumba 83, nyumba 52 tayari zimeshalipwa kwa maana hakuna matatizo ya nyumba hizo na nyumba 21 zilionekana na kasoro ambazo zinafanyiwa kazi hivi sasa na zinatarajiwa baada ya kukamilika tathmini hiyo basi na wao walipwe malipo yao. Sasa sina taarifa ya nusu nyumba. *(Makofi)*

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Spika, na mimi kwa kuniona na nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuamsha salama. Nashukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mauzri, lakini nataka nimuulize kwamba tunasema barabara zetu tunapozijenga zina sheria na kipimo cha kuifata barabara kwamba usijenge hili ni eneo la barabara, lakini kila siku wanajenga lakini nimuulize waziri, je, anayejenga katika eneo la barabara ambalo ndio *meter* ambazo zimepangwa kwamba hapa usifike barabarani, mwenye makosa ni serikali au mwananchi. Lakini kama ni mwananchi inakuwaje serikali ilipie fidia ya mwananchi yule.

Mhe. Spika: Mhe. Suleiman Sarahan swali la msingi linaulizia mitaro sio barabara. Samahani Mhe. Zulfa Mmaka Omar swali la nyongeza.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeze lenye kitoto (a) na (b).

(a) Ni watu wangapi watakaohusika katika bomoabomoa hii Jang'ombe na fidia yao ni kiasi gani.

(b) Watatumia taratibu zipi kuwalipa watu hawa ili kuepukana na matatizo ya lawama za wananchi kutokulipwa fidia zile kwa wakati na ukamilifu katika eneo hili.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Zulfa Mmaka Omar kama ifuatavyo. Kwanza kama nilivyosema katika eneo lililozungumziwa la Jang'ombe kuna nyumba 83 ambazo hizo zinaanzia Kwa-Mchina hadi Jang'ombe na tunatarajia katika eneo hilo zilipwe takriban shilingi 2.3 bilioni. Lakini nyumba 52 kama nilivyojibu mwanzo tayari zimeshalipwa na sasa kuna suala la kulipa nyumba zilizobakia 21.

Utaratibu unaotumika kulipa fidia hizi, ni kwamba wahusika wote wanatakiwa kuleta *account* zao na fedha zinaingizwa katika *account* zao.

Nam. 182

Mpango wa Kutoza Kodi Vyuo vya Qur-ani

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Kumekuwa na taarifa kuwa serikali inataka kuanzisha mpango wa kuvitoza kodi Vyuo vya Qur-ani wananchi wamekuwa na shauku kutaka kujua ukweli wa mpango huo.

Je, mpango huo upo kweli na kama upo kweli kitu gani kimezingatiwa katika kutoza kodi Vyuo vya Qur-ani ambavyo siyo sehemu za biashara.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango - Alijibu:

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 182 kama ifuatavyo:-

Serikali inaelewa umuhimu wa Vyuo vya Qur'ani na serikali inaelewa umuhimu huo kwa ukuzaji dini na utamaduni wa Zanzibar pamoja na kudumisha silka na maadili ya watoto wetu. Kwa ujumla, serikali imekuwa ikisaidia sana taasisi za kidini ikiwemo kwa kuzipa unafuu wa kodi. Hivyo taarifa alizonazo Mhe. Mwakilishi naomba nieleze kwamba sio sahihi kwani serikali haijafikiria na haina mpango wa kuvitoza kodi Vyuo vya Qur'ani. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu ya rafiki yangu Mhe. Waziri naomba kumfahamisha au kumuelimisha kidogo tu, sikusema taarifa nilizokuwanazo ni sahihi aiangalie *order paper* ilivyosema na tunaongozwa na Katiba ya Zanzibar kifungu cha 88 Mhe. Spika, naomba nikinukuu kazi ya Baraza la Wawailishi.

"Baraza la Wawakilishi pamoja na kuongeza juhudi zake kutokana na vifungu vya katiba...

Mhe. Spika: Mheshimiwa naomba uulize swali la nyongeza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Sasa tunapojibu haya maswali tujibu kwa utaratibu mimi sikusema taarifa zangu ni sahihi, sasa tunaongozwa na Kanuni hizi Spika tukiziweka kando tutakuwa hatukifanyii chombo chako haki.

Mhe. Spika: Naam!

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kama hizi kanuni hatukuzitumia tutakuwa hatukifanyii haki chombo chako hiki, lazima tuziongoze na ili zikafanye kazi.

Mhe. Spika: Mheshimiwa swali lako la nyongeza ni lipi mana naona kama unalalamika tu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Hewallah, pamoja na hivyo twende anavyoanguka ndivyo anavyochinjwa twende hivyo hivyo. Je, serikali kulikuwa kuna kitengo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na kama nitakosea nifahamishwe, kuhusu kitengo hicho kuhusu madrasa nataka kuelezwa, kama nitakosea nikosolewe bado kipo au hakipo, kinachoshughulikia Vyuo vya Qur-ani? Hapo nyuma nakumbuka kilikuwepo je, sababu havitozi kodi kufikisha bajeti katika Vyuo vya Qur-ani kutoa tamati hizo. Kwa mfano, kuvuja, saruji, sakafu na madirisha; kulikua kuna kitengo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kinashughulikia suala hilo.

Mhe. Spika: Mheshimiwa tafadhali usituhutubie uliza swali la nyongeza tu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mheshimiwa nakuja katika swali la nyongeza, kwa kuwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ina kitengo kinachotoa masuala ya madrasa na Vyuo vya Qur-ani

kama bado kipo naomba kusahihishwa. Je, serikali havitozi kodi ikafika bajeti katika Vyuo vya Qur-ani ili kutatua matatizo yao ikiwemo sakafu, madirisha na saruji. *That is (a)*

(b) Je, serikali haioni haja ya kutoa sabuni kwa walimu wale baada ya kusema tu kwa mdomo na vitendo kuwa tumepunguza kusaidia, mdomo rahisi kusema vitendo havipo hasa ukizingatia vyuo vya mashamba ikiwemo Unguja na Pemba ndio waathirika wakubwa.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Kwanza kama nilivyosema taasisi zote za kidini hazilipishwi kodi na ikiwemo vyuo vya Qur-ani. Kama kitengo kipo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali sina hakika kama kitengo hicho kipo, lakini kama kipo na taarifa iliyopo kwamba hicho kitengo kipo na inapohusika kwamba saruji, nondo, mabati au vifaa vyovyote vinakwenda kwa ajili ya madrasa wizara inatuandikia kuomba msamaha wa kodi na serikali inatoa msamaha huo kwa vifaa hivyo.

La pili alilolizungumza la kwamba serikali tuache kuzungumza kwa maneno kusaidia Vyuo vya Qur-ani, serikali haisaidii kwa maneno tu, lakini kusamehe kodi ni fedha ya serikali. Kwa hivyo, tukisamehe kodi ni kwamba tumevisaidia vyuo hivyo kifedha kabisa. Lakini vile vile serikali hadi sasa haina mpango wa kulipa au kuwalipa walimu wa madrasa kwa sababu; suala la sekta ya elimu linachangiwa na wadau mbali mbali ikiwemo jamii yenyewe, ina mchango wa kutoa katika sekta hii, lakini washirika wa maendeleo nao wanatusaidia na serikali pia inatusaidia. Kwa hivyo, mchango wa jamii katika vyuo vya Qur-ani nao pia unathaminiwa na serikali yetu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Utaratibu.

Mhe. Spika: Hapana Mheshimiwa, Mhe. Nassor Salim Jazira swali la nyongeza.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, mbali na majibu mazuri sana kabisa ya Mhe. Waziri kwa kuwa Jimbo la Kikwajuni kupitia Mbunge na Mwakilishi wa jimbo hilo, wamevitambua Vyuo vya madrasa viliomo katika jimbo la Kikwajuni na kuweza kuvisaidia posho la kila mwezi kwa walimu wote ambao wanasomesha madrasa katika jimbo la Kikwajuni, na kwa kuwa serikali yetu inavitambua na kuvisaidia na kuiendeleza dini yetu ya Kiisilamu. Je, serikali ina mpango gani wa kuwasaidia, lakini vile vile ni madrasa ngapi ambazo zinatambulika rasmi na serikali yetu ya Zanzibar kwa Unguja na Pemba.

Pili, ni mpango gani mkakati ambao unaoendelea au utaendelezwa kuhakikisha kwamba walimu wetu wa Unguja na Pemba wa madrasa wanapata misaada mbali mbali kutoka nchi mbali mbali misaada ambayo inatoka kupitia Wizara husika.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe Nassor Salim Ali swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Kwanza serikali inavitambua vyuo vyote vya Qur-ani viliopo lakini pia inatambua taasisi za kidini ziliopo nchini zote. Kama nilivyosema katika jibu nililolitoa mwanzo ni kwamba serikali haina mpango kwa sasa hivi wa kulipa posho au mishahara walimu wa madrasa hizo, na nilisema kwamba sisi Waheshimiwa Wawakilishi

kwanza nasi tuna mchango wetu wa kusaidia vyuo hivyo katika jamii kama sehemu ya jamii na naamini wapo Waheshimiwa Wawakilishi hapa ambao wanafanya kazi hiyo. Lakini vile vile jamii iendelee kuvisaidia vyuo vyetu vya Qur-ani na serikali nayo itaendelea kutoa msaada wake kwa maana ya kwamba kusamehe kodi zote kwa ajili ya kuendeleza madrasa na vyuo vya Qur-ani lakini pia taasisi zote za kidini nchini.

Nam. 52

Kuanza Ujenzi wa Hospitali ya Binguni

Mhe. Simai Mohamed Said - Aliuliza:-

Ni lini Hospitali ya Binguni katika Wilaya ya Kati, Jimbo la Tunguu itajengwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Kny. Mhe. Waziri wa Afya): - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Afya naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 52 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi iliahidi kupitia Ilani yake ya 2015 – 2020 kujenga hospitali ya kisasa eneo la Binguni, Wilaya ya Kati Unguja. Wizara ya Afya imeanza hatua za awali za kutayarisha mahitaji ambayo yataingizwa katika kufanya tathmini yakinifu (*Feasibility Study*) itakayotoa mahitaji halisi pamoja na gharama za majengo, wafanyakazi watakaohitajika, vifaa na gharama nyengine.

Matokeo ya tathmini hiyo yatawasilishwa serikalini na hatimae baada ya kupata ridhaa ya serikali kuendelea na taratibu nyengine za zabuni. Mchakato unaendelea vizuri na hatua zinazofuata tutawajulisha Waheshimiwa Wajumbe kama tutavyosikia.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante Mhe. Spika, mwaka jana wakati nauliza maswali au kupata maelezo juu ya Hospitali ya Binguni serikali iliniahidi kwamba katika zile kazi ambazo za ajira zilizokuwa zina ujuzi na zisizokuwa na ujuzi watapatiwa wananchi katika maeneo husika hasa Shehia ya Tunguu, Binguni pamoja na Mtakuja.

(a) Je nataka kujua ahadi ile ya serikali juu ya ajira wakati wa mchakato wa ujenzi utakapoanza je, ipo pale pale au serikali sasa imebadilisha mawazo yake.

(b) Kwa kuwa eneo la Binguni ni eneo ambalo lipo katika eneo la ndani ambalo haliko baharini na mwaka huu tuliona uchafuzi wa mazingira katika Hospitali ya Mnazi Mmoja hasa katika fukwe zetu.

Je, serikali katika kuhakikisha kulinda hasa maji ambayo yako chini ya ardhi pamoja na mazingira na eneo la kilimo kuhakikisha kwamba mazingira yetu katika eneo hili hasa la Shehia ya Binguni yanalindwa. Ni utaratibu gani ambao awali serikali imechukuwa ili kuhakikisha kwamba wananchi katika maeneo husika hawataathirika na madawa pamoja

na uchafu wa mazingira ambao utatokana au maji yatakayotumika katika eneo hili husika. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Kny. Waziri wa Afya): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Afya naomba kujibu swala ya nyongeza lenye a na b la Mhe. Simai Mohamed Said kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kuhusu utaratibu wa kuajiri ahadi ya serikali itakuwepo pale pale kama ilivyotolewa na Mhe. Waziri wakati akijibu swala hili.

(b) Kuhusu maswala ya mazingira Mhe. Spika, nataka nilihakikishie Baraza lako tukufu kwamba serikali inachukua hatua na itaendelea kuchukua hatua kuhakikisha kwamba mazingira yetu yanalindwa na yale yote ambayo yamejitokeza katika Hospitali ya Mnazi Mmoja hivi sasa serikali imeweka utaratibu maalum wa kuhakikisha matatizo ambayo yanajitokeza kuhusu uharibifu wa mazingira yanachukuliwa hatua ili tuendelee kuwa na hospitali safi na wananchi wapate huduma bora na katika ujenzi wowote wa hospitali utakaofanywa kabla ya kufanya ujenzi huo. Hatua zote za kimazingira na usafi wa eneo zitachukuliwa ili kuhakikisha wagonjwa wanaokuja hapo hawapati madhara zaidi na wananchi wanaoishi jirani katika maeneo hayo hawaathiriki kutokana na matatizo yatakayojitokeza ya uharibifu wa kimazingira.

Kwa msingi huo basi serikali itaendelea kuchukua hatua madhubuti kuhakikisha mazingira yetu yanakuwa safi na hali za wananchi wetu zinakuwa bora. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Spika, ahsante kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swala dogo sana la nyongeza.

Kwa sababu Mnazi Mmoja Hospitali tumeitangaza kuwa ni Hospitali ya Rufaa hivi karibuni na imekumbwa na matatizo makubwa ya uendeshaji lakini pamoja na vifaa tiba.

Je, serikali ina mpango gani wa kuhamisha fedha za Binguni kwanza tukalishughulikia Mnazi Mmoja ili tupeleke huko.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Kny. Waziri wa Afya): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Afya naomba kujibu swala la Mhe. Mohammed Said Mohammed kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, kwanza kwa mwaka huu wa fedha hakujatengwa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Binguni tumo kwenye maandalizi ya ujenzi wa Hospitali ya kisasa ya Rufaa iliyo kubwa katika eneo la Binguni na mimi naamini Wajumbe wa Baraza lako tukufu na wananchi wote watataka ujenzi huo uendelee.

Hata hivyo, serikali kwa umakini mkubwa kutokana na hali ya uwezo wake katika bajeti ya mwaka huu imetenga fungu maalum la kuimairisha Hospitali ya Mnazi Mmoja na hatua mbali mbali zinachukuliwa katika kuimairisha Hospitali ya Mnazi Mmoja na nyote ni mashahidi.

Baraza hili limelalamikia kuhusu *ICU*, sasa *ICU* iko katika hali nzuri, ililalamikia kuhusu wodi ya wazazi sasa iko katika hali nzuri, ililalamikia kuhusu *emergence* katika Hospitali ya Mnazi Mmoja sasa hivi ipo katika hali nzuri na kila hatua zinachukuliwa ili kuimarisha Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa maana ya kuelewa kwamba ndio Hospitali yetu Kuu hapa Zanzibar.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo lenye kifungu (a) na (b).

Kwa kuwa Mhe. Waziri katika majibu yake ameeleza kwamba serikali inaendelea kufanya utafiti kupata tathmini halisi katika uendelezaji wa huu ujenzi. Mara zote utafiti unapofanyika serikali huingia mikataba au kumtafuta mshauri elekezi kwa lugha nyengine *consultant*.

(a) Je, ni mshauri gani ambaye anafanya kazi hii ya utafiti kwa niaba ya serikali.

(b) Ni gharama gani ambazo tutatumia mpaka kukamilisha ule utafiti na lini utakamilika. Nakushukuru sana.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Waziri mahiri, shupavu, jemedari Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza Mhe. Miraji Khamis Mussa Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Chumbini swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

(c) Tuliemteuwa mpaka sasa ni Ardhi *Institute* ya Chuo cha Dar es Salaam hatua za awali zimeshatuonesha kwamba pale pahali panafaa kabisa kujengwa Hospitali ya Kisasa ya Rufaa ambayo itakuwa si ya Jimbo la Mhe. Simai Mohammed Said pake yake lakini itakuwa ya kitaifa kwa Zanzibar nzima.

(b) Katika eneo hilo hilo pia patakuwa na Taasisi ya Utafiti ambayo itakuwepo katika eneo hilo hilo. Lakini hapo hapo naomba kumueleza Mhe. Mwakilishi kwamba gharama za awali tulizopata ukilinganisha na ule upembuzi yakinifu pamoja na *feasibility study* ni milioni sitini na sita na hizo gharama tumeziangalia ni nafuu kuliko kwengine kote tulikopata *quotation* mbali mbali ahsante Mhe. Spika.

Nam. 91

Kudorora kwa Ujenzi wa Kiwanja cha Soka Kitogani

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, hoja ya kuleta maswali ni kazi kubwa Mhe. Spika, ndani ya chombo chako hichi na tunapata shida sana kuandika maswala ikiwa Waziri au Naibu Waziri anavyotaka kujibu anavyojua yeye .....

Mhe. Spika: Mheshimiwa naomba uulize swali.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, hapo nje Mhe. Rais shahidi, alipotupa semina kuhusu Mawaziri au Manaibu Waziri .....

Mhe. Spika: Mheshimiwa naomba uulize swali.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mheshimiwa kwa unyenyekevu wa hali ya juu naomba kuliondosha swali kugombana na mtu kutaka.

Mhe. Spika: Unaliondosha?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Naliondosha ndiyo.

Mhe. Spika: Ahsante sana swali limeondolewa, katibu wizara inayofuata.

Nam. 158

Umuhimu wa Matumizi bora ya Ardhi

Mhe. Suleiman Sarahan Said– Aliuliza**:**

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejitahidi kupanga mipango miji na vijiji katika sekta tofauti za maendeleo katika kwenda na kasi ya maendeleo kama Utalii, Viwanda na kadhalika. Lakini Zanzibar ni ndogo kwa ukubwa wa Ardhi yake na ni kubwa kwa ukuaji wa idadi ya wananchi wake. Lipo neno lenye maana kubwa na nzuri sana ya matumizi bora ya ardhi lakini neno hili ni kama nyimbo sio kitendo kwani sioni kama linatekelezwa.

(a) Je, Serikali hailijui suala la ardhi ya Zanzibar ni ndogo na haiongezeki lakini watumiaji wanaongezeka.

(b) Je, Serikali ina kipimo gani cha ukubwa kwa kupewa ardhi ya matumizi, kwa ajili ya mahoteli, viwanda, villa, nyumba za kuishi au kila mmoja anavuta kamba atakapo tu.

(c) Kama Sheria ipo mbona haitumiki au kama haipo mbona haiwekwi ili kuinusuru Zanzibar na watu wake kutokana na wajanja wachache wanaojichukulia maeneo makubwa bila kiasi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ardhi Maji Nishati na Mazingira naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 158 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo**:**

(a) Serikali inaijua hali hiyo na kwa kulielewa hilo vizuri ndio maana serikali ikaweka mikakati na taratibu za mipango miji kwa nchi nzima.

(b) Serikali imejiwekea taratibu maalum za ugawaji wa ardhi kwa matumzi mbali mbali. Kila mtumiaji anapewa kiwanja kwa ajili ya mahitaji yake na utaratibu ulivyo. Mkakati wa Maendeleo ya Ardhi na *Master plan* (2015) vimeweka wazi taratibu hizo ambazo zimeshaanza kutumika mijini na vijijini.

(b) Sheria na Kanuni za kuelekeza utumiaji ardhi zipo na zinatumika. Mfano, Mpango Mkakati wa Maendeleo ya Ardhi (*NSDS*) ni wa Zanzibar nzima na umeshaanzwa kutekelezwa. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Spika, sijui niseme vipi hili swali (b) naona halikujibiwa kwa sababu nilisema kwamba:

Je, serikali imeweka kipimo gani cha ukubwa wa ardhi ya matumizi kwa ajili ya mahoteli, viwanda, nyumba za kuishi au kila mmoja anavuta kamba atakapo. Hili suala sikulisikia. Sasa sijui niendelee na suala la nyongeza au inakuwaje.

Suala la nyongeza nauliza kwamba, katika sehemu zetu za mahoteli sehemu za ufukwe tumeweka mita 15 kwamba ardhi ya sehemu ya ufukwe iachiwe wazi isijengwe. Lakini kila tukipita kuna baadhi ya mahoteli mengine yamejenga ndani ya uzio huo. Suala langu nilikuwa nauliza.

(a) Wakati wa kuweka mikataba wale watu ambao wamepewa sehemu zile hawakuelezwa suala hilo.

(b) Kama wameingia ndani ya mita 15 je, serikali imechukuwa hatua gani.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mwakilishi wa Chake Chake swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwanza nilikuwa namjibu swali ambalo ameulizia kuhusu habari ya ufukwe kwamba zile mita ziko kwa mujibu wa sheria na kwa mujibu wa utaratibu na sasa hivi sio 15 tena ni 30 kwa mujibu wa sheria ya mazingira. Sasa kuna tatizo ambalo limejitokeza kuna maeneo ambayo yamejengwa kwa muda mrefu kabla ya sheria hii kupitishwa ndani ya Baraza lako hili tukufu, kwa hivyo kulikuwa kuna *consideration* nyengine. Lakini kwa wale wapya wote ambao wanajenga sasa hivi bado wataendelea na vigezo vile vile na kuvifuata kwa mujibu wa sheria ile ya mazingira iliyokuwepo ya mita 30 kwenye ufukwe wa bahari.

Lakini naomba nimjibu katika suala lake (b) lile la kwanza kiwango gani kimewekwa.

Mara nyingi inategemea mahitaji lakini kiwango ambacho moja kwa moja kiliwekwa kabla ya vigezo ambavyo sasa hivi tumevibadilisha kutokana na sheria hii ya *ZIPA* na utoaji wa watu, lakini mara nyingi tunawapa watu kwa mujibu wa mahitaji na eneo liliopo na ukubwa wa ile *project* ambayo inafanyika hicho ndicho kilichokuwepo. Ahsante sana.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante Mhe. Spika, na mimi namuuliza kidogo tu Mhe. Waziri pamoja na majibu aliyoyatoa.

Mhe. Spika, jimbo langu mimi la Tunguu ni katika eneo moja ambalo linapata makazi mapya na viwanja vingi vimekuwa vinakatwa kupatiwa wananchi wa Zanzibar wenye silka, madhehebu dini tofauti.

Mhe. Spika, ni kwa nini serikali haijaipa kipaumbele katika ujenzi wa nyumba za ghofa ili kuhakikisha kwamba rasilimali ya ardhi inatumika vizuri katika eneo la Jumbi mji mpya wakati wanagawa hivi viwanja pamoja na Tunguu hasa kwa watu ambao wanajulikana wana uwezo wa kujenga nyumba za ghorofa. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Simai Mohamed Said swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Ni kweli eneo la Tunguu ni eneo sasa hivi limekatwa viwanja kwa ajili ya mahitaji. Lakini pia kuna eneo limetengwa kule kwa ajili ya nyumba za ghorofa ambazo zitajengwa na wenzetu wa *ZSSF* kwa ajili ya kuendeleza mpango huu ambao tunaona tutumie ardhi vizuri. Lakini sasa hivi pia tutakwenda na mkakati wa kujenga za ghorofa kupitia Shirika la Nyumba la Taifa katika eneo lile la Tunguu nao watajenga majumba ya ghorofa.

Kwa hiyo, naomba awe na uvumilivu kidogo wenzetu hawa bado wanaendelea kujipanga ili mahitaji hayo yaweze kufanyika.

Nam. 17

Uendelezaji wa Kilimo cha Minazi

Mhe. Hidaya Ali Makame - Aliuliza**:**

Mashamba ya minazi yanayopatikana katika maeneo ya Kijichi, Kizimbani *Paidoc* na Kizimbani kwenye shamba la mikarafuu yana minazi ya asili ambayo imeshaleta manufaa makubwa kwa Serikali na kwa wananchi kwa ujumla, lakini minazi hiyo kwa sasa hadhi na ubora wake wa kuzaa umepotea kwa sababu ya kukosa kushughulikiwa.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuatika mbegu za minazi mirefu kama ile iliyomo kwenye shamba la minazi *paidoc,* ili uhalisia na ubora wa shamba lile usipotee.

(b) Wizara inachukua hatua gani kuona kwamba minazi iliyopo Kijichi na kwenye shamba la mikarafuu Kizimbani inafanyiwa upaliliaji makini ili iweze kuzaa kama minazi mengine ya kawaida.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 17 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuayavyo:-

(a) Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo ina jukumu la kuatika mbegu za minazi katika vituo vyake vya Kijichi, Selem, Bambi na vitalu vyenginevyo kwa ajili ya uimarishaji wa mashamba na kuwauzia wananchi wanaohitaji. Mwaka 2016/17 Wizara iliotesha miche 11,544 ya minazi ya asili. Kati ya hiyo miche 68 tu ilipandwa katika kituo cha Bambi na iliyosalia kuuzwa kwa wananchi. Upandaji mpya katika vituo hivyo ni mdogo kutokana na tatizo la wizi wa miche unaojitokeza mara baada ya upandaji kufanyika katika maeneo hayo.

(b) Mhe. Spika, palizi katika shamba la minazi la Kizimbani ni suala linalopewa kipaumbele na limewekewa mkakati maalum ambapo baadhi ya wafanyakazi huazimwa maeneo kwa ajili ya kupanda mazao ya muda mfupi. Upandaji wa mazao hayo husaidia kufanya usafi ikiwa ni sehemu ya palizi. Kwa upande wa shamba la mikarafuu la Kizimbani, Taasisi hupanga ratiba maalum ya usafishaji wa shamba hilo kwa kutumia wafanyakazi wake. Hata hivyo, nguvu za ukuaji wa magugu pamoja na upungufu wa wafanyakazi husababisha shamba kutokuwa katika hali ya usafi wakati wote.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Spika, kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake. Lakini ningependa nimuulize swala dogo la nyongeza lenye vitoto (a) na (b).

(a) Mhe. Waziri katika majibu yako hapa umetwambia kwamba miche 11,544 ilioteshwa. Je, ni miche mingapi iliyopangwa kwa ajili ya shamba la *Paidoc* ili kuliendeleza shamba lile na lisipotee uasili wake.

(b) Kuna aina ngapi za huu upalizi wa minazi yaani mashamba ya minazi kuna aina ngapi za kupalilia haya mashamba ya minazi.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kwanza naomba kumjibu Mhe. Hidaya Ali Makame maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Shamba la *Paidoc* analolizungumzia nilisema tunapanda minazi 68, lakini kwa bahati mbaya tunapata tatizo la wizi watu wanakuja wanachukua miche yetu, kwa hilo ni moja katika tatizo tunalolikabili sasa hivi.

Lakini kuhusu swali la pili kwamba ni miche mingapi tumewapa watu kama nilivyosema 11,544, tumewapa wananchi mbali mbali kuweza kupanda.

Suala la palizi aina gani za palizi, palizi ni aina moja tu pale ambapo tunafanya sisi wenyewe tunatumia watu wetu, pale ambapo hatuna tunawapa watumishi wetu maeneo yale walime huu ndio utaratibu wa palizi ambazo tunazifanya.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii kumuuliza Waziri wa Kilimo swali la nyongeza. Kwanza nimpongeze katika majibu yake, lakini kwa kuwa Waziri wa Kilimo ni muelewa kujua kwamba mikarafuu Zanzibar imepungua sambamba na minazi vile vile imepungua kwa wingi sana inaanza kupotea.....

Mhe. Spika: Waheshimiwa tusikilizane.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Tunaelewa kwamba mikarafuu imeanza kupungua mkachukua juhudi kubwa sana ya kuotesha miche na baadae mkawapa wananchi.

(a) Je, Wizara ya Kilimo itakuwa na mpango gani kuotesha miche ya minazi ya asili na kuweza kuigawa bure kwa wananchi nao wakafanye mikakati maalum ya kuirudisha minazi Zanzibar ili kuweza kupata viwanda vyake vikaweza kujirudia kama ilivyokuwa zamani.

(b) Suala la hili la wizi la miche ya minazi mnachukua hatua gani kwa sababu mambo kama haya yanapatikana hata katika mashamba ya wakulima bianfsi. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza kwa sasa hivi sera ya serikali kuwapatia pembejeo bure au kwa msaada mkubwa tumezianisha katika pembejeo maalum la kwanza ni mikarafuu. Mikarafuu tumeigawa bure na hatua ya pili ya minazi mpaka sasa hivi haifikiwa kwamba tuitoe bure lakini tunachofanya tunazalisha mbegu za kutosha ili tuweze kuwauzia watu kwa bei ambayo wanaimudu kwenda kupanda. Mimi nataka niwapongeze wale wakulima wote ambao wamejitahidi sana kuchukua minazi kwenda kuipanda.

Lakini lazima tukubali kwamba tumepungikiwa sana na idadi ya minazi tulikuwa na minazi si chini la milioni tano na laki tano, sasa hivi tuna minazi isiyozidi milioni mbili na laki saba. Kwa hivyo, nasema kiwango cha kupungua ni kikubwa sana. Lakini moja ambacho imesababisha kupungua ni ukataji wa minazi vile vile, ukiangalia watu wetu sasa hivi wanavyokata minazi kama kwamba hatuihitaji minazi.

Kwa hivyo, *speed* ya kupanda tunapata lakini na *speed* ya kukata imekuwa kubwa sana. Kwa hivyo, mambo yote mawili mimi ningeomba tukayazingatia.

La kwanza tutajitahidi kuotesha mbegu za miche watu wapande, lakini kwa sasa hivi hatuwezi kutoa bure. Mimi nafikiri mtu akinunua anakidhamini kile alichokinunua kuliko akipewa bure.

Lakini la pili tujitahidi vile vile kile ambacho kimeshapandwa basi tukitunze, watu wasikate minazi ovyo, ukataji wa minazi ovyo umekuwa mkubwa sana kiasi cha kutisha kabisa. Mimi ningeomba tushirikiane na viongozi wote masheha na kadhalika kudhibiti hali hiyo.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru Mhe. Spika, mimi nimuulize Mhe. Waziri na pamoja na majibu yake mazuri, kwamba kuna maneno kuwa minazi hii ambayo imekuja ya kisasa ambayo tunaitumia sana kwa muda mfupi inazaa haraka lakini inatumia muda mfupi, kwamba ilipofika hapa pamoja na kuunganishwa na minazi yetu ndio imekuwa sababu kubwa ya kuwa minazi yetu haizai.

Sasa namuuliza Mhe. Waziri kwamba je, umefanyika utafiti kuwa minazi mikubwa ile ya asilia ambayo inakaa muda mrefu na hii minazi midogo ukiichanganya kwamba ile minazi midogo eti inakufa haraka, eti kuna *element* fulani kwamba inaua uzima au ubora wa minazi ile mirefu. Lakini kama ni kweli au sio kweli, ni utafiti gani tuliofanya katika kuleta minazi ambayo haichukui muda mrefu kuishi.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Suleiman Sarahan Said kama ifuatavyo. Hakuna taarifa za kisayansi zinazosema kwamba mnazi mrefu au mnazi mfupi mmoja unamuua mwenzake, hakuna taarifa za kisayansi mpaka sasa hivi tuliyonayo sisi, kwamba pale ambapo tuna mnazi mrefu tukapanda mfupi basi ule mfupi au mrefu umemuathiri mwenzake. Mimi mpaka sasa hivi taarifa za kisanyansi sina, lakini nitaweza kuzifuatilia ili tujuwe uhakika wa hilo unalolisema na hapa kwenye meza sina, lakini nasema nitakwenda kuzifuatilia kama zipo, basi tutazileta hapa na tutawaambia, hapa sina. bride

Ila minazi hii ya kisasa Mhe. Spika, bado kwa sisi Wazanzibari nafikiri ndio peke yake inaweza kutusaidia. Suala la *hybrid* hizi zinazofanyika ni tafiti zinazofanywa ili kuonekana kwamba minazi mifupi inaweza ikazaa sana na kwa muda mfupi na ndio maana serikali ikakubali hiyo teknolojia kufanyika. Lakini kwa bahati mbaya imeonekana kabisa katika kipindi cha miaka 10 mpaka 15 minazi hii huwa haiwezi kuzaa tena. Kwa hivyo, bado nafikiri ile *self control* tunayoifanya, nafikiri ndio inaweza kutusaidia kutuendeleza katika kizazi kijacho mbele ya safari. Hii *hybrid* tuliyoifanya bado haijaleta matunda mazuri, matunda yake ni makubwa mafupi sana, mimi mwenyewe bahati nzuri nimepanda baada ya miaka 15 inaondoka. Kwa hivyo, nafikiri ni bora turudi kwenye *self control* mradi tuifanyie utafiti wa kutosha iweze kuzaa vizuri zaidi.

Mhe. Spika: Ahsante. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil nimekuona kwa swali la nyongeza.

Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kuniona. Mimi Mhe Spika, nitapenda kujua juhudi za mikarafuu. Upande wa Kusini kijiji cha Muyuni ni miongoni mwa kijiji ambacho kinakubali mikarafuu kwa ukanda huu, kwa ukanda wa Kaskazini inaeleweka. Katika miaka ya 16 nyuma tulipoweka juhudi za upandaji wa mikarafuu na matokeo yake yalikuwa mazuri. Sijui wizara ina mpango gani ile *moral* ya kupanda mikarafuu katika kijiji cha Muyuni iendelee pale ili zao lile liweze kukua zaidi kimapato na wananchi wa Muyuni wafaidike na zao lile na serikali itie *support* yake, ardhi yake kimaumbile inakubali sana tena. Kwa hivyo, Mhe. Spika, nataka kujua tu mpango wa serikali.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika. Mhe. Spika, kuna agizo la Rais baada ya kugundua kwamba mikarafuu Zanzibar iko michache sana ukilinganisha na Pemba, ameiangiza wizara ihakikishe kwamba tunaotesha miche ya kutosha na yale maeneo yote ya Unguja ambayo yanaweza yana rutuba nzuri ya kupanda mikarafuu tufanye.

Kwa hivyo, sio hilo eneo ambalo unalisema tu, tutayapitia maeneo yote ambayo yana rutuba na nafikiri mikarafuu inaweza kustawi tuweze kuipanda tuwe na mikarafuu mingi kama vile ambavyo tunayo Pembea.

Hiyo programu tunayo na sasa hivi tunapanga kupita katika maeneo hayo kuratibu kujua ni mikarafuu mingapi tunaweza tukapanda katika maeneo hayo. Nataka niwashukuru sana wale wananchi ambao tayari wameanza Kaskazini kuanza kupanda mikarafuu na wameitunza sana, mkarafuu kwa bahati mbaya haupendi sana kuchanganywa na miti mingine, ukichanganya na miti mingine maisha yake yanakuwa mafupi sana.

Kwa hivyo, naomba tutumie teknolojia ya kisasa na taaluma tutakayoitoa ili tupande mikarafuu kwa wingi hii ni *asset* kwa Wazanzibari, ndio uchumi wetu miubwa unategemea karafuu, naomba tuendeleze.

Nakubaliana na wewe kabisa kuna haja ya kuangalia maeneo hayo ili tuweze kupanda mikarafuu.

Nam. 180

Kodi Kubwa Kwa Wachimba Mchanga

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Mhe. Spika, hili swali limegusa wananchi na wananchi wanakabiliwa na sikukuu na pesa nyingi zinapotea kule karibu milioni 10 kwa siku nilivyopata taarifa, nilikuwa niliondoshe lakini naomba serikali ilijibu swali hili hivi sasa. Niko tayari na wananchi hasa wa Donge kwenye wakereketwa wengi wa CCM wanatarajia ushindi 2020 panapo uhai.

Kumekuwa na malalamiko kutoka Jumuiya wa Wachimba Mchanga kuwa kodi ya kuchimba rasilimali hiyo imekuwa kubwa na wao kushindwa kumudu gharama zake.

Je, kwa nini Serikali imepandisha kodi ya uchimbaji wa mchanga na kuwaumiza wananchi wanyonge.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo, Maliasili na Uvuvi - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa niaba yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 180 kama ifuayavyo:-

Mhe. Spika, kwanza nachukua fursa hii kulikumbusha Baraza lako Tukufu wakati akilifunga Baraza hili tarehe 3 Machi 2017 Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Balozi Seif Ali Iddi, alisema kuwa kuanzia sasa serikali itaweka utaratibu mpya wa uchimbaji wa mchanga nchini. Kwa mnasaba huo na kwa ruhusa yako naomba niuainishe utaratibu huo ili Wajumbe wa Baraza lako tukufu, wanajumuiya wanaochimba mchanga na wananchi wote kwa ujumla waweze kuufahamu.

Kwanza Mhe. Spika, suala la uchimbaji wa mchanga, serikali imeamua na kuweka utaratibu mpya wa uchimbaji wa mchanga kama ifuatavyo: -

(a) Uchimbaji wa mchanga usimamiwe moja kwa moja na serikali badala ya wananchi.
(b) Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji na Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira zipange utaratibu wa kuchimbwa mchanga chini ya usimamizi wa serikali.
(c) Kuanzia sasa maeneo ya kilimo yasiruhusiwe tena kuchimbwa mchanga.
(d) Wizara iandae zamu za magari kuchukua mchanga, ili kupunguza msongamano wa magari huko shimoni.
(e) Ufanyike utafiti wa kiwango cha mchanga uliopo katika eneo la Kiwanda cha Sukari - Pangatupu, eneo la Kichwele na maeneo mengine na kuangalia kama upo kwa wingi gani na kama unafaa kwa kazi za ujenzi.
(f) Wizara itangaze rasmi bei ya mchanga unaouzwa sokoni ili kuepusha ongezeko la bei ya mchanga lisilo la lazima.
(g) Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Wizara ya Maji, Ardhi Nishati na Mazingira na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji iandae mwongozo

wa uagiziaji wa bidhaa za ujenzi, ikiwemo mchanga, kokoto, kifusi na mawe, zitakazoingizwa nchini kutoka nje ya Zanzibar.
(h) Wizara ifuatilie taratibu zilizotumika katika kuuza maeneo ya kilimo kwa ajili ya kuchimba mchanga ili kubaini kwa kina ujanja unaotumika kuyabadilisha matumizi maeneo ya kilimo na kudhibiti hali hiyo isiendelee.
(i) Serikali haitolazimika kulipa fidia kwa wamiliki wa maeneo yaliyoidhinishwa kuchimbwa mchanga itapoamua kuchimbisha mchanga huo chini ya usimamizi wake isipokuwa kwa mazao ya kilimo na mali zilizomo ndani ya eneo hilo.

Mhe. Spika, maamuzi na maelekezo hayo ya serikali yameanza kutumika kuanzia tarehe 6 Machi 2017 katika eneo la Donge-Chechele. Maamuzi na maelekezo hayo yamechukuliwa kwa nia njema ya kudhibiti mambo yafuatayo:

(1) Ukiukwaji wa Sheria ya Hakimiliki ya Ardhi
(2) Ukiukwaji wa Sheria ya Uhaulishaji wa Ardhi
(3) Ukiukwaji wa Sheria ya Usimamizi na Uhifadhi wa Rasilmali za Misitu
(4) Ukiukwaji wa Sheria ya Mazingira
(5) Ukiukwaji wa Sheria ya Ulipaji Kodi

Mhe. Spika, matokeo ya ukiukwaji wa sheria hizo

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kuhusu utaratibu.

Mhe. Spika: Naomba ukae aendelee kujibu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kanuni Mhe. Spika, ndio inayotuongoza. Sio maneno yangu kanuni, waziri anatakiwa ajibu kwa ufupi na kwa ufasaha.

Mhe. Spika: Naomba ukae. Natambua uwepo wa kanuni mheshimiwa naomba ukae. Mhe. Waziri endelea.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo, Maliasili na Uvuvi: Mhe. Spika, niliomba idhini kwanza ya kutoa maelezo kabla ya kujibu swali.

Matokeo ya ukiukwaji wa sheria hizo nilizozitaja hapo juu, kumepelekea kuwepo kwa mauziano holela ya ardhi, ukataji wa miti muhimu ya kiuchumi, uharibifu mkubwa wa mazingira, mabadiliko ya ovyo ya matumizi ya ardhi na wafanya baishara ya mchanga kukwepa kulipa kodi stahiki serikalini.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi. Sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifatavyo:-

Mhe. Spika, naomba waondoe hofu wanachama wa Jumuiya ya Mchanga na wananchi kwa ujumla juu ya kuongezeka kodi ya mchanga, kwani kuanzia tarehe 6 Machi 2017 uchimbaji wa mchanga umekuwa ukisimamiwa na serikali kupitia Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka. Kwa kipidi chote ambacho uchimbaji wa mchanga uliokuwa ukifanyika hapo nyuma, serikali

haijawahi kutoza kodi yoyote. Kwa maana hiyo, sio sahihi kusema kuwa serikali imeongeza kodi.

Mhe. Spika, hata hivyo, kwa mara ya kwanza tangu uchimbaji wa mchanga uanze nchini, serikali imeanza kutoza kodi ya stempu kuanzia tarehe 6 Machi 2017. Aidha, kodi hii haihusishi kabisa na uchimbaji wa mchanga lakini inagusa moja kwa moja usafirishaji wa mchanga huo.

Mhe. Spika, wasafirishaji mchanga, ambao ndio wauzaji wa mchanga, wanatakiwa kulipa kodi ya stempu ya asilimia 3 ya bei ya mauzo kwa mujibu wa Sheria ya Bodi ya Mapato. Kodi hii haikuongezwa na haikutozwa hapo awali kama Sheria ya Bodi ya Mapato ilivyotaka. Kodi ya Stempu ni kodi inayotakiwa kulipwa na mfanyabiashara yoyote anaefanya biashara hapa nchini.

Mhe. Spika, katika mwezi wa Machi, jumla ya tani 75,000 zilichimbwa katika eneo la Donge Chechele na kuingiza mapato ya serikali ya jumla ya shilingi 536,856,820/-, kati ya hizo shilingi 51,142,626/- ni kodi ya stempu. Katika mwezi wa Aprili, tani 51,000 zilichimbwa ambazo ziliingiza serikali mapato ya shilingi 366,278,100/-, kati ya hizo 34,929,200/- ni kodi ya stempu. Hivyo, katika kipindi cha miezi miwili ya uchimbaji chini ya usimamizi wa serikali, jumla ya shilingi 86,071,826 zimekusanywa kama kodi ya stempu, kodi ambayo wasafirishaji wa mchanga walikuwa hawailipi. Naomba nirudie kwa msisitizo kuwa serikali haikuongeza kodi katika uchimbaji, bali sasa inatoza na kukusanya kodi ya mauzo ambayo ilikuwa haitozi hapo nyuma.

Mhe. Spika, napenda kulijuulisha Baraza lako Tukufu kwamba, serikali katika suala hili la uchimbaji wa mchanga, imejipanga sawa sawa katika kuhakikisha mapungufu yaliyojitokeza hapo awali hayatajirudia chini ya usimamizi wake. Katika mauzo ya mchanga shilingi 6,500 kwa tani, kabla ya yapo ilikuwa ni shilingi 6000, serikali imeongeza shilingi 500 kwa ajili ya kukarabati eneo linalochimbwa mchanga. Serikali inayagawa mapato hayo kama ifuatavyo:

(1)	Ada ya Uchimbaji	Sh. 1,500
(2)	Ada ya Halmashauri	Sh. 1,000
(3)	Ada ya Kurekebisha eneo	Sh. 1,500
(4)	Ada ya Usafirishaji	Sh. 1,000
(5)	Fidia kwa mazao ya kilimo	Sh. 1,000
(6)	Gharama za uendeshaji	Sh. 500
	Jumla kwa tani 1	**Sh. 6,500**

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe, watakubaliana nami kuwa katika uchimbaji hakuna kodi iliyoongezwa na mgao wa mapato ya uchimbaji umezingatia mambo yote ya msingi. Naomba kuwaomba wajumbe wa Baraza lako tukufu kusaidia kuwaelimisha wananchi kuwa serikali haijaweka na wala haijaongeza kodi ya uchimbaji. Aidha serikali haijaongeza bei ya mchanga, lakini ukweli ni kuwa bei ya mchanga machimboni imepungua kwa faida ya wananchi na watumiaji ambapo wasafirishaji wanatakiwa walipe kodi ya stempu kama wanavyopewa wafanyabiashara wengine. Nakushukuru sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Waziri majibu ya swali hili yamekuwa marefu mno, yaani ingepaswa kuja kama ni taarifa ya serikali naona kuliko jawabu, yaani robo saa nzima imechukua majibu tu.

Nashindwa hata kuwapa watu nafasi kwa ajili ya maswali ya nyongeza kwa sababu ya muda ambao tunao. Kwa hivyo, nitamruhusu mtu mmoja tu mwenye swali la msingi. Mhe. Mjumbe naomba ukae. Nitamruhusu Mhe. Jaku Hashim Ayoub mwenye swali lake la msingi ili aulize swali la nyongeza halafu tutaendelea.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, hili swali limegusa wananchi, kama tungeliacha hata likaja kwenye *Order Paper* ya kesho sio vibaya, maana yake limegusa wananchi hili. Mimi ushauri wangu huo.

Lakini baada ya Mhe. Waziri kujibu, hakujibu swali la msingi kama inavyotakiwa, ni kosa kubwa alilolifanya. Huku anasema kodi hazikupanda na huku mchanga tunaona ni wa gharama umepanda, na tumepitisha stempu ni lini humu Baraza la Wawakilishi ya mchanga *stamp duty*, hebu aniambie Mhe. Waziri ni lini tulopitisha sheria humu, sheria zote humu zinakuja ndani ya Baraza la Wawakilishi, aniambie sheria hii ya mchanga imekuja lini kuhusu *stamp duty*.

Mhe. Spika, tunawadanganya wananchi. Aniambie tu Mhe. Waziri *stamp duty*. Hapa tuna mswaada unakuja wa *stamp duty* ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, leo au kesho. Lakini *stamp duty* ya mchanga imekuja lini, huku anasema serikali haijapandisha mchanga na huku mchanga umepanda tunamdanganya nani. Waziri hamfanyi wajibu wenu. Sisi tuna macho akili zetu timamu kila mtu. Sasa kuna kijiko kule Mhe. Spika

Mhe. Spika: Swali lako mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mimi ninachokuomba ungeunda Kamati Teule ya Baraza ikaenda ikaona hali halisi ilivyo, wanaumia wananchi. Suala hili linatutesa siku zote tutachoipanda ndicho tutakachokivuna wananchi wanaumia, watu wana hati miliki ya ardhi yao wamenyang'anywa. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Swali lako. Naomba hilo swali lako mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Swali langu, kodi za stempu katika usafirishaji wa mchanga umepitishwa na nani, katika kodi hizi kwenye sheria za Baraza la Wawakilishi na lini. Swali langu hilo tu anijibu. *(Makofi)*

La pili serikali haijajibu swali la msingi kwamba ada zilizokuwepo vibali vya Halmashauri vimetoza usafirishaji wa mchanga, wakati serikali inakataa na huku mchanga umepanda bei, which is which. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo, Maliasili na Uvuvi: Mhe. Spika, kwanza niseme tu *Stamp Duty Act* tumepitisha kwenye Baraza hili la Wawakilishi na biashara yoyote inayofanywa nchini inatakiwa itozwe *stamp duty*. Kisheria hawa watu walikuwa hawatozwi *stamp duty*, serikali imesema tulikuwa hatutozi sasa tunatoza kodi yetu na *stamp duty* kwa mujibu wa sheria ni biashara, mchanga ni biashara na kitu chengine chochote ni biashara.

Kwa hivyo, sheria ipo ni kwamba ilikuwa haitekelezwi, sasa serikali inatekeleza sheria kama inavyopasa basi.

La pili, Mhe. Spika, kabla ya mchanga huu haujasimamiwa na serikali bei yake ilikuwa ni shilingi 6,000, serikali imeongeza shilingi 500 kwa ajili ya ku-*rehabilitate* yale maeneo ni shilingi 6,500. Tani moja ya mchanga pale shimoni inalipwa shilingi 65,000. Gari ya tani 10 ni shilingi 65,000. Wao wamepewa bei elekezi ni shilingi 220,000, wanapata faida ya shilingi 148,000 kwa *trip* mbili wanazofanya, ukitoa shilingi 70,000 za mafuta wanabakiwa si chini ya shilingi 78,000 kwa *trip* moja. Akifanya *trip* mbili ni kiasi gani, hizi hazitozwi kodi. Tena kama mnataka tuwe *serious* hata hizi pesa zingetakiwa zitolewe kodi nazo, serikali imefanya hivyo. Wenyewe wanapandisha bei wanauza shilingi 400,000, wanatengeneza shilingi 245,000, hivyo ndivyo wananchi wanavyofanya Mhe. Spika.

Mhe. Spika, serikali imeweka bei elekezi shilingi 225,000 wao wanauza shilingi 400,000, serikali ina kosa gani hapo. Waheshimiwa Wajumbe, tunaomba tuheshimu sheria na taratibu. Lakini uharibifu wa mazingira ulioko kule hekta 560,000 zimeharibika. Leo serikali imetenga fedha ziende ku-*rehabilitate* yale maeneo ili tupande tena miti angalau paweze tena kutumika. Wananchi wale maskini wamekuwa maskini, ukisoma ile *house budget survey* ndio wamekuwa maskini kwa sababu maeneo yote ya kilimo yametumika. Serikali inasema sasa maeneo haya tulime, tuyarudishe ili yaweze kutumika vizuri.

Mhe. Spika, tatizo liliopo wafanyabiashara hawataki kwenda. Hao wenye magari nimekutana nao tumefunga mahesabu wameshindwa ku-*prove* hesabu zao, ukifanya *trip* mbili unapata matokeo yake. Serikali imekuwa wazi, imeweka na kamati kama mtu ana tatizo lolote aje kwenye kamati tutamsikiliza na tutamsaidia Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Waziri. Waheshimiwa Wajumbe, hili swali litachukua karibu nusu saa na bado tumebakiwa na muda mfupi sana na kuna maswali mawili yamebaki. Nashawishika tuendelee.

Nam. 59

Fidia Kwa Wananchi wa Kibele na Bungi Wakati wa Ujenzi wa Barabara ya Tunguu

Mhe. Simai Mohamed Said - Aliuliza:-

Kwa kuwa wapo wananchi wamejenga katika maeneo ya barabara kutoka makutano ya Barabara ya Tunguu (*Junction*) na kuelekea Kaebona.

Je, Serikali imepanga kuwafidia vipi siku za usoni, wananchi wa Kibele na Bungi wakati itakapopanga mpango wa kupanua barabara.

Mhe. Spika: Samahani, umeliondosha.

Mhe. Simai Mohamed Said: Hapana nimeomba lijibiwe Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 59 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, mnamo mwaka 2012 serikali ilipitisha marekebisho ya sheria ya barabara (*Road Decree chapter 134*) moja ya vifungu vilivyofanyiwa marekebisho ni kifungu 18 cha sheria mama sehemu ya nyongeza 23A(2) kinachoainisha daraja la barabara (*road classification*) na eneo la hifadhi ya barabara kutoka katikati ya barabara kwa pande zote mbili kama ifuatavyo:-

i) Barabara kuu (*Main/trunk road*) ni mita 15;
ii) Barabara za Vijijini (*Secondary/Rural roads*) ni mita 12;
iii) Barabara za mchepuko (*Distrct/Feeder roads*) ni mita 10, na
iv) Barabara mpya zinazojengwa eneo la hifadhi kama itakavyoamua idara inayohusika na barabara.

Mhe. Spika, barabara ya Mwanakwerekwe-Makunduchi kupitia Tunguu *junction*, Kibele, Bungi na Kaebona ni barabara kuu. Kwa mantiki hiyo eneo la hifadhi haruhusiwi kwa mtu yeyote yule kujenga wala kupanda miti ya kudumu ndani ya eneo la mita 15, kufanya hivyo ni kutenda kosa kwa mujibu wa kifungu 19(2) cha Sheria ambapo adhabu yake ni kulipa faini isiyopungua T. Shs. 500,000/= na kifungo cha miezi 12 jela au vyote kwa pamoja.

Mhe. Spika, suala la kuvamia eneo la hifadhi ya barabara haliwahusu wananchi wa Kibele na Bungi peke yake au jimbo la Tunguu peke yake bali inahusu watu wa aina hiyo kwa nchi nzima yaani Unguja na Pemba, hivyo basi kikundi cha watu taasisi yoyote ya mtu yoyote aliyejenga nyumba, kibanda, maskani au kupanda miti ya kudumu ndani ya eneo hilo la hifadhi ya barabara nililolitaja hapo juu kuanzia mwaka 2013 atakuwa ametenda kosa kwa mujibu wa sheria hii na anastahiki kuchukuliwa hatua za kisheria, vyenginevyo kwa kuepuka hasara na usumbufu utakaojitokeza hapo baadae. Majengo hayo wayavunje kwa gharama zao na Serikali haitalipia fidia kwa yoyote pamoja na miti ya kudumu mazao chochote kilichojengwa ndani ya maeneo hayo wakati inapotekeleza miradi ya ujenzi au matengenezo ya barabara kwa maendeleo ya nchi na faida ya wananchi walio wengi.

Mhe. Spika, kupitia Baraza lako hili tukufu nitoe wito kwa Wakuu wa Mikoa, Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya, mabaraza ya Miji, Manispaa, Masheha na wananchi wote nchini kusimamia na kuhakikisha kuwa maeneo ya hifadhi ya barabara zote hapa mimi kwa kujenga majengo na kupanda miti ya kudumu na mazao, kufanya hivyo ni kukiuka sheria tulizojitungia wenyewe lakini baya zaidi ni kuwa Serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi sana za kulipia fidia majengo, miti na mazao kwa faida ya watu ambapo kama fedha hizo zingetumika kwa miradi mingine ya maendeleo wananchi wengi wakafaidika. Vile vile napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza na kumshukuru sana Mkuu wa Mkoa wa Mjini wa Magharibi ameanza kusimamia hili.

Mhe. Spika, Wizara yangu imeanza kuweka nguzo kwenye mikapa ya hifadhi za barabara hata hivyo kuna watu wachache wenye kujali maslahi yao binafsi kwa makusudi kabisa wamekuwa wakiving'oa viguzo hivyo, ama kwa kuviuza viwanja au kujenga majengo yao hasa kwa upande wa Unguja, barabara zilizowekewa viguzo kwanye mpaka wa hifadhi ya barabara ni Amani/Dunga, Mfenesini/Bumbwini, Amani/Mtoni na Mazizini hadi Fumba. Wizara yangu

imepanga kufanya zoezi la kuhakiki kwa kuweka alama maalum kwenye mipaka ya maeneo ya hifadhi ya barabara kwa kila daraja au barabara kwenye mwaka wa fedha 2017/2018 ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri aliyoyatoa Mhe. Waziri kwanza niseme amekiri kwamba sheria hii ambayo iliyokuja ya mwaka 2012 ambayo ili-*replace ya road decrew* ya *chapter* No. 134 na kifungu hicho 18 kwamba wapo watu ambao walikuwa wamejenga kabla ya hapo. Sasa suala langu ni hili ?

a) Ni utaratibu gani utakaotumika hasa kuyalinda maeneo ya hifadhi kwa mfano katika Bungi Miembe mingi lakini pia pale pana uwanja wa mpira, ili kuhakikisha kwamba yale maeneo yaliyokuwepo ya kihistoria kabla hawaathiriki na pia wanapata *compensation* ya Serikali ipasavyo kwa sababu sheria ilikuwa bado haitumiki.

b) Katika Shehia yangu ya Dunga Bweni wakati inajengwa barabara ya Dunga kuelekea Kinyasini wapo wananchi waliathirika na hadi hivi leo wana claim zao kwamba hawakulipwa mazao au vipando vyao na ardhi yao pia iliyotumika katika mambo mbali mbali.

Sasa Mhe. Spika, ningependa nipate majibu sahihi juu ya haya masuala yangu mawili kutokana na suala mama ambayo majibu aliyoyatoa.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Kama nilivyosema mwanzo utaratibu tunaoendelea kuutumia ni utaratibu ule ule ambao tumeueleze katika sheria yetu kwa hivyo sisi tunahakikisha kwamba tunafuata hii sheria na iwapo itakuwa jengo lote limeingia ndani ya hifadhi yetu basi wakati wa ujenzi wa barabara sisi tutachukua hatua ya kulihamisha hilo jengo.

Kama nilivyosema hapo kabla kwamba tunalipa fidia kwa mujibu wa taratibu na kama kuna watu wake walioingia katika utaratibu huu hawajalipwa fidia basi mimi nitamuomba tukae pamoja anipe orodha ikisha nifuatilie Wizarani Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Spika, na mimi nimuulize Mhe. Waziri kwa majibu yangu yenye (a) na (b). Mheshimiwa Waziri amezungumza hapa kwamba barabara ina kipimo chake na kila kitu kina kipimo cha barabara pamoja na eneo la hifadhi, lakini mpaka leo Serikali ikitaka kujenga barabara bado kuna malipo ambayo yanalipwa na wakati ambapo kipimo kile kimeshaidhinishwa tokea zamani suala linakuja.

a) Ni mpaka siku utakayoweka viguzo kuonyesha hapa ndio alama ya mwisho ndio itakuwa Serikali imeweka alama ya barabara au ni kwamba mtu ambae atakuwa amefuata barabara katika kipimo kile ndio itakuwa sahihi.

b) Kwa nini Serikali inalipa mafao ya hifadhi ya barabara wakati ambapo mtu anajua sheria ya barabara.

Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye kifungu (a) na (b) kama ifutavyo.

Kama nilivyosema mwanzo sisi tunaendelea kutoa wito kwamba watu wafuate taratibu zinazotakiwa wakati wa kuomba viwanja kujenga au kufanya hatua yoyote ile mfano ya kupanda vipando, Wakuu wa Mikoa vile vile na watu wa upimaji tunawaomba sana wanapotoa vibali basi waangalie kwamba kwa sababu mfano Wakuu wa Mikoa wao ndio wanaoanza kutoa vibali kupitia Masheha mpaka Wadi na baadae kuja katika Wizara ya Ardhi kwa ajili ya Viwanja. Mimi nitatoa wito tu kwamba watu wafuate taratibu na sisi tunasisitiza kwamba yoyote atakayejenga ndani ya chanzo cha barabara baada ya sheria hii kupitishwa hatutomlipa fidia, kwa hivyo namjibu na jibu lake (b) kwa pamoja. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 170

Kuibuka kwa Usafiri wa Boda Boda Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Hivi karibuni Zanzibar kumezuka usafiri wa Boda boda katika maeneo mbali mbali ya Wilaya ya Mjini, ambapo sio jambo baya kwa vile vijana wetu wengi wanapata kujiajiri. Hata hivyo, imeonekana hakuna udhibiti wa shughuli za bodaboda Zanzibar kama vile abiria kuvaa kofia ngumu (*helmet*), kofia nyengine zikiwa chini ya kiwango cha usafi na kuhatarisha afya za watumiaji, baadhi ya matendo ya uhalifu yakitumia usafiri huo na kupuuza sheria za usalama barabarani.

(a) Je, Serikali inatambua usafiri wa Boda boda kama moja ya vyombo rasmi vya kupakia abiria.

(b) Usalama wa barabarani wanachukua hatua gani kudhibiti vitendo vya uvunjaji sheria ya boda boda.

(c) Suala la afya za watumiaji linazingatiwaje kwa watumiaji wa boda boda.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 170 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Usafiri wa Boda boda kwa Zanzibar haujaruhusiwa kwani chombo cha maringi mawili kinaruhusiwa kwa matumizi binafsi na biashara ya kukodisha kwa kuendesha mwenyewe. Hivyo Serikali haitambui usafiri wa boda boda kama ni biashara rasmi ya kusafirisha abiria kwa njia ya biashara.

(b) Usalama barabarani huchukua hatua za kuwakamata wote wanaofanya biashara bila ya kuwa na leseni za biashara hiyo na kuwapeleka mahakamani kwa mujibu wa sheria yetu.

(c) Afya za abiria na usalama wao ni miongoni mwa sababu zilizoifanya Serikali kutoruhusu usafiri wa Bodaboda hapa Zanzibar.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, Serikali imeshatoa *order* kuwa usafiri wa boda boda haujaruhusiwa.

Je, kwa nini atunashuhudia mbele ya macho yetu usafiri huu ukiendelea na Serikali ipo na hakuna hatua zinazoendelea, au ilikuwa zoezi maalum tu kama wale ng'ombe wa mjini waliokuwa wakikamatwa na kuwaachia wenye bodaboda.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:

Kama unavyojua katika kumkamata mtu wa bodaboda unahitaji lazima na yule aliyepakiwa akiri, imekuwa tunapata wakati mgumu kwa sababu yule anayepakiwa huwa hataki kutoa ushirikiano na sisi. Lakini hata hivyo tumekuwa tukishikana na Jeshi la Polisi kuhakikisha kwamba tunatumia mitego yetu katika kuwakamata hawa wahusika mpaka pale hii biashara tunavyosema kwamba haijaruhusiwa basi hawa watu huwa tunawakamata kwa mitego maalum.

Tunaendelea kufanya zoezi la kushtukiza na la kawaida na pale tunapowapata hawa watu tunakuwa na uthibitisho basi adhabu zinapelekwa mahakamani na zinachukuliwa sheria kwa ajili ya wahusika.

Mhe. Abealla Maulid Diwani: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri napata ukakasi katika suala hilo, kwa sababu suala hili nilikuja kuliuliza nyuma Waziri wa Nchi Afisi ya Rais alisema sio taratibu lakini Serikali imeruhusu usafiri ule kwa sababu unasaidia wananchi wetu.

Je, tushike lipi katika hili?

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Waziri siku ile alisema kwamba wataangalia kama kuna uwezekano wa kuiruhusu hii biashara, alisema tutaangalia hakuruhusu moja kwa moja kwa mujibu wa sheria yetu namba 7 ya 2003 mpaka sasa hivi kifungu 48 mtu anaruhusiwa kufanya biashara kwa mujibu wa zile aina alizoziweka. Kwa hivyo bodaboda haimo katika sheria yetu Namba. 7 ya 2003 kifungu cha 48.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Spika, ahsante kwa kuniona pamoja na majibu ya Serikali yenye kigugumizi naomba kuuliza suala dogo sana la nyongeza.

Kwa sababu usafiri huu sasa umekuwa ni maarufu na wananchi wengi wenye kipato cha chini wanatumia, Serikali ina ukakasi gani kule kubadilisha sheria yake ili kuweza kuwaruhusu na kuwapatia baadhi ya mapato bodaboda.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, napenda kumwambia Mhe. Mohammed Said Mohammed kwamba sisi tunapojibu maswali tunakuwa hatuna kigugumizi tuna sheria hii hapa tunaifuata na tunafuata utaratibu, kwa hivyo mimi namwambia hatuna kigugumizi na pale ambapo tunaona kuna maslahi ya wananchi wetu basi tutaileta tena hii sheria. Lakini hizi sheria tumezitunga ili zifuatwe na tunapokuwa hatukuzifuata nyinyi ndio mnaolalamika hapa.

Mhe. Spika: Ahsante Muda wa maswali umekwisha Waheshimiwa kwa sababu tunataka kuendelea Mhe. Machano Othman Said.

UTARATIBU

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, naomba kutumia utaratibu wa kifungu Nam. 63 cha Kanuni hii na kwa sababu muda umekwenda sitaki kukisoma watu wote wanakijua, lakini utaratibu wangu utaegemea kifungu 42 na kifungu 94 cha kanuni hii.

Mhe. Spika, kifungu 42 naomba kwamba wewe kwa mamlaka uliyonayo uiagize kamati ya Serikali ya Mawaziri wanaoshughulikia mchanga kwamba tukutane nao siku ya Alhamis na baadhi ya Waheshimiwa Wawakilishi, tuzungumzie suala hili kwa sababu linawaudhi sana wananchi hiyo ndio hoja yangu kwa sababu mjadala umekuwa mrefu kwa hivyo tuagize hivyo.

La pili kifungu cha 94 cha Kanuni kinazungumzia matumizi ya Serikali naomba nipate maelekezo yako Mhe. Spika, mimi ni Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini ambae pia nastahiki kupata mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, lakini hadi leo ni Jimbo pekee ambalo halijapata fedha za Maendeleo ya Jimbo na tumebakiza siku karibu nane tu za kumaliza mwaka wa fedha wa bajeti, Je, hii haiwezi kusababisha kwamba watu wa Mfenesini wakose mgao wao na kuingizwa katika mwaka mwengine wa fedha nilikuwa naomba kauli ya Serikali kuhusu hili.

Mhe. Spika: Mheshimiwa kwanza muongozo wangu kwenye hili la mwanzo nakubaliana na wazo lako kwamba tukae na Serikali na baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe ili tuone hili suala la mchanga likoje hasa, limefikia wapi kwa sababu Serikali ilishatoa maelekezo lakini inaonekana yale maelekezo ambayo Serikali ilikwisha kuyatoa hayajafanyiwa kazi kama hivyo inavyopaswa, ndio maana hata majibu ya Serikali hapa leo yalikuwa marefu sana kuhusiana na suala la mchanga kwa sababu bado ni ushahidi tatizo kwamba bado halijaondoka. Kwa hivyo nakubali kwamba tukae siku ya Alhamis tunatafuta muda ili tukae na Serikali ili tuone namna gani tunaweza kukaliweka sawa suala hili la mchanga.

Suala la fedha za jimbo hili nafikiri Wizara ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais inahusika labda nimruhusu Mhe. Waziri sasa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais atupe kinachoendelea, Mheshimiwa ana wasiwasi kwa sababu tunafikia mwisho wa bajeti lakini yeye jimbo lake halijapata kitu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, labda utusaidie tu kwenye hii hoja ambayo amekuja nayo Mhe. Machano labda ungetusaidia muongozo vizuri kwa sababu kwa mujibu wa kanuni ya 37 ya Mhe. Spika, kama jambo hili la mchanga kwanza Mhe. Machano alitaka kuleta hoja binafsi ya jambo hili la mchanga wakati tunapoujadili bajeti ya Wizara ya Kilimo.

Lakini baada ya majibu yaliyotolewa na Serikali mazuri hata yeye Mhe. Machano akaridhika akasema kwa majibu haya nimeridhika na sitoendelea tena na hoja yangu binafsi, haya yaliyofanyika leo maana yake Serikali imeendelea kujibu jambo ambalo tayari imeshalitolea ufafanuzi kwenye mkutano huu huu ambao unaendelea na kanuni zetu zinatuongoza hivyo. Kama kwenye jambo ambalo tayari limeshatolewa ufafanuzi kwenye mkutano ambao unaendelea halitojadiliwa tena ndani ya Baraza.

Sasa labda Mhe. Spika, utuongoze vizuri kwenye jambo hili lakini wenye mijadala ambayo itaendelea ndani ya Baraza kuhusiana na taarifa ambazo zimeshatolewa kauli yake na Serikali.

Mhe. Spika: Mheshimiwa mimi sikutaka mjadala humu ndani na ndio maana nimesema tukae nje tukutane nje na Serikali ili muwaridhishe waheshimiwa kinachoendelea sio humu ndani, hata mimi humu ndani nisingeruhusu mjadala kuhusiana na suala hili kwa sababu ulishafikia pahali lakini inaonekana kuna watu hawatekelezi maelekezo ya Serikali huko nje.

Kwa hivyo ndio tukae ili tuweze kufahamiana na Serikali namna gani bora zaidi ya kuweza kufanikisha lile zuri ambalo walikuwa wameliwasilisha ndio nia yangu hiyo, sasa naomba nimpe Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kuhusu lile la pili la fedha za jimbo.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi lakini pia nimshukuru Mhe. Machano Othman Said kwa hoja zake, lakini nimshukuru Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa maelezo ya kina kuhusu jambo ambalo limezungumzwa.

Mhe. Spika, nianze na suala la mfuko wa jimbo upo kwa mujibu wa Sheria iliyopitishwa na Baraza lako tukufu na katika kila jimbo ambalo limetekeleza taratibu kwa mujibu wa sheria tayari fedha zao zimepatikana, na kwa upande wa Jimbo la Mfenesini ikiwa utaratibu umekamilishwa wa masharti kwa mujibu wa Sheria hakuna shida yoyote ya kupatikana fedha za jimbo kwa jimbo la Mfenesini. Hata hivyo kwa kuwa Mhe. Machano amelilalamikia suala hili nitachukua hatua nionane na watendaji wangu ili niweze kujua kwa kina ni jambo gani lililokwamisha mapaka sasa.

Kwa sababu kila jimbo ambalo limekamilisha utaratibu fedha zinapatikana, niwaombe tu Waheshimiwa Wawakilishi wasimamie vizuri taratibu walizoziweka katika Sheria ili zikamilike na mfuko wa Jimbo huo uweze kutumika kwa wananchi na wananchi wasipate bughudha ili ulete maslahi yaliyokusudiwa. Ni nia na dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba tunawasaidia wananchi wetu katika ile mipango yao katika maeneo yao wanayoianzisha ili kuunga nguvu jitihada hii.

Kwa hivyo nataka nimhakikishie Mhe. Mwakilishi nitafuatilia ili niweze kujua ni lipi limekuwa tatizo kwa upande wake.

Mhe. Spika, masuala ya mchanga kama uongozi wako ulivyoutoa kwa kuwa tayari kama alivyosema Mhe. Mwanasheria Mkuu na utaratibu wetu wa kanuni kuhusu jambo hili, nadhani bado Baraza lako tukufu iwaachie Serikali ifanye kazi yake nzuri kwa kina na majibu yatazidi

kuletwa katika Baraza lako tukufu, kwa sasa bado Serikali inaona jambo hili liko katika uwezo wake ina uwezo wa kulishughulikia na kulimaliza na limezungumzwa vizuri katika vikao vya ndani vya Serikali na Serikali imetoa maelekezo, naamini kabisa kwamba jambo hili kwa sasa bado Serikali ina uwezo mkubwa wa kulimaliza na kuondoa kabisa malalamiko yanayojitokeza.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha ahsante sana.

Utaratibu

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Spika, nasimama kwa kununi ya 63 kuhusu utaratibu lakini na mimi niko 42 naona sina haja ya kuisoma kwa sababu unayo katika hapo na watu wote wanaijua.

Mhe. Spika: Naombe uendelee lakini tafadhali lisihusu mchanga tuendelee.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mheshimiwa *as you now issue* hii ya mchanga ndio *issue* kubwa hapa nchini na mimi ni mjumbe wa wananchi ungeniruhusu kidogo niiseme.

Mhe. Spika: Mheshimiwa tumeshafikia pahali kwenye hili naomba uliache, Mhe. Machano Othman Said.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, …..

Mhe. Spika: Unaendelea na mchanga pia.

Mhe. Machano Othman Said: Naendelea na Jimbo kwanza, pengine Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais hakuwa *aware* sana na huu mwenendo wenyewe ulivyokuwa ukienda, lakini kwa bahati nzuri Naibu Waziri wa Ofisi hii anaijua kadhia yote ilivyo.

Tulivyoanza kupeleka *account number* bahati mbaya sisi wenyewe tulikosea mwanzo baadae tukarekebisha lakini karibu mwezi mmoja nusu kuanzia wakati huo mpaka leo na wakati tunaambiwa kwamba wiki ijayo mtaingiziwa wiki ijayo mtaingiziwa, lakini kwa sababu ya mvua za masika na sisi tukawa hatuna haraka nazo, kwa sababu fedha ukizichukua masika huna la kwenda kuifanyia. Kwa hivyo tukasema ngoja ipite masika halafu tukachukuwe fedha yetu. Sasa Mhe. Spika fedha mpaka leo bado zimebakia siku sita kumaliza mwaka wa Bajeti ndio hofu yangu tusije tukaliwa panga.

Lakini la pili tumepeleka majina ya *account* watia saini kama wenzetu walivyofanya, sisi tumeelekezwa pengine kwa marekebisho ya sheria kifungu 9 cha saini moja awe Mkurugenzi wa Halmashauri na Mwenyekiti wa Kamati ambaye ni mimi, lakini nao pia utaratibu unachelewa. Hofu yangu pia nyengine nataka niweze wazi il *account* inao watia saini wa zamani mpaka leo, tusije tukaingiziwa milioni 20,000,000 zikenda kuchukuliwa halafu likawa jimbo tuna matatizo kwa hivyo yote haya nilikuwa nataka kumwambia Mhe. Waziri wa Nchi ayashughulikie.

Mwisho kabisa Mhe. Spika ukitoa *ruling* inakuwa ndio utaratibu, ushatoa *ruling*

kwamba Alhamisi tukutane sisi na Kamati nje ya ndani ya Baraza kwa hivyo lazima tukutane hakuna tatizo kuhusu hilo jambo la mchanga sio kulihoji humu ndani.

Mhe. Spika: Tushalimaliza nadhani na mimi nimekwisha kuelekeza hivyo sivyo vyenginevyo suala hili la mfuko wa jimbo naomba pia mkutane nje Mheshimiwa ili muweze kulimaliza tusiendelelee nalo hapa. Baada ya maelezo yangu hayo Waheshimiwa kuna tangazo la wageni mgeni wa Mhe. Shadya Mohamed Suleiman ni mshauri katika Kitengo cha Watu Wenye Ulemavu, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Pemba mgeni mwenyewe ni Ndugu Mohamed Othman Omar kama yupo hapo naomba asimame.

Waheshimiwa Wajumbe muda mchache tu unaokuja nitampisha Mhe. Naibu Spika ili aweze kuendelea kuendesha hichi kikao, lakini nitoe indhari tu, hapa leo tuna Mawaziri ambao wameomba kuchangia ni Mawaziri kumi na moja mpaka sasa hivi, Mawaziri kumi na moja kwa maana ya Mawaziri tisa na Manaibu Waziri wawili na pia kuna wajumbe wawili ambao wamebaki Mhe. Mussa Ali Mussa na Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwa hiyo ningeomba tuendelee kwa hiyo kabla sijaita utaratibu wa kuendelea namuomba Naibu Spika aje achukue nafasi.

Mhe. Spika: Mhe. Naibu Spika, karibu sana.

(Hapa Mhe. Naibu Spika alikalia kiti)

HOJA ZA SERIKALI

Mpango wa Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na lijadili na kuyakubali Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2017/2018

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea mchangiaji wetu wa mwanzo atakuwa ni Mhe. Mussa Ali Mussa baada ya Mhe. Mussa atafuata Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Mhe. Mussa karibu.

Mhe. Mussa Ali Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunichagua kuwa wa mwanzo kuchangia hotuba hii. Nimefurahi sana pia namshukuru *Allah Subhana wataala* kwa kutujaalia sote humu Wakilishi tukaamka wazima, pia namtakia maisha marefu na uongozi mwema Mtukufu Rais Dkt. Ali Mohamed Shein pamoja na familia yake kwa uongozi wake mzuri hapa Zanzibar.

Pia Mhe. Naibu Spika, nakata nimpongeze kwa dhati Waziri wa Fedha pamoja na Naibu wake, Makatibu wake wote na Maafisa wadhamini kwa Bajeti ya Serikali nzuri aliyotuletea Bajeti ambayo ni nzuri sana, imezingatia pembe zote hasa kwa wanyonge imeondosha kodi imeweka mambo sawa sawa. Pia nataka nimpongeze mtoto wangu Mwakilishi wa Mpendae Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa) pamoja na wajumbe wake wote, kwa kututengenezea bajeti hii nzuri ambayo kwa kweli roho zetu zote zimefurahika. La mwisho kabla sijaendelea na

mchango wangu nataka niwape pole wale wapenzi wote Dar Yanga African kwa kutukabidhi Nuzima kuja Msimbazi ahsanteni sana wapenzi wa Yanga na poleni. *(Makofi)*

Sasa Mhe. Naibu Spika, naanza na mchango wangu kwenye Bajeti kuu ya Serikali, Mhe. Naibu Spika mchango wangu huu kuhusu Bajeti hii ya Serikali namuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha angalie sana majengo au mradi mkubwa wa Serikali unaosimamiwa na fedha za Serikali. Majengo ambayo yanafanyiwa matengenezo ili kurudia uhalisia wake halisi, majengo haya anapoyaingizia fedha, fedha hizi azifuatilie kwa sababu kumekuwa na uharibifu mkubwa sasa wa fedha za Serikali anapozipeleka na zikawa hazina usimamizi.

Nitatoa mfano kwa Mahakama ya Chake Chake ambayo imefanyiwa ukarabati hata mwaka mmoja bado, hata miezi sita bado imekwenda pale ikafunguliwa na Rais na sisi Wawakilishi tukawepo tukachezeshwa mdumange tukafurahi sana, jengo zuri sana matokeo yenyewe kumbe tumepigwa changa la macho, hivi sasa zile rangi zake zimeshapayuka na jengo lile linavujisha. Ile ni kutokana na usimamizi mbovu ya watendaji waliopita sasa Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri wa Fedha jambo hili aliangalie kwa vizuri sana, kwa upande mwengine kuna jengo ambalo limejengwa Tibirinzi, karibu na ukumbi wa ZSSF mabilioni ya shilingi, pesa za wavuja jasho zimepotea jengo lile halikusimama, halikufaidisha Serikali wala wananchi wa Serikali ya Zanzibar lipo pale na mkandarasi yule ameachwa amekimbia, katuachia jengo ambalo halina faida yoyote kwa Serikali hii, ule ni utendaji mbovu namshauri Waziri afanye kila njia mkandarasi yule akamatwe aletwe nchini aje kwanza aondoshe hatari aliyotuwekea pale ile ni hatari kubwa kwa wananchi wetu jengo lile laweza likaanguka wakati wowote likaelekea barabarani ikawa pana watu watu wakapoteza maisha. Ikabebeshwa Serikali lawama kumbe ule ni uzembe wa mtu binafsi, kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri wa Fedha atakapokuja anithibitishie lini atamleta mkandari yule na tutasaidiana sote wawakilishi wote tumlete mtu yule aje atupe fedha yetu halafu aondoshe pale taka taka zake. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika nikirudi kwa upande wa matumizi mabaya ya fedha za Serikali naenda tena kwenye Soko la Wete Mhe. Naibu Spika, namuomba Waziri aliangalie soko la Wete soko ambalo limepoteza fedha nyingi, likafunguliwa na Rais kwa sherehe na magoma leo Soko lile hali yake liko vile marangi yamepayuka Soko linavujisha, hata mwaka mmoja wa uongozi wa Dkt. Ali Mohamed Shein mambo gani tunayofanyiwa katika fedha za Serikali. Mhe. Naibu Spika, hiyo haiwezekani wala haikubaliki kuchukuliwa fedha za wavuja jasho wakapewa watu wakazitumia visivyo. Pia namuomba Mhe. Waziri wa Fedha atakapokuja hapa anieleze mradi wa barabara kutoka Ole-Kengeja ulioanza 2013 mpaka leo 2017 hatujapata hata kilomita moja iliyowekwa lami, fedha zinatumika ovyo barabara haina kiwango barabara haikubalinki kwa nchi ya sasa na ulimwengu wa kisasa na mahali tunapokwenda. Bararaba ile itumike kwa muda wa mwezi mmoja hauzidi, hivi sasa barabara ile haipitiki.

Fedha nyingi zimepotea Mhe. Naibu Spika, namuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha mtoto wangu angalie sana, matumizi ya fedha za Serikali wakati huu si wakati tena wa kuleana, huu ni wakati wa hapa kazi tumewaona wenzetu Bara wanavyofanyiwa wakati wa kupoteza Serikali mpaka leo asubuhi namsikia mpinzani mkuu wa nchi hii amsifu Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anayoifanya sisi kwa nini tuwafiche wazembe.

Mhe. Naibu Spika, hata barabara ya kutoka Mtambile kwenda Kengeja kwani ile barabara imefika miezi sita, hivi sasa haipitiki nimekwenda juzi na Makamu wa Pili wa Rais, tulipokwenda kukagua majumba yaliyopata mafuriko barabara haipitiki ndani ya miezi sita iweje.

Mhe. Naibu Spika, namuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja anieleze hata ile barabara iliyojengwa na H Yang kutoka Mtambwe Daya kuja Bahanasa imejengwajengwaje barabara imeshapayuka imeshachanika fedha zile ni za Serikali hatuoni kinacho fanyika tunakaa na watu wazembe, tunakaa na baadhi ya watendaji wazembe hata hatuwaangalii hatuwashughulikii fedha zetu zinakwenda ndivyo sivyo. Nina uhakika kabisa Mhe. Naibu Spika, ingekuwa miradi mikubwa ya Serikali inasimamiwa vizuri inapopatiwa fedha na inakaguliwa basi sasa hivi Zanzibar ingelikuwa inan'gara. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nataka nimwambie Waziri ende akaangalie jengo lililojengwa Unguja Ukuu watakaloishi watu walioathirika na madawa ya kulevya akaangalie fedha ya Serikali ilivyopotea, jengo halina kiwango, jengo halina thamani jengo kwa sasa halikubaliki, halikubaliki kwa ulimwengu wa leo. Mabilioni ya fedha yamepotea hivi tukakuwa tunakwenda wapi, bajeti hii inayokuja ni bajeti nzuri na kubwa na rafiki. Tena namuomba Mhe. Naibu Spika namuomba, namuomba sana Waziri wa Fedha azipatie fedha Wizara zote kwa ukamilifu bila ya kuwapunguzia hata senti baadaye tupate kuwakagua tuyaone matumizi ya fedha walivyozitumia. Fedha zetu zinapotea sana sana nchi hii Mhe. Naibu Spika, kwa tunavyokwenda kuoneana muhali, kupendana, ushemegi, hatuwezi kupiga hatua. Hatuwezi kupiga hatua ushemegi tumeufanya mkubwa mapenzi tumeyafanya makubwa.*(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, hapa tunapita tutakwenda kuulizwa jinsi tulivyokuwa tukisimamia fedha za wavuja jasho wa Zanzibar, fedha zinatumika vibaya kwa maana hiyo nataka niseme kwa baadhi ya watendaji ambao hawawezi kuendana na Serikali hii wapumzike watuache tusonge mbele, kwa sababu hatuwezi kuwachumia watu wachache tukaacha kundi kubwa la wavuja jasho masikini wa nchi hii. (Makofi)

Mhe. Naibu Spika, nataka nimwambie Waziri kwamba kuna mambo mengine ambayo nikiyataja hapa ni aibu, aje anione tuyafanyie kazi kwa sababu mali za Serikali zinakwenda vibaya Serikali inakosa mapato na sasa Mhe. Mtukufu Rais ameongeza mishahara, mishahara hii inataka kulipwa kunakuja ajira, ajira hizi zinataka kulipwa Serikali inategemea mapato. Hivi sasa tumepoteza mapato kwa sababu tumepata matatizo ya magonjwa haya ambayo kwa uwezo wa *Allah* kesho na kesho kutwa yataondoka, ukitangaza magonjwa haya unafukuza watalii. Hasa kwa hivyo kipindi hichi ambacho bado hali yetu haijawa nzuri Mhe. Waziri asimamie vizuri fedha za Serikali nafasi hii aliyopewa na Mtukufu Dkt. Ali Mohamed Shein amempa kwa sababu anaiweza na sisi tunakubali anaiweza. Asikubali hata siku moja kukaa na wazembe wakatupotezea fedha ya Serikali, hapo Mheshimiwa nipaache nende kwenye hatua ya pili. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli tuliponunua meli ya M.V Mapinduzi II nilisema sasa Pemba imeshagomboka kiusafiri, lakini kwa masikitiko makubwa sana juzi wananchi wanakata *ticket* kutoka Zanzibar kwenda Pemba meli ika-*cancel* ikapita kwengine watu wanafika bandarini wanaambiwa meli haiendi tena Pemba. Tunarudi kule kule tulipotoka, ili jahazi Mhe. Naibu

Spika linaugunda ndani hili jahazi lina mgunda, tumepanda wengi abiria tumo wengi lakini na mgunda yumo haiwezekani tena analipekecha. Kwa sababu tatizo la mgunda anapokaa chini kazi yake ni kupekecha, hata tukija tukiamka jahazi sasa lishaingia maji tutakwenda wapi. Wewe unawapeleka watu na watoto bandarini wanafika unawambia meli leo haiendi tena na wana *ticket* zao mikononi unafanya nini unafanya Serikali ilaumiwe, unataka Serikali ikose mapato.

Mhe. Naibu Spika, hapo nataka nipaache nende kwenye majengo pamoja na vipando vya wananchi vilivyon'golewa na majengo yaliyoharibika au yaliyovyunjwa wakati wa kupisha njia. Kuna Gando kuna Kiwani Mkoani kuna Ole-Kengeja. Gando huu ni mwaka sita mpaka saba wakati na-*Peruse* vitabu vya Wizara ya Fedha zikuona mahali ambapo pamezungumzia fidia, kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anieleze wananchi wa Gando wananchi wa Ole-Kengeja wananchi wa Kiwani-Mtambile ambao wote hawa wamepoteza majumba yao na vipando vyao watalipwa lini mwaka huu mwaka ujao au hawalipwi tena.

Kwa sababu Mhe. naibu Spika, ninalotaka kukwambia na nataka kumwambia Mhe. Waziri kwamba kuna watu wanafanya mambo makusudi ili serikali ibebe lawama. Masikini ya Mungu uliyemvunjia nyumba yake 2004 mpaka leo mwaka 2017 hujamlipa, ataipenda serikali huyo? Ataichukia serikali na haja yetu sisi ni wananchi, wananchi ndio wanayoiweka serikali kupitia kwa Wawakilishi wao. Wananchi wakapige kura wawachague wawakilishi, wamchague na Rais. Rais asimame achague viongozi, achaguwe mawaziri, achaguwe Naibu Mawaziri na Makatibu Wakuu. Bila ya serikali kusimama hakuna Mkurugenzi, hapana katibu, hapana Naibu Katibu.

Leo wenzetu tumeshawapa madaraka wanatufanyia ndivyo sivyo, tutasema nini sisi. Kama mwananchi nyumba yake imevunjwa zaidi ya miaka minne hajalipwa kesho kutwa tarehe 20 imefika ikimaliza Ramadhani hii Ramadhani ijayo ngoma imeanza. Sasa unamwendea mwananchi nipe kura, atakwambia nyumba yangu uliisemea nini, nilikusikia. Juzi nilisema na leo nasema, kesho kutwa Baraza linafungwa mimi nataka kurudi. Nakwambia tena Mhe. Naibu Spika, mimi nataka kurudi siwezi kuishi Zanzibar sijui kimji, sijui Kiunguja, siwezi kutembea kwa mikogo, sasa nikirudi nitasema nini. Nataka Mhe. Waziri atakapokuja anipe jambo la kwenda kusema nitakapoulizwa juu ya watu majumba yao, mali zao, miembe, minazi, migomba. Nifika tu watu wananingojea bandarini wataniuliza.

Mhe. Naibu Spika, naomba Mhe. Waziri aseme hapa wananchi kule wamsikie kwamba bwana Mwakilishi wenu kasema lakini nitawalipa mwaka huu, tarehe kadha mwezi kadhaa au silipi tena, au nitalipa bajeti ya mwakani. Lakini namuomba Mhe. Waziri wa Fedha atakapokuja jambo hili asilisahau anambiye wananchi wangu wasikie ili na mimi nitapate kurudi kwenye jimbo langu kwa Amani na salama.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa umebakiza dakika mbili.

Mhe. Mussa Ali Mussa: Lakini Mhe. Naibu Spika, mimi ni mzee wako uzee nao uupe nafasi, uzee una nafasi yake.

Mhe. Naibu Spika: Dakika zako ni mbili malizia.

Mhe. Mussa Ali Mussa: Humu ndani ya Baraza hili naona mimi ndiyo naongoza waliobakia wote ni watoto wangu ndugu zangu, mimi o naongoza, kwa hivyo nipe nafasi.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa malizia dakika zako mbili.

Mhe. Mussa Ali Mussa: Haya ahsante Mhe. Naibu Spika. Ninachotaka kusema kumwambia Mhe. Waziri wa Fedha kwamba inapotokezea ya mgambo itakuwa ikilia huwa ina jambo. Tumepata mitihani kidogo ya maradhi ya Kipindupindu. Lakini maradhi haya hayapo Zanzibar nzima, maradhi yanaweza yakawa Chumbuni wagonjwa wawili watatu lakini ukasikia Nungwi kumezuiliwa biashara zisende. Nataka nieleweke vizuri maana mnatabia nikishakusema mimi nikiondoka watu wanabadilisha. Nisije nikaelewaka kwamba mimi napinga maradhi ya kipindupindu.

Mhe. Naibu Spika, lakini kama maradhi yapo Chumbuni basi *curfew* ipigwe Chumbuni, Kiembesamaki kuna wanawake wajane. Sasa ninachotaka kukwambia kwamba wanawake ndiyo wenye nguvu kwa sababu wanaweza bila ya kuwezeshwa. Sasa leo mtoto wa kike, mjane hana mume, ukimzuia biashara na ana mkopo wa Benki anadaiwa kwenda kuchukua kwa ajili ya biashara, maradhi yapo Donge unamzuia wa Kiembesamaki asifanye biashara. Hili nalo tulimurike kwa tochi kwa sababu nchi hii kila mtu anatakiwa ajiajiri mwenyewe, wale wamejiajiri. Sasa tunapokaa tukawafungia tu wasifanye biashara kwa upande mwengine tunawathiri wao na tunawaathiri na watoto wao.

Wakati wa nyuma mahali pakitokezea malaria au kukitokezea ugonjwa wa kuharisha panakuwa panazuiwa watu wa pale ndiyo wakipigiwa *curfew* wasiondoke mpaka wapatiwe matibabu. Lakini leo utasikia daktari anaeleza mtu kapatiwa mabibabu karejea nyumbani wengine wawili wamelazwa, watano wameruhusiwa. Sasa hawa walioruhusiwa kwa muda wa siku ile wa kwenda hospitali ndiyo maradhi yao yameshamalizika. Wale wazuiwe wapatiwe matibabu lakini hawa waliokuwa kwao hakijenda kipindupindu waruhusiwe wafanye shughuli zao. Maisha magumu, watoto wa kike sasa hivi ni wanaume katika majumba. Sisi wanaume wengine tunalishwa na watoto wa kike.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa muda wako umekwisha.

Mhe. Mussa Ali Mussa: Ah! sasa nilikuwa nataka kukupa hadithi nyengine nilikuwa bado nataka kukuomba Mhe. Naibu Spika, unipe ruhusa lakini ni Ramadhani basi, nilikuwa nitoe nyimbo leo lakini nimekumbuka ni Ramadhani, niwaimbie hadithi ya hapo tulipotoka na sasa tunapokwenda.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa muda wako umekwisha.

Mhe. Mussa Ali Mussa: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naunga mkono asilimia mia moja hoja hii nakushukuru kwa kunipa nafasi ya mwanzo.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Jaku Hashim, baada ya hapo watafuata Mawaziri, nitaanza na Mhe. Naibu Waziri wa Elimu (Mmanga Mjengo Mjawiri) na baadaye atafuata Mhe. Mohamed Ahmada Salum. Mhe. Jaku Hashim karibu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, na mimi nikushukuru kwa kunipa fursa hii, bila ya kupoteza muda kwanza nichukue fursa hii kuipongeza serikali kwa kuongeza fedha bajeti ya mwaka huu wa fedha kutoka *billion* 8 hadi kufikia *trillion*, hii ni kuonesha jitihada za Serikali ya Dkt. Ali Mohammed Shein kutekeleza vyema Ilani ya CCM na kuleta maendeleo kwa wananchi ni jambo la kupongeza sana Mhe. Naibu Spika, kazi ya Rais wetu anayoifanya.

Mhe. Naibu Spika, bajeti imeongezeka ni jambo la kuridhisha na la kutia moyo. Lakini hata hivyo naomba nieleze wasiwasi kuhusu ongezeko hili kama je, litakwenda sambamba na utekelezaji halisi na vipaumbele vilivyowekwa. Huu ndio wasiwasi ulipo hapo. Vipaumbele vya bajeti vya mwaka huu kuimarisha ubora wa huduma za kijamii zikiwemo elimu, afya, makaazi, upatikanaji wa maji safi na salama kama alivyotueleza Mhe. Waziri pamoja na kuimarisha miundombinu.

Mhe. Naibu Spika, kama kawaida yangu nitagusa katika sekta ya Afya. Lakini cha kushangaza namtafuta Mhe. Waziri wa Afya humu ndani naona simuoni wala Naibu wake hawapo. Hii itakuwa kama tunampigia mbuzi gitaa wakati hii ndio inamuhusu Waziri wa Afya au Naibu Waziri, tulimuona hapa asubuhi sasa hivi hatumuoni sijui kwa sababu gani. Huwezi kupeleka Mhe. Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais uzoefu wa kule aliokuwa nao kule ni tofauti, huwezi kupeleka Dkt. Khalid Waziri wa Fedha ingawa ndiye anayetoa pesa kule hawezi kujua kitu kama hichi.

Bajeti zote za miaka mitano, vipaumbele ilikuwa ni sekta hizi. Afya imekuwa ina changamoto nyingi na kwamba hakuna ubajeti kabisa. Natambua hatua kadhaa za maendeleo zilizofikiwa kwenye sekta hii lakini bado kazi kubwa inahitajika katika sekta ya afya. Hoja yangu kubwa Mhe. Naibu Spika, changamoto za afya hazipungui, kuna nini kule Wizara ya Afya. Kila Rais akifanya jitihada kuna nini Wizara ya Afya. Jitihada kubwa zinafanywa katika sekta ya Afya ndiyo Wajumbe wakaomba pale Kamati Teule ipelekwe. Rais anafanya jitihada kubwa za chakula bila shaka kuna uzembe ndiyo jawabu lake na uzembe mwengine Wizara ya Afya hautaki tochi.

Mhe. Naibu Spika, pameletwa jenereta pale limekaa miezi mitano au minne kwa pesa chungu mzima, hakuna *activities* yoyote iliyofanywa kufungwa jenereta lile mpaka tumekuja kupiga kelele wakati wa bajeti. Haya tunamfanyia nani? Huku kipaumbele Afya, Rais anafanya jitihada, watendaji wanarudisha nyuma jitihada za Rais hatuwezi kwenda. Jenereta la kileo tena ni msaada yule mwenyewe aliyetoa msaada akija akiona hali kama ile atasaidia tena kweli pale, hawezi kusaidia na linahitajika, umeme ukizimwa tunashuhudia *lift* zikikwama, masaa matatu watu wakataka kupoteza maisha yao ndani. Pana maji pale mbele ya hospitali ikija mvua yanakwama utafute kama kiboti uweze kuvuka kuingia hospitali, ule ni uzembe.

Mhe. Naibu Spika, nilipiga kelele katika sehemu wa wangojwa wa Sukari ile sakafu yake ukimchukua mgonjwa ukimburura hakuna njia hakuna barabara, utafikiri njia ya Mitakawani. Mifuko mitano au sita ya saruji Wizara ya Afya inashindwa pale mgonjwa anakwenda kupata matibabu unakwenda kumzidisha maradhi, haielekei.

Tunaweka fedha kuhudumia akina mama wajawazito lakini bado wanachangishwa, pamoja na jitihada zinazofanywa, bado mama wajawazito wanachangishwa. Waziri hayumo Naibu Waziri hayumo, lakini twende hivyo hivyo. Tunaweka fedha za ununuzi wa dawa, vifaa, tiba, bado huduma hizo hazipatikani kwa uhakika kabisa. Juzi tu hapa kumekuwepo kwa upungufu wa chanjo za mtoto wa siku moja hadi miezi tisa hakuna maelezo yaliyotolewa na kuambiwa wananchi wakati sisi Wawakilishi wao tumeshapitisha fedha hizo kwa nini hakuna huduma hiyo katika sekta ya afya.

Mhe. Naibu Spika, kuna tarifa ya *x-ray machine* ni kitu cha ajabu, hivi sasa hakuna *x-ray*, pale mgonjwa keshatoka shamba anakuja kufata huduma anaambiwa bure pale Mnazi Mmoja ambayo inatagemewa kuwa Hospitali ya Rufaa, anaondoka pale aende Al-Rahma, mnyonge, mkulima, mvuvi, mchukuzi wa nchi wa nchi hii hana pesa ya kupigia *x-ray* si anapoteza maisha, tunafanya nini? Ndiyo yale maneno yangu ninayosema kwamba tunasema kwa mdogo, vitendo havipo. Mtu keshatoka Pwanimchangani, keshatoka Muyuni, keshatoka Paje anafuata huduma Mnazimmoja kwa kusikia kwenye vyombo vya habari kwamba huduma Mnazimmoja ni bure, kwenda kule hakuna kitu mlango umefungwa tena umeandikiwa na tangazo hasa "Huduma ya *x-ray* haipo". Kile ni kitengo nyeti. Tusiweke nambari kubwa za fedha kwenye bajeti ikiwa hatuwezi kutekeleza bora tuweke fedha kidogo ambazo zitatekelezeka. Hatuwezi kufanya vitu kama hivyo.

Mhe. Naibu Spika, nimuombe Mhe. Fedha na Uchumi katika bajeti ya mwaka huu kama kweli afya ni kipaumbele basi tuone fedha za OC kwa Wizara ya Afya zinapatikana kwa asilimia kama vile fedha za kuendeshea vikao vya Baraza la Wawakilishi zinavyopatikana kwa asilimia mia. Huku fedha za Baraza la Wawakilishi kwa asilimia mia zinapatikana hakipungui kitu, Wizara ya Afya hatuwaingizii kwa asilimia kweli afya hiyo itapatikana, haiwezi kupatikana afya tutakuwa tunapiga makelele asubuhi mchana jioni. Hii ndio maana hasa kipaumbele mwaka huu tuone utekelezaji wa bajeti ya afya kwa asilimia kama wanavyofanya kwenye vikao vya hapa.

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Afya ina changamoto nyingi Waziri mimi nikuombe sana na mrithi wako alikuwepo hapa Waziri wa Fedha Omar Yussuf Mzee, alijitahidi hasa na Wizara hii. Nikuombe na wewe vile vile jitihada zako kubwa na uwezo wako tutauona. Ile ni *area* nyeti hata Mhe. Rais inamgusa sana Wizara ile, sijui kwa kuwa katokea pale na uzoefu wake anaijua pale Wizara. Wahanga wale uwape asilimia mia vyenginevyo vyovyote itakuwa tunapiga kelele tu humu ndani. Ikiwa Baraza la Wawakilishi linapata asilimia mia na Wizara ile ni nyeti sisi sote tunahitaji afya pale. Bila ya afya tusingekuwepo hapa kila kiumbe hai anahitaji afya.

Mhe. Naibu Spika, nikuombe sana Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi iangalie Wizara ya Afya, waingizieni kwa asilimia mia. Huku tulikuwa tanataka kuipitisha Hospitali ya Rufaa haina hadhi kuwa Hospitali ya Rufa, vitendea kazi havipo, wataalamu hawapo.

Mhe. Naibu Spika, sasa nije kwenye sekta ya Elimu. Jamani taifa lolote linaendelea kwa elimu bora ya watu wake. Sisi bado tunapiga sana siasa hatutaki kukubali ukweli wa elimu yetu bado ipo chini na sekta hii kila mwaka bajeti yake kipa umbele ni serikali, ajabu skuli nzuri zimejengwa, Rais amezindua lakini bado ni uzuri wa majengo tu lakini skuli haziendani na ubora wa elimu. Majengo mazuri lakini elimu haipo tatizo hatutaki kuambizana ukweli, tuache siasa.

Mhe. Naibu Spika, hoja yangu katika mitihani ya kitaifa hairidhishi tungekuwa Zanzibar na Mtaala wetu, kutoka mwanzo mpaka mwisho tusitegemee NECTA huu ni ushauri wangu. Zanzibar imekuwa na matokeo mabaya tusifichane katika mitihani hii. Imefika wakati sasa Zanzibar iendeshe fomula yake ya elimu, tulifikirie hili jambo baada ya kutegemea NECTA tuwe Baraza letu la Mitihani kama tulivyotoa orodha ya mafuta katika suala la mafuta ya muungano. Tumetoa tukaona hakuna faida na hili tulitoe. Lakini vyenginevyo vyovyote Zanzibar tutashika ushiriki wa chini katika matokeo haya ya mitihani. Kama wazee wetu waliweza kuikomboa nchi hii kwa nini tukashindwe kufanya kitu kama hicho.

Hapo hapo katika Wizara ya Elimu kuhusu elimu pia niseme kuhusu Vyuo vya Amali na Elimu Mbadala, hapa naipongeza serikali tokea Baraza hili lipitishe Sheria ya Mamlaka ya Vyuo vya Amali mwaka 2006 kwa mara ya kwanza SDL imeongezewa fedha katika kumbukumbu zangu ni jambo la kulipongeza Wizara ya Fedha na tumepitisha sheria.

Mhe. Mwenyekiti, kilio changu mimi kikubwa kuhusu mambo ya Mtambuka hichi ni kilio kikubwa nimekiona Bara. Nafikiri sisi Zanzibar tunataka kuiga Bara, lakini hili tutamtafuta mchawi hatumjui nani hapa. Jambo jipya linalotaka kuanza sijui kama lipo kitaratibu au lipo kisheria sifahamu. Nimeona mradi wa umeme wa EU hapa nataka kufahamu Mhe. Waziri serikali inategemea ufadhili hapa au kuna mchango Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika mradi huu wa umeme, ni suala zuri na la kupongezwa tulikuwa tunalipigia kelele sana, mtegemea cha ndugu hufa masikini. Umeme huu utatusokota mara nyingi, mara tukatiwe mara tuna deni, mara miundombinu. Tulishuhudia hapa tulikaa miezi mitatu giza. Umeme wa Zanzibar tunaoutumia ni mdogo sana kuliko kiwanda chengine duniani. Tumeshuhudia juzi juzi China, ziwa tu la maji wametengeneza umeme. Tutafute *formula*, narudia tena "Mtegemea cha ndugu hufa masikini". Kuna madeni tunaambiwa tunadaiwa, miundo mbinu.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kuhusu ugatuzi huduma za kijamii kwenye Serikali za Mitaa. Mimi nina wasiwasi mkubwa sana kwenye bajeti zetu ni ndogo huduma hizi za muhimu za serikali za mitaa, kuhusu kupigwa bajeti. Leo Serikali za Mitaa zinataka kupewa jukumu la kusimamia afya. Huko Bara sasa hivi wanasokotana kati ya TAMISEMI na Wizara ya Afya, hili jukumu litakuja kushindwa. Mamlaka haya tuwaachie wenyewe Wizara ya Afya hatuwezi kupeleka Serikali za Mitaa. Tumeona mfano mmoja Mbunge wa Chwaka kanunua *Ambulance* mbili kazipeleka pale kwenye Afisi ya Halmashauri zimeshindikana.

Hizi *formula* tumezitoa wapi, ukitaka kwenda huku watakwambia hili la Halmashauri, ukenda huku watakwambia Wizara ya Afya. Hatutokuja kuwafanyia wananchi haki, kama mtataka kufanya tujaribu kwa Mkoa mmoja tuone tumefikia hatua gani angalau yale maendeleo yake tuyaone, tusifukuzie tu kama mwezi wa Ramadhani, utakusanya kaimati, vitumbua, chapati tutavuta hapa baada ya magharibi navyo huvihitaji tena. Tujaribu kuandaa tusifukuzie tu huyu kafanya na mimi nikafanya *no* hapa tumekuja kutafuta mchawi Wizara ya Afya atakwambia hili si langu mwenyewe Halmashauri. Halmshauri itakwambia Wizara ya Afya itakuwa kama sekta ya maji lakini Mhe. Salama wizara yake ni moja na waziri ni mmoja. Ukienda kunako maji ikaungua *transformer* wanakwambia wenyewe umeme, umeme wanakwambia wenyewe Mamlaka ya Maji ukamate wapi.

Mheshimiwa kwa kumalizia tena miundo mbinu, kuna barabara hizi za ndani wananchi wamekuwa wakipiga kelele sana Kibonde Mzugu njia ile imekuwa ikilalamikiwa mpaka kwenye vyombo vya habari mimi kule si kwangu, Uzini, Kiboje, Ndagaa wananchi walikuwa wakilalamika Miwani kuna wazazi wanazaa wakati mwengine wanazaa njiani kutokana na mtikishiko ule wa mashimo. Hili Waziri Dk. Karume nafikiri yupo hayupo na yeye waliangalie. Lakini kichekesho chengine hili la Uwanja wa Ndege kwanini hatutaki kusema ukweli wetu ya jengo jipya, kwa nini Serikali haitaki kusema ukweli wa jengo lile kuwa tumefeli tumeshuhudia Rais wetu wa Tanzania juzi tu katika Sekta ya madini ya mchanga kaweka wazi vitu kwa nini Serikali inapata kigugumizi huu si uwanja wa ndege huu wa jengo hili jipya kila siku tunapiga kelele suala hili huu mkataba uko wapi.

Tumeshuhudia Rais wetu juzi kachambua ripoti ya kwanza ya pili keshaziweka wazi kwa nini Serikali inapata kigugumizi na jengo lile la uwanja wa ndege uwanja ambao umejengwa ghali duniani kuliko uwanja wowote, kwa nini tusiweke wazi wananchi wakafahamu *Terminal* ile ina matatizo tukubali makosa yametendeka na hatua kama itawezekana zichukuliwe hichi kichekesho.

Mheshimiwa nije katika Hoteli ya Bwawani Mhe. Waziri wa Fedha hili jengo limehama limekuja mpaka kwako sasa hivi zile ni fedha zinapotea mheshimiwa wakati ni mali waziri jengo lile halitizamiki leo riski tunaipiga teke, muda ule tungekuwa tushafanya jambo lile jengo tungekuwa tuko wapi, Serikali ingepata mapato gani ndio ile hadithi yangu niliyosema kazi yetu kuvunja kutengeneza hatuwezi. Mkataba uko wapi Mwanasheria Mkuu tuletee mkataba tuuone wananchi wapate kufahamu. Mikataba inawekwa wazi zile pesa za wakulima na wachukuzi wa nchi hii na wavuvi jengo lile limevunjwa hakuna kinachoendelea hadithi imekuwa ndefu pesa zile ni raslimali hazina ile inapotea, leo jengo lile la kileo hatumtendei haki Rais wetu wa mwanzo kwa kututengenezea jengo kama lile, kajenga kwa nguvu gani lile tena wakati wa dhiki leo tumeliacha limeporomoka pesa ngapi zinazopotea pale kwa jengo lile huo mkataba alokodishwa nani, hata hakuna *activity* ilofanyika hakuna hatua yoyote ilofanyika pesa nyingi zilizokuweko pale. Ile hoteli ya mwanzo Zanzibar kwa Unguja leo imekuwa haina hadhi yoyote imekuwa nyumba ndege wanajenga tu ndani.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye Sekta ya Maji, maji bado tatizo na Serikali iandae *formula* maalumu kama ilivyoandaa *formula* ya Mfuko wa Barabara kuchangisha pesa hizi barabara haziwezi kupitika bila ya kuwepo wananchi na wananchi bila ya maji hawawezi kuishi, matatizo yote ni maji sisi sote humu tumezaliwa kutokana na maji hospitali ukazimia kitu cha mwanzo unatiwa dripu ya maji, maji ndiyo *engine* lakini leo Mamlaka ya Maji (ZAWA) ina wakati mgumu pamoja na jitihada wanazozifanya Mhe. Waziri, Mamlaka ya Maji kuna wakati mgumu mimi nakushukuru Mhe. Waziri napelekewa vigari viwili, siku 3 hazifiki nahangaika mengine naongeza mengine. Michamvi tokea dunia ilipoanza narudia tena mpaka leo hii tokea urembo ungali tunguja wazee wetu wanavaa tunguja kwenye masikio mpaka leo hakujafika maji kule wamekosa nini watu wa Michamvi wale jamaa, Serikali inapeleka na mimi najitahidi napeleka hivyo hivyo pesa nyingi zinapotea na wakati huu mzito wa ramadhani leo ukienda Bwejuu kushahariba *pump* ya maji nimetengeza juzi tuu miye juzi nimetengeza juzi juzi leo wananisubiri tena nao sikukuu kesho kutwa na maji ya kule wakati kama huu...

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Jaku umebakiza dakika tatu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika nakushukuru lakini watu wanaumia kipindupindu ndio hichi lakini la mwisho nisije nikamaliza dakika zangu nataka kufahamu naiuliza Serikali sasa hivi tunakwenda katika kipindi cha sikikuu huku Manispaa ndio wanaotowa vibali vya hoteli au mikahawa, huku Wizara ya Afya kuna wengine washapewa vibali kwa vigezo gani wengine hawajapewa.

Kuna wengine washaruhusiwa na wengine wana hadhi ya ujenzi kuliko wale wengine jee hii sheria ni upande mmoja, upande mwengine hakuna sasa sisi tukamate Manispaa tukamate Wizara ya Afya kuna watu wanakwenda kutafuta riski wengine washaruhusiwa kupewa vibali hivi sasa, wengine hawajapewa na halmshauri ndio waliotoa vibali hivyo huu ndio upendeleo wa aina gani, tunakwenda katika kipindi cha sikukuu kama kufungwa zifungwe zote kama kupewa na wengine wapewe kutoka na mujibu wa haki stahiki hili litakuwa si haki.

Jengine kwa kumalizia kuhusu Skuli ya Bwejuu Naibu Waziri alijibu swali hapa lakini akawa anam-*quote* Mhe. Mbunge lakini mfuko wa Mbunge una majukumu mengine pengine, lakini kule wananchi wa Bwejuu bado wana kitendawili kizito Naibu hukaa huko mtu akaa na huko mtu haji huko na huko akawa mtu anamtaza huko haji huko ndio anakwenda kujisaida. Huu si uungwana nataka vile vyoo mheshimiwa ulitoa ahadi kama utakwenda lakini hukwenda mwezi wa ramadhani huu hakuna kinachoendelea na ile si kazi ya Mwakilishi wala Mbunge kaokoeni ile hali Mbunge na Mwakilishi wana majukumu mengi nimetaja hapo sasa hivi sauala la maji na nikasubiri mfuko wa Mbunge utachukuwa muda. Hakuna dalili hizo Naibu Waziri hili sitostahamili kama yuko Waziri hili sitostahamili kuanzia kesho naanza kumkamata mtu shati nasema wazi jua halijatuwa saa 5:30.

Mhe. Naibu Spika, nikushukuru sana ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Jaku kwa mchango wako sasa waheshimiwa nilisema kwamba wanachangia Mhe. Mmanga Mjengo na baadaye atafuata Mhe. Mohamed Ahmada ni kidogo nifanya mabadiliko kwa sababu Mhe. Salama Aboud Waziri wa Ardhi, ameniomba achangie ana shughuli nyengine baada ya hapo mheshimiwa kwa hiyo naomba radhi baada ya Mhe. Salama atachangia Mhe. Mmanga Mjengo Majawiri Mhe. Salama karibu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na mimi naomba nichangie katika hotuba hii ya Mpango wa Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Makadirio ya Mapato ya Wizara ya Fedha kwa mwaka huu wa fedha 2017/2018.

Pamoja na kuchangia kwangu naomba pia nitowe ufafanuzi kwa baadhi ya hoja ambazo Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako hili tukufu walizozianisha.

Kwanza kabisa nianze na swali zima la ufungaji wa mita za TUKUZA ambazo waheshimiwa walizisisitiza ule ubadilishwaji wa mita za zamani za *postpaid* na sasa hivi tuweze kuwafungia wananchi mita za TUKUZA.

Mhe. Naibu Spika, naomba nikiri na niseme kwamba Shirika langu la Umeme Zanzibar ZECO lina mkakati maalum wa kubadilisha mita hizi za zamani na sasa hivi tunakwenda kwenye mita za TUKUZA na mita zote ambazo tunazo sasa hivi karibu ni laki 159,000 *plus* ambazo ni mita

zote kwa wafungaji wa Zanzibar ambazo wanatumia umeme lakini jumla ya mita laki 127,000 *plus* tayari zimeshabadilishwa na bado karibu 31,000 *plus* ambazo hizi tunategemea kuzikamilisha baada ya miaka miwili tutakuwa tayari tushakamilisha zoezi zima ndani ya miaka miwili basi mita zote zitakuwa zimebadilishwa.

Lakini vile vile tukiwa katika mkakati huu wale wateja wapya wote ambao wanaomba kuingiwa umeme basi moja kwa moja wanaungiwa mita za TUKUZA, nilikuwa naomba nilieleweshe Baraza hilo Tukufu ili waweze kuelewa hilo.

Lakini jengine nilikuwa naomba nizungumzie swali zima la mkakati wa kulipa deni ambalo tumeliainisha sana lakini Waheshimiwa Wajumbe walikuwa na hofu kidogo ya kusema deni hilo lisije likaachwa likazidi kuendelea likazidi kukuwa pamoja na mkakati ulokuwepo, naomba niwaarifu sana wajumbe wako wa Baraza lako tukufu pamoja na wananchi kwa jumla kwamba pamoja na mkakati wa kulipa deni lakini bado tuna mkakati wa kulipa ankara za bili zike za kila mwezi za umeme ambazo tunaletewa na Tanesco ili hivyo hiyo kuondoa ile hofu na wasiwasi wa kusema kwamba deni hili lije liwepo. Kwa hivyo sasa hivi Shirika limejipanga linalipa bili zake za kawaida sambamba na kupunguza lile deni la zamani ambalo tumeliainisha hapa awali kwamba tunalipinguza, kwa hivyo naomba niwatowe hofu kwamba hakuna ukuaji au ulimbikaji tena wa madeni kuanzia sasa hivi.

Lakini pia Mhe. Naibu Spika, kupitia Baraza lako hili tukufu niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe lakini niwaomba wananchi kwa ujumla wanaotusikiliza kwamba waweze kutumia umeme kutokana na mahitaji yao na matumizi yao na waweze kulipa umeme kutokana na mahitaji ambayo wanayatumia na tuondowe vile vitendo sasa hivi vya udanganyifu katika kutumia umeme, niwaombe sana wananchi tuwe waaminifu tusifanye vitendo ambavyo haviko sahihi katika kuiba umeme na kufanya vitu vyengine ambazo havistahiki.

Lakini Mhe. Naibu Spika, pia nilizungumza swali zima la gharama za upelekaji umeme vijijini naomba niseme kwamba Shirika langu linabeba mzigo mkubwa kupitia Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar, kuhakikisha umeme unafika vijijini bila ya wasiwasi lakini bado wananchi wanatakiwa waendelee kuchangia ili waweze kufikishiwa umeme ndani ya maeneo yao ndani ya majumba yao, lakini bado Serikali itapeleka umeme katika vijiji vyote vya Zanzibar na katika maeneo yote na gharama hizo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar bado inazibeba lakini wananchi kwa ujumla lazima na wao wachangie ili Shirika pia liweze kujiendesha kibiashara.

Mhe. Naibu Spika, pia kulikuwa swali la uendelezaji na kuwekwa mpango mahsusi kuhusu swali zima la eneo la Mangapwani naomba niseme na niwajulishe Baraza lako Tukufu na wananchi kwa jumla kwamba tangazo la uhifadhi la eneo la Mwangapwani kuwa ni eneo la mafuta vilainishi tayari limeshatolewa rasmi katika Gazeti la Serikali kwa hivyo naomba hili watu wote walijuwe kwamba eneo hili sasa hivi limeshatangazwa ni eneo la hifadhi ya mafuta ya vilainishi.

Lakini pia vile vile lilijitokeza swali kuhusu usafishaji wa mafuta baada ya *exploration* wakati wa uchimbaji. Hili tumelipokea tunaomba tunawashukuru sana Waheshimiwa Wawakilishi kwa umakini wao na kuona umuhuimu wa kuwa na hii sekta, kwa hiyo tumelipokea na wakati ukifika basi *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atatuwezesha ili tuweze kulifanya hili *final* tuweze kulifanyia hapa hapa Zanzibar na Inshaallah Mwenyezi Mungu atatupa uwezo wa kuweza kulifanya hili.

Lakini pia limejitokeza swali zima la maeneo ya ardhi ambayo hayaendelezwa ya uwekezaji hili pia tumelipokea lakini naomba niwakumbushe wajumbe wako wa Baraza letu tukufu wakati wa mjadala wa hotuba yangu swali hili lilikuwa ni *hotcake* lakini tumekifikia pahala sisi tumelipokea na tunalifanyia kazi na maeneo tumeanza kuya-*identify* tukishirikiana na Kamati ya Ujenzi na Mawasiliano. Kwa kweli lazima niishukuru Kamati ya Ujenzi na Mawasiliano kwa kazi kubwa ambayo tunaifanya kwa pamoja na wizara yangu kuhakikisha kwamba sheria zote zilizotungwa na Baraza lako hili tukufu basi tunazisimamia katika sekta hii ya ardhi na mimi niwaombe tu sana wajumbe na wananchi kwa jumla, tuko katika kusimamia sheria kwa hiyo maeneo yote ambayo yatakuwa hayakuendelezwa kwa hali yoyote ile basi sheria itachukuwa mkondo wake na tutandelea kusimamia sheria kama ilivyo.

Lakini pia lilikuja swali la Mipango Mjini Wizara yangu kupitia Kamisheni ya Ardhi na Usajili bado inaendelea na zoezi la kupanga mji lakini *Master Plan* ya mji tayari ishazinduliwa na miji kumi na nne tayari inaendelea kupangwa kama nivyoianisha katika hotuba yangu, kwa hiyo naomba niwatowe khofu na wasiwasi Wajumbe wa Baraza lako Tukufu mji tunaendelea kuupanga lakini hili lifanikiwe pia tushirikiano kwa pamoja, kwa sababu kuna maeneo unakuta kuna changamoto ambazo ni za kibinadamu zaidi kwa hiyo mimi niwaombe wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa umakini wao na umahairi wao basi tuendelee kushirikiana ili tuwe na mji mzuri wenye mfuto na kuweza kuwa na maisha bora ndani ya Zanzibar.

Lakini vile vile swali la maji ambalo limekuwa kilio cha wengi, kilio cha wengi katika kila Jimbo mimi naomba niseme na siku zote nitaendelea kusema kusema dhamira na nia ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Rais wetu Jemadari wetu Dk. Ali Mohamed Shein siku zote jinsi anavyowajali wananchi wake katika sekta hii. Kwa kweli tumehangaika sana na bado tunafanya kazi kubwa na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atatusaidia ili kuhakikisha kwamba maji safi na salama yanapatikana.

Lakini katika hili naomba niseme sote tunakiri kwamba vianzio vya maji sasa hivi chini ya ardhi vimepunguza kile kina cha maji na kwasababu kina cha maji kumepungua kwa hivyo hata ile *speed* ya maji utokaji wake umekubwa bado mdogo. Lakini kwa kuwa bado tunahangaika na Serikali iko makini sana na ndio maana tunatafuta fedha huku na kule kuna ufadhili ambao tayari tushauomba katika maeneo mawili matatu ambayo tunategemea kwamba fedha hizi zikipatikana basi kwa asilimia kubwa kilio cha wananchi kitakuwa kimepungua. Nnaomba tushirikiane katika kusimamia, naomba tushirikiane katika kufanikisha hili, lakini naomba tuendelee kushauriana nasema tuendelee kushauriana katika ku-*facility* hata hizo pesa tukipata basi tuwe na mipango ya pamoja kwa kushirikiana na Waheshimiwa Wawakilishi lakini wakishirikiana na Wizara yangu pamoja na Mamlaka ya Maji.

Niwashukuru sana Bodi ya Mamlaka ya Maji ZAWA kwa mkakati wao ambao sasa hivi wanakwenda nao kuhakikisha hata yale maeneo machache lakini wanapata maji kwa muda na wanapata muda muafaka na maeneo mengi sasa hivi kuna *improvement* kubwa naomba niseme hili lakini wanaendelea kuchukua jitihada, ili hata huko ambapo tumekusudia kufika basi *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atatufikisha na tukipata hii fedha basi tunaweza hasa kwa Mkoa wa Mjini Magharibi basi tunaweza kamaliza tatizo la maji ambalo litakuwepo.

Mhe. Naibu Spika, naomba baada aya hayo nimpongeze sana Waziri wa Fedha, niwapongeze sana watendaji wake kwa umakini wao lakini pia kwa kushirikiana nasi siku hadi siku kwa kweli wanatusaidia na wanahakikisha huduma za jamii kupitia Wizara yangu zinafika kwa wananchi kwa kiasi ambacho Mungu anachotuweza. Tunajitahidi sana na Mungu awape moyo ule ule ili tuweze kushirikiana tuweze kufikia yale malengo ambayo wananchi wanayatarajia.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja asilimia mia moja nakushukuru sana.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Ardhi sasa tunaanza na Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri baada ya hapo afuata Mhe. Mohamed Ahmada ajitayarishe Mhe. Said Soud Said. Waheshimiwa Wajumbe kwanza Mawaziri samahanini sana nilikuwa nataka tu kuomba kwamba kwa kuwa leo ndio tumekusudia kumaliza Wizara hii na *almost* Mawaziri wote wametaka kuchangia, nilikuwa nazungumza na Mawaziri naomba sana nyote mtapata nafasi ya kuchangia lakini ningeomba sana kwamba muda mtakaoutumia usiwe muda kama ule wa kawaida.

Kwa hivyo jitahidi sana kufupisha maneno yenu ili tuweze kumaliza siku hii ya leo *otherwise* nikiangalia kwa hesabu tu hapa ikiwa tutatumia dakika ishirini, ishirini kwa Mawaziri wote tunaweza tukajikuta tunapindukia saa tisa leo tunatumia masaa matatu *almost* kwa mawaziri, kwa hivyo naomba sana hilo mnikubalie kwamba mjitahidi kila mmoja kwa mujibu wake, kila mmoja analotaka kulielezea lakini isiwe muda wa dakika ishirini nafikiri mmenielewa vizuri.

Tunanza na Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri mheshimiwa karibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, nakushuru na mimi kunipa fursa hii kufafanua baadhi ya taarifa ambazo au hoja ambazo zimetolewa na baadhi ya wajumbe wenzetu kuhusu hasa katika nukta ya Wizara ya Elimu na nitaanza kuzungumzia suala la ubora wa ufaulu hili limezungumzwa sana na limezungumzwa kwa namna ambayo inahitaji kuwekwa wazi zaidi. Ubora wa ufaulu katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali unatokana na mitihani, mitihani ya taifa ndio inayoamua ubora wa ufaulu na tunayo mitihani ya darasa la nne, darasa la sita, kidato cha pili, kidato cha nne na kidato cha sita. Lakini mimi nitakwenda zaidi katika kidato cha nne na cha sita ili kuweka sawa taarifa hizi.

Mhe. Naibu Spika, tunasema kwamba tunapozungumzia ubora wa ufaulu tunazungumzia ufaulu katika daraja la kwanza, la pili na la tatu. Kwa mfano, katika mitihani ya kidato cha nne mwaka huu wanafunzi waliopata daraja la kwanza walikuwa 242, daraja la pili 879, daraja la tatu 1,862 ukijumlisha wanafunzi waliopasi daraja la kwanza mpaka la tatu unapata 2,983. Huu ni ufaulu mzuri, huu ni ubora wa ufaulu si mbaya kama inavyosemwa kwa mujibu wa takwimu zetu, na kwa pamoja inafikishia asilimia 70.09 ya ufaulu kidato cha nne. Sasa kama asilimia 70 ni mbaya sijui nzuri itakuwa ni ipi.

Mhe. Naibu Spika, sasa niendelee katika matokeo ya mitihani ya kidato cha sita ambayo hata ule ambao tulikuwa tunasemwa kwamba tumefanya vibaya, haikuwa vibaya ufaulu katika mwaka ule ulifikia asilimia 93.13. Sasa labda nioneshe mwelekeo ule wa ufaulu katika miaka mitano iliyopita halafu tuone ufaulu ni mbaya au si mbaya.

Mwaka 2012 wanafunzi waliopasi daraja la kwanza mpaka la tatu ambalo ni la ubora hilo, walikuwa ni asilimia 55.43. Waliopasi daraja la kwanza mpaka la nne katika ujumla wake walikuwa asilimia 78, mwaka 2013 wanafunzi waliopasi katika daraja hilo la ubora walikuwa ni asilimia 76.29, mpaka daraja la nne walikuwa ni asilimia 96.37. Mwaka 2014 walikuwa ni asilimia 75.41 daraja la kwanza mpaka la pili, na daraja la kwanza mpaka la nne ilikuwa asilimia 95.50. Mwaka 2015 daraja la kwanza mpaka la tatu ambao lina ubora ni asilimia 86.67, daraja la kwanza mpaka la nne ni asilimia 97.47. Mwaka 2016 daraja la kwanza mpaka la tatu ni asilimia 79.16, daraja la kwanza mpaka la nne ni asilimia 92.31. Sasa sisi wizara na serikali tunaamini kwamba ufaulu huu uko katika hali ya ubora si mbaya hata kidogo kama walivyodhani baadhi ya watu. Ndio maana baadhi ya wataalamu na naomba radhi kama mtu nitamkwaza wanasema *no research no right speak*, bila ya kufanya utafiti basi kwa kweli ni vigumu kuweza kusema zaidi.

Mhe. Naibu Spika, niendelee na nukta ya pili ambayo ilizungumziwa kuhusu msaada wa serikali kwa skuli za maandalizi za jamii, tuelewe kwamba kuna mifumo mitatu ya skuli za maandalizi. Kuna skuli za maandalizi za serikali, kuna skuli za maandalizi za watu binafsi na kuna skuli za maandalizi za jamii. Kwa maana hiyo, serikali inapaswa kusimamia hizi skuli za maandalizi ambazo ziko chini ya wizara, hizi nyengine zinajiendesha wenyewe isipokuwa wizara hutoa msaada wa kitaaluma pale inapohitajika hasa katika sehemu ya mafunzo. Lakini uendeshaji mwengine wa kifedha unafanywa na skuli binafsi na zile za jamii unafanywa na jamii.

Mhe. Naibu Spika, ni kwamba kulikuwa pia na *concern* ya madarasa yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi. Tumetoa maelezo mengi na tutaendelea kwamba madarasa haya hapo awali yalikuwa 501, serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ikatengeneza mpaka ifikia 285 ambayo tunazo sasa. Kama tulivyosema katika bajeti hii kwamba tutafanya kazi ili kuzipunguza asilimia zote hizi za madarasa ili tuweze kuona vijana wetu wanasoma katika nafasi na katika uwiano unaokubalika.

Mhe. Naibu Spika, lakini niseme kwamba wakati wananchi wanapotaka kujenga hizi skuli lazima wafuate vigezo vilivyowekwa na Wizara ya Elimu vyenginevyo inakuwa ni vigumu sana kuweza kumalizia kazi hiyo. Pale tunapokabidhiwa kazi hiyo inaonekana kama kwamba tunaanza sasa, si kuezeka tu kwa sababu zimekosa viwango nyingi zao. Kwa hivyo, tunashauri kwamba wanapotaka kujenga wananchi lazima wafuate vigezo vilivyowekwa na Wizara ya Elimu.

Mhe. Naibu Spika, nakubaliana sana na wazo la Mhe. Hidaya Ali Makame alizungumzia suala la kutumia fursa hizi za elimu mbali mbali, na nadhani hili ni muhimu sana kwamba ni vyema sasa tukatumia kitu ambacho tunaita *indigenous knowledge* kwa ajili ya kusaidia masuala mbali mbali katika jamii. Kwa mfano, suala la kuhifadhi mazingira, suala la malezi, suala la tafiti hata suala la tiba. Nimesoma sehemu nyengine wanatumia masuala haya yaani maarifa ya watu katika kuhifadhi mazingira, pengine hapo kale watu walikuwa wanahifadhi mazingira vipi, hapo kale watu wanaleana vipi. Sasa tunapozichukua fikra hizi na tukazichanganyisha na za sasa nadhani tunaweza tukafanya kitu chenye manufaa kwa jamii zetu.

Mhe. Naibu Spika, pia kulikuwa na kauli kwamba skuli za serikali ni dhaifu sana katika kutoa elimu. Si sahihi kama tulivyosema kwamba zina ubora wake, zina viwango vyake na zina

taratibu zake na mitaala yake ambayo yanafuatwa kwa ukamilifu. Kama tulivyoona data zetu hali ya ufaulu ulivyo katika skuli za serikali.

Mhe. Naibu Spika, pia kuna suala la mwisho ambalo nataka kulisema na nimesema kwa haraka ili nitoe muda. Ni kwamba kulikuwa na maoni ya kuwa na haja ya kuimarisha masomo ya lugha. Tunakubaliana kwa sababu hili ni suala la la sera, Sera ya Elimu imetaja masuala ya kufundishwa lugha hizi za kigeni mbali mbali kwa wananchi wetu. Kwa sasa zimeshaanzwa baadhi ya lugha mmeona zinafundishwa katika Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni pamoja na baadhi ya skuli za sekondari. Lakini msisitizo ulikuwa pia katika kusomesha lugha za Asia, kwamba kwa sasa tulikuwa tunasomesha zaidi lugha za ki-Ulaya, Kijerumani, Kiingereza, Kifaransa, Kireno, Kispanish na nyenginezo.

Kwa hivyo, hili ni wazo zuri na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kimeanza lugha ya Kichina, inasomeshwa kule lugha ya Kichina na nadhani tutajifunza lugha nyengine zaidi, kwa sababu tukikuza lugha wanasema ni buradani, ni fahari. Unajisikia fahari mtu ambapo atakuwa anajua lugha nyingi anajisikia fahari zaidi. Kwa hivyo, nadhani suala la lugha litatiliwa mkazo na kwa mukhtadha huu usomeshaji wa lugha ya Kiingereza nao pia utatiwa mkazo sana, sana. Ndio maana katika mpango mkakati wetu wa miaka mitano sehemu ya lugha ya Kiingereza imepata nafasi kubwa sana. Tunatarajia kwamba tutaweza kujenga msingi imara wa kuweza kujifunza lugha, si Kiingereza peke yake lakini pia na lugha nyengine zote kwamba watu wengi inawezekana sisi wenyewe hatujijui wanawasifia sana watu wa Zanzibar kwamba wanajua lugha nyingi. Anasema watu wengi unaokutana nao ukizungumza lugha hii anafahamu, ukizungumza na lugha hii anafahamu kwa hivyo tuna sifa hiyo wanatusema kwamba tunajua lugha nyingi.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa nimalizie mchango wangu kwa kuunga mkono kwa ukamilifu hotuba hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri, mchangiaji anayefuata ni Mhe. Mohammed Ahmada, Naibu Waziri atafuatia Mhe. Said Soud Said MBM na baada ya hapo atafuata Mhe. Hamad Rashid, Waziri wa Kilimo na Uvuvi.

Mhe. Naibu Waziri Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, awali ya yote na mimi sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kukutana siku hii adhimu ya mwezi mtukufu wa Ramadhani ikiwa mwezi 24 tukiendeleza kujadiliana na Bajeti ya Serikali na Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2017/2018. Kwa hivyo, mimi nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa uwasilishaji wake mzuri, bajeti iliyojaa hekima, busara na imebeba dhima kubwa kwa maendeleo ya nchi yetu. Sote tunaelewa kwamba ni bajeti ya mwanzo ambayo imeanza na trilioni moja na zaidi ya bilioni 87.4, inaonesha wazi kwamba wizara hii imejitahidi katika ukusanyaji wa mapato na nina imani kubwa sana ikifika 2020 lile lengo letu la kukusanya kwa mwaka bilioni 800 tutalifikisha bila ya wasiwasi wowote.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo nije kuchangia kwa yale ambayo wajumbe wameulizia kuhusu Wizara yetu ya Mawasiliano na Usafirishaji kwa ufupi tu kwa sababu kuna mengi ambayo tuliyajibu wakati wa uwasilishaji wa bajeti yetu na ambao wawakilishi waliipitisha tena bila ya kufanyiwa marekebisho ya aina yoyote.

Mhe. Naibu Spika, mimi niendelee kuchukua nafasi hii kuishukuru serikali yangu chini ya uonogozi wa Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuitengea wizara yetu ambayo ndio muhimili mkubwa wa uchumi etu hasa katika hii sekta ya miundombinu takriban bilioni 209.4 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Ni pesa nyingi sana, ni pesa ambazo iwapo tutazipata zote na tukazitumia vizuri basi mimi nina imani kubwa sana miundombinu kuanzia viwanja vya ndege, bandari na barabara basi itakuwa katika hali nzuri na hivyo kufikia katika yale malengo yetu ya dira 2020 kuelekea uchumi wa kati.

Mhe. Naibu Spika, kuna baadhi ya masuala yameulizwa katika sekta ya barabara, kusema kweli tuliyajibu vizuri siku ile kwamba nia na lengo letu ni kuhakikisha kwamba miundombinu hii ya barabara tunaiendeleza na zile sehemu ambazo zimeharibika basi tutachukua juhudi ya kuhakikisha kwamba tunafanya marekebisho ili zirudi katika hali yake ya kawaida. Naishukuru Wizara ya Fedha na Mipango kwa kututengea pesa zaidi ya bilioni 2.5 kwa ajili ya ununuzi wa mtambo wa lami. Vile vile *pavers* na *roller* hizi zote zitasaidia sana katika kuharakisha maendeleo ya miradi yetu hii ya barabara. Nina imani kubwa sana kilio chetu cha muda mrefu ambacho pia wawakilishi walikisema kwamba UUB wanafanya kazi kubwa iwapo watapatiwa zana za kisasa basi kuna uwezekano wa kufanya mambo mengi zaidi. Tushaanza kufanya na tutaendelea kufanya na vikija vifaa hivi basi tutafanya mengi mazuri zaidi ili kuhakikisha kwamba ilani ya uchaguzi ambayo sisi tuliinadi kwa wananchi wetu chini ya uongozi wa Dkt. Ali Mohamed Shein tunayatekeleza kwa asilimia mia yote tuliyoyaahidi hasa katika sekta ya barabara.

Kweli ziko baadhi ya barabara zimeharibika sana lakini kama nilivyosema tutazitengeneza na niushukuru Mfuko wa Barabara ambapo wametenga fedha maalum kwa ajili ya matengenezo na nina imani kubwa sana tutazitumia vizuri fedha hizo. Sisi kwa upande wetu UUB vile vile tumeanza kuvitengeneza vile vifaa ambavyo vimeharibika na hivi sasa vinaanza kufanya kazi, kwa hivyo tutakuwa na kasi zaidi ya kuhakikisha kwamba barabara tunazifanyia matengenezo. Tunaendelea kufanyia baadhi ya matengenezo barabara baada ya mvua kwisha, juzi nilikuwa niko Chaani/Gamba na maendeleo ya wananchi wameona wametushukuru sana.

Mhe. Naibu Spika, vile vile nimetembelea barabara ya Kizimbani mpaka Miwani/Kiboje ambayo nayo tunakiri kwamba iko katika hali mbaya. Katika bajeti yetu serikali imetenga zaidi ya milioni 830,000,000 na vile vile wahisani ambao walikuwa wakiendeleza ule mradi wa barabara tatu BADEA wametutengea bilioni 7. Tutaomba sana kwa Mwenyezi Mungu tuzipate hizi fedha ili baadae barabara ya Jumbi/Koani yenye urefu wa kilomita 6.3 na ya Kizimbani hadi Kiboje yenye urefu wa kilomita 7.2 tuweze kuzitengeneza kwa kiwango cha lami. Mhe. Naibu Spika, sisi tumesema tutachukua dharura ya kuzitengeneza barabara zile ili zipitike wakati wote.

Mhe. Naibu Spika, wako waliozungumzia kuhusu barabara ya Ole/Kengeja, mimi nataka kuwaambia Waheshimiwa Wawakilishi na wananchi kwa jumla kwamba ule mradi umechelewa kidogo kuanza kwa sababu ya upatikanaji wa fedha na vile vile uhaba wa vifaa. Lakini licha ya hivyo kupitia wakandarasi wetu wazalendo tumepiga hatua kubwa sana mpaka hivi sasa kuanzia Ole/Kianga mpaka Vitongoji tutamaliza tabaka la kifusi na Mfikiwa tunaendelea kuweka tabaka la mwisho la kifusi, na tuna imani kubwa sana tulichelewa tu kupata lami, lakini pale lami itapokuja basi kilomita 11 zile tulizozipanga katika kipindi cha mwaka huu wa bajeti unaomaliza

tuwe tayari tushazitia lami. Ukiacha hivyo tunajua kwamba kuna wananchi walikuwa wanatudai fidia.

Mhe. Naibu Spika, mimi napenda kuchukua nafasi kuwaomba wananchi waendelee kuwa na subra lakini napenda kutoa taarifa kwamba mpaka sasa hivi tushatumia zaidi ya milioni 320,000,000 kulipa nyumba 40 Ole/Kengeja mpaka Vitongoji na vile vile vibanda saba. Kwa hivyo, tunajitahidi na vile vile mimi na Makamu wa Pili tulienda kule kutembelea wakati wa mvua, kuna ziwa pale linaitwa ziwa Kiwaa lilijaa kweli maji hadi kusababisha ile barabara baadhi ya sehemu kuharibika. Ni mvua kubwa sana ambazo zilikuwepo maeneo yote ya Unguja na Pemba na zile mvua kusema la kweli zimeathiri sana barabara zetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi napenda kutoa taarifa kwamba wananchi wa Ole/Kengeja ambao tayari tushawalipa wathamini ule mchango wetu basi wawe tayari kuvunja nyumba zao ili tuendelee na ule ujenzi wetu wakati tutapokuja kutia lami. Nitaomba Mhe. Mwakilishi mahiri Mhe. Mussa Ali Mussa atumie nafasi hii kuwashajihisha wananchi wake waanze kuondoka katika yale maeneo wakati wowote mvua zimeisha tutajitayarisha kutia lami.

Mhe. Naibu Spika, vile vile amezungumzia kwa nini ile barabara inachelewa. Kama nilivyosema ile barabara imechelewa kwa sababu ya hizo pesa, lakini hivi sasa tushasafisha eneo kubwa sana tu na Mhe. Bahati anajua hivyo na karibuni tu tunaanza kufanya tathmini kwa ajili ya kulipa fidia katika kipindi hiki mpaka Juni wale wote ambao wataathirika na vipando vyao.

Mhe. Naibu Spika,y amezungumzwa masuala ya vipando maeneo tofauti. Tunakiri kwamba kuna maeneo ambapo barabara tayari zishajengwa bado hatujalipa fidia za vipande kama vile maeneo ya Gando. Kama alivyosema huu mradi wa NORAD vile vile tunakiri wenzetu hapo kabla walikuwa hawajalipa, lakini sisi kwa utaratibu wa sasa hivi tumeweka kwamba hatuanzi mradi wa barabara kabla ya kulipa fidia. Tumeanza kulipa kuanzia Bububu mpaka Mahonda/Mkokotoni zaidi ya bilioni 1,300,000,000 na tutaendelea kulipa kwa maeneo mengine, na vile vile tunajipanga kwenda kulipa barabara ile ya Wete hadi Chake-Chake. Kwa hiyo, mimi napenda kumtoa wasi wasi Mhe. Mwakilishi tuko katika jitihada na tutahakikisha kwamba wale wanaostahiki kulipwa fidia kwa mujibu wa tathmini iliyofanywa na Wizara ya Fedha basi tutawalipa fidia zile.

Mhe. Naibu Spika, pia wamezungumzia sana kuhusu suala la *Airport*. Mimi nina imani kubwa sana wawakilishi wana hamu sana kuliona jengo linataka kumalizika, hata Rais wetu na sisi tuna imani kwamba sote tuna hamu ya kuliona lile jengo linamalizika ili tuendelee kupokea watalii wengi zaidi kwa ajili ya maslahi ya nchi yetu. Kwa hivyo, mimi nina imani kubwa sana tuliyoyasema katika bajeti yetu yanatosha watuamini na kwamba ule ujenzi utapoanza hautochukua zaidi ya miezi 18 tuombe Mungu mambo yote yaendelee kama yalivyopangwa katika bajeti hii inayokuja ya 2017/2018 basi ule ujenzi uanze na uende kwa haraka upate kumalizika.

Mhe. Naibu Spika, vile vile wengine wameulizia na kutaka ushauri kuhusu ujenzi wa barabara ya Mpigaduri na wengine wakashauri labda tuijenge Bumbwini. Mimi nina imani kubwa sana wale wataalamu wetu wa Kichina waliokuja kuangalia eneo la Mpigaduri ni eneo ambalo linastahiki

kujengwa ile bandari yetu ya Mpigaduri na nina kwamba itapoanza ujenzi basi itakwenda kwa haraka na baadae utamalizika kwa mujibu wa kipindi kile kilichopangwa.

Mhe. Naibu Spika, wapo ambao wametushauri kuhusu ujenzi wa nyumba za ghorofa kwa ajili ya watu wetu wa kipato cha kawaida. Tumeuchukua na sisi kama wizara tunaendelea kufanya juhudi za kuwatafuta wawekezaji ili na wao watusaidie katika kujenga nyumba za bei nafuu. Kweli iko miradi imeanza lakini miradi ile ni zaidi kwa watu wa kipato cha kati na kwenda juu. Nina imani Shirika la Nyumba wamejipanga zaidi na tutafanikiwa.

Mhe. Naibu Spika, wamezungumzia kuhusu Shirika la Meli na hasa meli yetu ya MV. Mapinduzi II. Mimi kwanza niwapongeze wananchi kwamba wamekuwa wakiipenda sana meli yetu na wameamini kwamba imekuwa ndio mkombozi kwa usafiri hasa wa kwenda Pemba. Kweli meli ile hivi sasa iko Comoro na imeenda Comoro kwa sababu inatakiwa tubadilishe na tuangalie maeneo tofauti ya visiwa vyetu kwa ajili ya kufanya biashara na ndugu zetu. Kwa hivyo, meli ile itarudi na tarehe 26 tunategemea meli hiyo itaenda Pemba kama kawaida.

Vile vile Mhe. Mussa amezungumzia kuhusu suala la kuuzwa tiketi. Mimi nina imani kubwa sana na sijui ilikuwaje lakini nitamuomba Mhe. Mussa anipe huo uthibitishe. Sisi tumetoa matangazo mapema kwamba meli yetu ya MV. Mapinduzi II itakwenda zake Comoro, kwa hivyo sisi kupitia Shirika la Meli hakuna tiketi iliyouza. Kama kuna watu wameuziwa tiketi na watu wetu au na mtu mwengine yeyote nitamuomba sana Mhe. Mussa atuletee uthibitisho ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya watu hawa.

Mhe. Naibu Spika, vile vile napenda kuwaomba sana wawakilishi waendelee kuwashajihisha wananchi wetu waendelee kufuata taratibu za ujenzi na vile vile wasiende kuingilia katika maeneo yetu ya hifadhi ya barabara kwa sababu baadae inabidi tunapata tabu sana pale ambapo tunaona mtu anajenga nyumba yake nzuri tunaenda kumbomolea kwa sababu hakufata zile taratibu. Hivi sasa kama nilivyosema barabara ya Chake-Chake mpaka Wete tushatenga zaidi ya bilioni 1,500,000,000 kwa ajili ya kulipa fidia na tuna imani kubwa sana wakati wowote ile barabara itaanza ujenzi wake baada ya kukamilisha taratibu.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa nitumie nafasi hii kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Malindi na mimi mwenyewe binafsi kuiunga mkono asilimia mia moja hotuba hii ambayo ni hotuba ya kupigiwa mfano kwa ajili ya mustakabali ya nchi yetu na nina imani kubwa sana wawakilishi na wananchi wote wameona kwamba, serikali inayoongozwa na Dokta Ali Mohamed Shein imekusudia kuwasaidia wananchi wake kuwapeleka katika uchumi wa kati na nina imani kubwa sana tutafika iwapo tutakuwa na mashirikiano ya kutosha na tutaendeleza amani na utulivu ambayo tunayo hivi sasa katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana naunga mkono hoja. (*Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana nakushukuru. Waheshimiwa Wajumbe mawaziri wengi ambao sasa hivi watakuwa wanachangia watakuwa wanajibu hoja ambazo zimetokana na nyinyi Waheshimiwa Wajumbe. Kwa bahati mbaya sana ninaona wengi ambao wamekuja na hoja muhimu hawamo humu ndani, ikifika wakati wa kupitisha vifungu hoja zimeshajibiwa na

mawaziri wakaja na hoja zile zile Waheshimiwa Wajumbe msije mkanilaumu. Tunaendelea Mhe. Said Soud. *(Makofi)*

Mhe. Soud Said Soud (Waziri Asiye na Wizara Maalum): Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia na mimi nafasi hii ambayo nitaweza kuzungumza kuhusiana na wizara hii ya fedha, wizara ambayo ni wizara mama katika nchi yetu. Lakini kabla ya hapo Mhe. Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi ya kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kazi kubwa ambayo anaifanya katika nchi yetu ya uongozi bora uliojaa busara na hekima, uongozi ambao hauangalii dini, kabila, wala rangi ya mtu.

Mhe. Rais wetu ni kiongozi ambaye sasa ameweza kuiweka Tanzania katika hali ya dunia kuonekana kwamba ni nchi ya mfano. Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein pamoja na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. John Pombe Magufuli ni viongozi ambao wanastahili kupigiwa mfano kutokana na harakati za kunyanyua uchumi wa nchi hii na kupeleka taifa hili pale ambapo Wazanzibari na Watanzaia wamekusudia. Lakini kabla ya hapo nilikuwa nataka niseme kwamba, iko haja kwa Wazanzibari na Watanzania wote kuamini kwamba serikali zote mbili zinatekeleza kwa umakini sana Ilani ya Chama cha Mapinduzi, ambayo nimeiangalia kwa umakini kabisa ni ilani ambayo inahitaji kuigwa na vyama vyote vya siasa ndani ya nchi hii.

Ilani hii unapoiangalia haikuacha kitu chochote ambacho kinastahili kwa Watanzania kufanyiwa ikiwa kama ni ishara ya kuwapeleka kwenye maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, ningependa kusema kwamba sijapata kuona kitu ambacho kinatendwa na serikali hii ambacho hakimo ndani ya ilani hii. Kwa mfano, napenda kidogo nichukue nafasi ambayo kwa taifa letu la Tanzania limeweza kukutana na mambo mengi na kwa haraka sana na limeyagundua kwenye ilani hii.

Katika kipindi cha miaka mitano ijayo 2015/2020 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa Chama cha Mapinduzi itaendeleza mapambano dhidi ya madawa ya kulevya kwa kutekeleza yafuatayo:

Utekelezaji wa sheria ya madawa ya kulevya kwa kuandaa mazingira bora ya utendaji kazi kwa vyombo husika, kudhibiti uingiaji na usafirishaji wa dawa za kulevya, kuendeleza mafunzo na elimu kwa jamii juu ya athari ya madawa ya kulevya na kuandaa mkakati wa kuwasaidia waathirika na mambo hayo ili kuachana na utumiaji. Aidha, itajenga kituo maalum cha kurekebisha vijana walioathirika na madawa ya kulevya, yaani hiki kitabu hakikuacha kitu ni kitabu ambacho watanzania tunahitaji kukisoma kwa umakini ili kiweze kutoa nguvu za uhakika juu ya viongozi wetu wanaoongoza nchi hii. Mhe. Rais, John Pombe Magufuli na Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein na endapo tutakuwa tayari Watanzania kuamini kitabu hiki kwamba kina miongozo sahihi nchi hii imepiga mifano ya aina yake na itakuwa inajikwamua kila siku katika hali ya kuondokana na umasikini.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nataka niseme kwamba, Wizara ya Fedha ambayo sasa inatekeleza majukumu yake makubwa sana na ya kupigiwa mfao katika nchi yetu, na yaliyowezesha kuifanya ilani hii ya Chama cha Mapinduzi itekelezeke basi wizara hii iko haja ya kupigiwa mfano. Kwa uhakika kabisa kulikuwa na mambo ambayo sisi wengine tulikuwa hatuyajui, lakini

baada ya maelekezo mazuri na yenye kina ndani yake tumeweza kugundua. Sasa ni vizuri Watanzania, hasa Wazanzibari tukawa tayari kuisaidia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika hali ya ukusanyaji wa mapato, ili mapato haya yaweze kufanya kazi zile ambazo zimeendelezwa na serikali yetu. Mapato ya kuwasaidia wazee wetu ambao wanafikia miaka 70 wanapewa shilingi 20,000 kuna uwezekano wa kuongezewa na hilo jambo haliwezi likapingika pale mapato yatakapokuwa yameongezeka. Wengi wetu tunakaribia huko kupata hii shilingi 20,000 ya kila mwezi, jambo ambalo tunamshukuru Mhe. Rais kwa hoja hii. Halikadhalika suala la kuwaongezea mishahara wananchi wa Zanzibar wale wa kima cha chini, cha kati na hata wa juu. Hili jambo limefurahisha sana na limekuja kutokana na ukusanyaji wa mapato.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nataka niwatoe wasiwasi Wazanzibari kuhusiana na suala zima la ukusanyaji wa mapato kupitia *TRA* na *ZRB*, kumbe hawa watu wa *TRA* sisi tulikuwa hatuna habari kwamba wanafanya kazi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, pamoja na kwamba *TRA* ni ya Muungano, lakini kwa sababu wako forodha na forodha ni ya Muungano wanaikusanyia mapato Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na hili jambo ni la kufurahisha ni jambo la kupigiwa mfano na ni kweli kabisa kama ingelikuwa tunajikusanyia sisi wenyewe kwa wenyewe, basi naamini hatua hizi za kupata mapato haya tunayoyapata isingefikiwa. Lakini kwa bahati nzuri leo hii tumefika pahala tumeliona hili.

Mhe. Naibu Spika, kwa nini nasema hivyo, ufahamu wa mtu hauwezi kuja mara moja kwamba labda akizaliwa tu atafahamu, ufahamu wa mtu unakuja kwa kufuatilia ili aweze kujua athari ina matatizo na hasara, lakini baada ya kufuatilia kwa uhakika kabisa napenda kuwatoa wasiwasi Wazanzibari wenzangu kwamba *TRA* ni chombo kweli cha Muungano lakini *TRA* iliyopo Zanzibar nakusanya fedha kwa ajili ya Zanzibar na ndio maana leo wizara hii ikafikia hatua ya kujivuna kwamba inakusanya mapato kwa kiasi kikubwa na inaondoa matatizo yote yaliyokuwa yameweza kuikumba nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, usahihi wa hoja hii unakuja kwamba kuna vyanzo vitatu vya ukusanyaji wa mapato, kuna yale mapato yanayokusanywa na *ZRB*, kuna mapato yanakusanywa na *TRA* na kuna mapato yanakusanywa na Serikali za Mitaa. Mimi nazungumzia sana *TRA*, kwa sababu hii *TRA* imetuathiri siku nyingi, tulikuwa tuna imani kwamba hawa wanakusanya pesa wanazipeleka Tanzania Bara kumbe sivyo. Mimi leo nawaambia Wazanzibari wenzangu kwa uhakika kabisa na laiti ingelikuwa hawa wanaendelea kukusanya pesa hizi na kuzipeleka Baraza mimi kwanza siogopi ningesema hapa hapa kwamba pesa zetu wanazipeleka Bara. Lakini nawathibitishia wafanyabiashara wote Wazanzibari wote kwamba fedha inayokusanywa na *TRA* kwenye Forodha inabaki Zanzibar na tunajivunia kutokana na hoja hiyo.

Mhe. Naibu Spika, jengine la kumalizia ningetaka niseme kwamba, Wizara ya Fedha bado ina majukumu ya kuangalia hata wale ambao walithubutu kuleta meli mbovu katika nchi hii na wakashindwa kuzikatia bima, basi ni vizuri bima ikatafutwa ya meli zile wakazilipa ili wizara ikapata fedha yake.

Mhe. Nabu Spika, kosa la jinai halifi, jinai inaweza kufufuliwa wakati wowote. kwa hivyo, watu walionunua meli mbovu wakaja nazo hapa yakazamisha watu na meli zile zimawa hazina bima lazima Wizara ya Fedha iwatafute walipe bima ya meli zile ili serikali iweze kupata mapato.

Mhe. Naibu Spika, si vibaya kudai bima si vibaya kwa sababu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilijitolea kutoa mkono wa rambirambi kila familia, kwa vile na wao wale waliokuwa na meli mbovu walipe bima kwenye Serikali ya Mapinduzi ya Zazibar ili wizara hii ipate kunyanyua uchumi wake.

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana naunga mkono hoja.

Mhe. Naibu Spika, Nakushukuru sana Mhe. Said Soud kwa maelezo yako mazuri kabisa na nafikiri Mhe. Waziri wa Fedha atakushukuru sana kwa sababu anajua semina ya jana imesaidia sana. Sasa ninamkaribisha Mhe. Hamad Rashid Mohammed, baadaye atafuata Balozi Amina Salum Ali.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mazingira na Ushirika: Mhe Naibu Spika, awali ya yote na mimi naomba kuungana na wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema na Utukufu kwa kutujaalia salama usalimini na tunaendelea na mfungo na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atujaalie atupe *Husnul khatima*..

Mhe. Naibu Spika, tarehe 21 Machi, 2016 kwa niaba ya vyama vilivyoshiriki uchaguzi tulipata fursa ya kumshukuru, kumpongeza Dokta Ali Mohamed Shein na katika maneno ambayo niliyasema nilisema maneno mawili makubwa. Kwanza nilimwambia changamoto kubwa inayokukabili mbele yako ni hali ya kisiasa na ya pili ni hali ya umasikini yaani uchumi wetu ni kwamba unahitaji watu wetu kipato chao kiweze kuongezeka. Nataka nichukue fursa hii kumshukuru sana Dokta Ali Mohame Shein kwamba ameyafanyia kazi na leo tunaishi kwa amani na utulivu, haya maendeleo tunayozungumza hapa ni hekima, busara, katika kupambana na suala zima la kisiasa, nchi yetu imebaki katika utulivu na amani na ndio tunapata maendeleo tunayoyaona. Hii ni kazi kubwa sio kazi rahisi hata kidogo. Lakini pili ni suala zima la kiuchumi la kwamba bado kipato chetu ni kidogo, watu wetu ni masikini kwa hiyo nalo amelifanyia kazi nzuri sana.

Mhe. Naibu Spika, kusimamia *cash budget* sio kazi rahisi hata kidogo, kwamba unatumia unachochuma, kuendesha serikali kwa kutumia *cash budget* sio kazi ndogo hata kidogo, hii kazi Mheshimiwa ameifanya kwa uadilifu mkubwa sana kwanza amekata matumizi ya ovyo ovyo mengi, ameongeza nidhamu ya kazi, *performance* yetu imefikia kama asilimia 68 sasa na zaidi, kodi imekusanywa vizuri sana ndio maana serikali imeweza kufanya hayo iliyofanya mpaka tukaongeza mishahara ambayo imeongezwa mara mbili sio kazi rahisi hata kidogo. Nataka nimsifu Rais mwenyewe, makamo wake anayemsaidia, lakini na watu wa Wizara ya Fedha kwa jumla wote wakiongozwa na waziri na Katibu Mkuu wao kwa kazi kubwa waliyoifanya kuhakikisha kabisa serikali inakwenda vizuri na hata sisi tulioko mawizarani hatuna malalamiko kwamba hiki hakipatikani na kadhalika. Kuna upungufu wa utendaji wa hapa na pale lakini nasema wamefanya kazi kubwa sana na tumpongeze sana Rais kwa kazi hiyo.

Mhe. Naibu Spika, mjadala mkubwa sana ulikuwa katika suala zima la kilimo kwamba serikali iwekeze sana kwenye kilimo. Nataka kuwaambia tena waheshimiwa serikali imewekeza, mara hii tumepata bajeti si chini ya 27 *billion* ambayo inakwenda kwenye *Exim Bank* kwa ajili ya kuwekeza hekta 1,500 za kuzalisha mpunga. Nataka nimshukuru Makamu wa Rais pamoja na Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko juzi tulikuwa kwenye mazungumzo na Kampuni ya

China itachukua hekta 1,500 za kuzalisha tena mpunga. Kwahivyo, tutakuwa na kama hekta 3,000 tunazalisha kwa *irrigation* mpunga na tunahitaji hekta 4,000 ili tujitosheleze kwa chakula kwa njia ya *irrigation*.

Hekta 1,000 zitakwenda kwenye Kampuni, hekta 500 atawapa wananchi na zile 1,500 watapewa wananchi. Kwa hivyo, wananchi watakuwa na hekta 2,000 zilizotengezwa miundombinu mizuri ya *irrigation* na upande wa pili Wachina watalima hekta 1,000 kwa *irrigation*. Naamini kabisa *investment* hiyo iliofanywa na serikali chini ya uongozi wa Rais wetu naamini kabisa suala la mpunga miaka miwili na nusu inayokuja hadithi itakuwa nyengine hapa. Jana nilikwenda Bumbwisudi pamoja na Mhe. Machano Othman Said tukazindua ukulima wa shadidi watu wanavuna sasa kwenye shadidi, wamefurahi sana wakulima na wenyewe wakatuonesha kwamba wao wamepata utaalamu mkubwa sana, walichukua mbegu ya shadidi ambayo punje moja unapata miche 37, wakachukua punje hizo wakenda wakapanda tatu paala wakavuna, wakapata miche 15. Kwa hivyo, waka-*prove* kwamba sayansi tuliyoitumia ya punje moja kwa miche 37 inaweza kabisa kutuondolea na kinamama wale wametuomba tuwaongezee eneo waweze kulima zaidi.

Kwa hivyo, nataka kuchukua fursa hii kuanza kuwashukuru sana wakulima wote wamefanya kazi nzuri, wameitikia sera ya serikali kwamba sasa lazima tujitosheleze wenyewe kwa chakula na kazi hiyo inaendelea vizuri. Kwa hivyo, waheshimiwa wasiwe na wasiwasi katika *investment* kwenye kilimo, tumejitahidi, tumejipanga vizuri, cha msingi zaidi ni wao wawakilishi mashirikiano.

Jana nilipata funzo sana kwenye jimbo la Mfenesini, nilikuta Mwakilishi, Mbunge, Diwani na Kikundi chao cha Ushirika pale wote wapo wamewasaidia hasa katika suala la kulipia umeme na tukichukua utaratibu huo mimi naamini kabisa gharama nyingi wanazopata wakulima zinaweza zikapungua na tukalima vizuri. Nataka niwapongeze sana wakulima kwa hilo.

La pili tumeambiwa vile vile tufanye *investment* kwenye uvuvi. Nataka tena nimshukuru Rais kwa kuanzisha kampuni ya uvuvi. Juzi amepata mwenyekiti mahiri naamini kabisa bodi itaanza kazi yake karibuni na meli mbili za mwanzo zitaweza kupatikana. Lakini kubwa zaidi ni *hatchery* ambayo tunaifanya sasa ambayo itatoa vifaranga 10,000,000 za samaki na majongoo.

Waheshimiwa jongoo mbichi kilo moja ni shilingi 50,000; akikaushwa akipatikana kilo moja anafika mpaka US$ 200, soko liko kubwa, *hatchery* sasa tunayo na bahati nzuri tumeshaanza mashamba ya kupanda majongoo, nawaomba Wawakilishi katika maeneo yao waliyonayo wakawatayarishe wananchi waanze kufuga majongoo. Ni biashara kubwa ina kipato kikubwa, ina soko la uhakika na tuna uwezo kabisa wa kusafirisha kwa tani nyingi sana. Hivyo nawaomba sana tufanye. Nataka niwashukuru sana kinamama mwakilishi hapa alikuwa anazungumzia ushiriki wa kinamama. Ushiriki wa kinamama katika kilimo ni asilimia 78, kila unapokwenda asilimia 78 ni akinamama, nataka niwashukuru sana kinamama kwa kuitikia hiyo na ndio maana katika mwani kuna kaya 24,000 wanawake ni asilimia 88. Kwa hivyo, ushiriki wa wanawake katika kilimo ni mkubwa sana ningeomba waendelee na juhudi hizo na sisi tuwasaidie.

Vile vile nataka niishukuru sana benki yetu ya kilimo ambayo imekubali kuja kufanya *investment* kubwa. Hii itasaidia sana kuondoa lile tatizo ambalo nimelizungumzia la *investment*,

kwa sababu *investment* imegawika mara mbili, kuna upande wa serikali na kuna upande wa *private sector* kusaidia. Hii benki itasaidia upande wa *private sector* ili iweze kuwekeza katika kilimo. Kwa hivyo, na hilo nasema wasiwe na wasiwasi nalo hilo limefanyika vizuri sana.

Mhe. Naibu Spika, kazi nyengine iliyoko ni suala zima la ufugaji wa samaki. Sasa hivi kama nilivyosema hapo nyuma tunazo *pond* 152 lengo hii *hatchery* ikishamalizika tuhakikishe kabisa ma-*pond* haya tunazalisha samaki kwa wingi ili kuondokana na tatizo la utapia mlo, lakini vile vile kupata kitoweo cha kutosha. Kwa hivyo, nasema kwa jumla wizara imejipanga vizuri na serikali imejipanga katika suala hilo la uwekezaji kwenye kilimo.

Mhe. Naibu Spika, jambo ninaloliomba kwa Waheshimiwa ni suala zima la kusimamia mazingira yetu, tunajitahidi sana kulima lakini kwa kweli uvamizi wa mabonde umekuwa mkubwa sana, ukataji wa miti umekuwa mkubwa sana na tatizo la hali ya hewa linatusumbua sana. Serikali imeamua kuwekeza katika umwagiliaji maji ndio kitu cha uhakika lakini itafanikiwa zaidi kama na sisi tukijitahidi vyanzo vya maji kuvitunza, vyenginevyo tutaendelea kuchimba maji kwenye visima vyanzo vya maji vitakuwa vimekauka na hatimaye hata maji chini nayo vile vile yatakuwa na athari ndani yake. Naomba sana hili tulisimamie kwa pamoja na sisi tunasema tuko tayari kushirikina na wao kikamilifu.

Mhe. Naibu Spika, nilitaka kusema jambo moja bajeti ambayo imeondosha au inapunguza utegemezi ni bajeti ya kusifiwa sana, na hii haifanyiki kama serikali haiko makini, kama kiongozi wetu hayuko makini, leo tumeteremka katika utegemezi kuwa na asilimia 7.4; Kenya wenye uchumi mkubwa kabisa ni asilimia 4. Kwa hivyo, tunaonekana tumefanya kazi kubwa sana tena katika kipindi kifupi sana. Hili lazima tujipongeze sote, lakini zaidi tumpongeze nahodha wetu anayesimamia mana bila ya yeye mwenyewe kuwa na nidhamu na anayo akalisimamia hili jambo tusingefika hapa tulipofika. Nidhamu ya kusimamia matumizi ndio iliyotufikisha hapa ningeomba tuendelee, tukapitisha sheria za matumizi, naomba sana kabisa kama hatukusimamia matumizi kikamilifu, kama hatukisimamia mapato kikamilifu, kama tutakuwa na muhali katika watu kuwatoza katika vipato bado hali yetu ya utegemezi itakuwa inaendelea.

Lakini nasema juhudi iliyochukuliwa ni kubwa inawezekana kabisa mwaka huu hii asilimia 7 tukapambana nayo na ikaondoka kama tutakuwa sote tumeungana na wizara na taratibu ambazo tumekubaliana na serikali. Nasema hili ni jambo kubwa Mhe. Naibu Spika, wengine wanaliona kama dogo lakini ni kubwa wenzetu hawalali katika kuhakikisha fedha inapatikana inatunzwa vizuri, tumemsikia Waziri wa Fedha hapa watu kawachukulia hatua mbali mbali. Ningeomba juhudi hizi ziendelee ili tufike pahala pazuri bajeti ikiwa inajitegemea tuna jeuri katika nchi.

Nchi zote zinazojitegemea ndizo zinazoleta jeuri, lakini sisi tutakosa jeuri kama tutagemea watu wengine na tumeona mtihani mara hii, kwamba kumbe wenzetu wakitwambia hawataki kutusidia ndio tumepata nguvu ya kusimama wenyewe na tumesimama vizuri na mimi naamini kabisa tukiendelea na utaratibu huu tutaweza kabisa kupiga hatua.

Mhe. Naibu Spika, nilitaka kusema hayo mambo makubwa ili niwahakikishie tu wananchi Wizara ya Kilimo, Mifugo, Maliasili na Uvuvi imejipanga vizuri kuna sekta ya mifugo, tunafanya vizuri nayo karibuni sana mtaona mabadiliko yake. Lakini nasema ni mapema

mshaipitisha ya kilimo tungoje bajeti kubwa ipite mtaona matokeo hapo baadae. Mhe. Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

Mhe. Waziri Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, mimi pia naomba kuchukuwa nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango na watendaji wote alionao katika wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya. Mimi nina imani kubwa kwa sababu Waziri wa Fedha ni mchumi kama mimi mbobezi wa mambo haya ana uwezo wa hali ya juu na mtendaji mzuri kabisa na watendaji wake wote akiwemo Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Mtendaji wa *secretary* wa Tume ya Mipango na wote.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa na mimi nichangie hoja za baadhi ya Wajumbe ambao wamechangia. Lakini kabla ya kuzichangia zile hoja na nadhani niziunganishe ili tuweze kuwa na *flow* ile ambayo inatakiwa iwepo.

Kwanza ningeomba Mhe. Naibu Spika, niwashukuru Waheshimiwa wangu wa Baraza hili na wananchi wote wa Zanzibar kwa kuangalia hali halisi ya dunia tulionayo, inatusaidia kujua hasa nini kama Zanzibar tunatakiwa tufanye na vile vile kujua jinsi ya serikali yetu inavyojitahidi na kuipongeza katika kuinua uchumi wa nchi yetu. Nyote mnaelewa msuguano uliopo duniania sasa hivi kati ya Marekani na *European Union* (*EU),* Marekani an Ulaya. Lakini pia mnajua msuguano uliopo kati ya Ulaya na Ulaya kwa sababu Waengereza wametoka Ulaya wamebakia Ulaya hawako Uengereza.

Lakini pia mnajua msuguano ulipo ndani ya dunia, sasa hivi kuna vita zinaendelea nchi za kiarabu, lakini pia kuna msuguano kati ya Warabu na Warabu wenyewe. Nimesikia Serikali ya Qatar ilivyoekewa vile vile *sanction* kwa ajili ya mambo ya kiuchumi na kadhalika. Kwa hiyo, Mhe. Naibu Spika, tujiulize sisi Wazanzibari tuko wapi tunajiandaa vipi Mheshimiwa kwa hali halisi ilivyo tunakokwenda mbele mambo yanaweza yakabadilika kabisa kabisa, tukawa mipango yetu tunayopanga ikabidi tuwe na mipango mingine ya kujihami na mambo ambayo yatakayotokea katika dunia.

Sasa hivi suala zima la *free trade* tunasema biashara huria imeshaingia katika mtihani mkubwa kwa sababu nchi nyingi zinazungumzia sasa hivi hasa nchi kubwa kama hii Marekani inazungumzia kujiangalia yeye yenyewe kiuchumi na yeye yenyewe kibiashara. Hiyo nayo vile vile inaweza kutuletea athari katika baadhi ya mambo ambayo hasa katika sekta zetu za biashara na sera za viwanda.

Mhe. Naibu Spika, nadhani kwa msingi huo tunahitaji tubadilike kama Zanzibar tubadilike tujitegemee zaidi tufanye kazi zaidi tujipange zaidi. Lakini kubwa Mhe. Naibu Spika, tujitolee zaidi moyo wa kujitolea uzidi kuhimizwa na tuweze kupiga hatua tunazozitaka.

Mhe. Naibu Spika, niseme tu kwamba kipindi hichi kilichokuwa cha maendeleo tukianzia katika mapinduzi ya maendeleo yaliokuwepo hasa katika sekta ya viwanda. Huko nyuma katika miaka ya karne ya nyuma mapinduzi ya viwanda tuliyakosa sisi tulikuwa chini ya utawala tukitawaliwa. Lakini baadae mapinduzi yakaja ya kilimo bado Afrika hatujafika na Tanzania hatujafikia huko mapinduzi ya maziwa tunataka tufanye mapinduzi ya Maziwa sio tu kuzalisha ng'ombe wa maziwa lakini na wananchi nao watumie maziwa kwa sababu ni miongoni mwa

mafanikio ya viwanda ambavyo kwa mfano Zanzibar tunavyo lakini matumizi maziwa bado madogo na mapinduzi haya hatujafikia.

Kuna Mapinduzi ya *Blue* kwa upande wa mali za asili za baharini na uvuvi, vile vile kuna mapinduzi yaliyotokea kwa upande wa mapinduzi ya nne yanaitwa sasa hivi Mapinduzi ya *digital*. *Digital* sasa hivi tayari tumeshaingia katika Mapinduzi hayo. Lakini ukiangalia nini kilichokuwa cha msingi wakati ule kwa mfano mapinduzi yale ya viwanda wakitumia zaidi mashine za maji na mvuke kuendesha mashine zao. Mapinduzi yaliyofatia wakitumia zaidi nguvu za umeme kuzalisha bidhaa nyingi *mass production*.

Lakini vile vile mapinduzi ya sasa hivi tunayozungumza sisi ya *TEHAMA* tunategemea kutumia ziadi *TEHAMA* na mambo mengine. Kwa hivyo, swali linakuja tumefika wapi na tutawezaje kutumia mapinduzi hayo. Kuna haja na Zanzibar sasa hivi tuweze kutumia mapinduzi wanasema kuruka kama anavyoruka chura kwa ajili ya kuweza kuleta maendeleo ya haraka. Bado kasi ya kufuata mapinduzi hasa haya ya *TEHAMA* ya *digital* bado kasi ni ndogo lakini serikali imepiga hatua kubwa sana na tujipongeze kama tumo katika maendeleo hayo.

Mhe. Naibu Spika, bajeti hii tumeiita Bajeti ya Mageuzi na Bajeti ya Huduma Bora za Jamii. Mhe. Naibu Spika, tujiulize tuseme kwamba hili neno halikuja hivi hivi, hili neno kwamba Bajeti ya Mageuzi na Huduma Bora za Jamii limekuja kwa ajili ya makubaliano na mazingitio na mkatati kabisa kabisa wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Mheshimiwa wetu Dr. Ali Mohammed Shein. Hapa tumefikia matumizi yetu tumefikia *figure* ya *Trillion*, huko nje wanauliza sasa hii *trillion* yaani ni nambari iliyokuja hivi hivi tu. Hapana *figure* hii ya *Trillion* katika bajeti yetu imekuja kutokana na kazi tulizozifanya huko nyuma na mkakati wetu wa mbele na matumaini ambayo tumewawekea na vile vile vipaumbele ambavyo tumevipanga. Tumengia katika matumizi yetu ya Bajeti yetu imefikia *figure* hiyo ya *trillion*.

Mhe. Naibu Spika, hapa tulipo uchumi wetu unakuwa lakini pia uchumi unakuwa lakini na watu vile vile wanakuwa, *figure* za Sensa 2012 zilikuwa watu milioni moja laki tatu, lakini tunaambiwa leo mwaka 2017 wananchi wa Zanzibar tunafikia milioni moja mia nne na sitini elfu, hawa ni sawa sawa na milioni 1.46 milioni ni watu hawa wameongezeka.

Lakini pia tukiangalia katika hii hesabu tuangalie sasa suala zima la vijana wetu *population censer*. Kuna vijana hapa Zanzibar asilimia 43 kati ya miaka 15 na 35 lakini ukichukuwa chini ya miaka 15 asilimia 43. Ukichukuwa kuanzia miaka 15 na 35 ni zaidi ya asilimia sitini na humu asilimia 3 tu ndio zaidi ya watu ambao wamefikia miaka 60. Hii Mhe. Naibu Spika, tuangalie hii ni tegemezi kwa hivyo, hata kama tumo katika uchumi tunaendea katika bajeti ya *trillion* bado kuna mambo ya ziada tunatakiwa tuyafanye. Ukiangalia idadi ya wategemezi kwa mujibu wa *household budget* iliyofanywa juzi tu mwaka jana unakuta utegemezi kwa watu kwa Zanzibar kwa kila watu 100 wa umri wa miaka 15 hadi 64 kuna watu wategemezi 86 hiyo ni hesabu ambayo tunatakiwa lazima tujitahidi kufanya mambo makubwa zaidi kwa ajili ya kuweza kuendeleza uchumi wetu.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, ukiangalia Kaya kwa sababu ningeowaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu hizi taarifa za Kaya zilizotolewa wakazisoma wakazielewa vizuri sana zinatueleza jinsi tulivyofika hatua, serikali imepiga hatua kiasi gani inatueleza katika

maeneo mbali mbali tumetoka wapi tunakwenda wapi kuna mifano, matumizi ya umeme, matumizi ya vyoo, matumizi ya skuli huduma mbali mbali yanatueleza tumetoka wapi tunakwenda wapi na yote yanatueleza ni mambo mazuri sana yamefanyika na serikali yetu inayoongozwa na Jemedari wetu Dr. Ali Mohammed Shein.

Mhe. Naibu Spika, vile vile ukiangalia umaskini kati ya vijiji na mjini na hii nimetaka niiseme kwa sababu lazima mipango yetu tu-*target* kwa sababu sasa hivi tumefikia ukingo wa hii *vision* tunayoiita 2020. Maana yake sasa hivi tunajiandaa kwenda katika *vision* nyengine inayotupeleka na vizuri Mhe. Dr. Ali Mohammed Shein amekuja hivi *vision 2020*, lakini anaondoka baada ya uchaguzi 2020 yeye ndie atakaetutayarishi na *vision* ya *2020 beyond*. Kwa hivyo, ina maana kwamba ni sisi Wawakilishi tuna majukumu ya kutayarisha sasa hivi *vision* hiyo ambayo itatuvusha tena kwa siku ya mbele.

Mhe. Naibu Spika, maana ya *transformation* maana ya mabadiliko ya bajeti hii ni kwamba bajeti hii na inayokuja na inayokuja inataka tujiandae sasa tunaingia katika *vision* nyengine katika maeneo ya uhakika ambayo itaongeza uchumi wetu na yatakayotuwezesha uchumi wetu uingie katika uchumi wa kati ambao ni uchumi wa viwanda na watu ambao ni uchumi wa kati na moja ya sifa zake ni maendeleo ya viwanda.

Mhe. Naibu Spika, tukiangalia bajeti hii na kumalizia hiyo *vision 2020* Mhe. Waziri wa Fedha ametwambia vipaumbele miundombinu kwa mfano Uwanja wa Ndege huu wa *terminal II*, bandari ya pili mpya, barabara zinazojengwa na kadhalika. Sekta ya viwanda ni mikakati mikubwa na mizuri endelevu, vile vile kwa upande wa Sekta ya Utalii yote haya Mhe. Naibu Spika, yatatusaidia sisi kuingia katika hiyo *vision* inayokuja tukiwa tunaingia na *push* inayotakiwa. Ndio maana Waziri wa Fedha akasema bajeti hii ni ya mageuzi. Lakini pia ni bajeti ambayo imeangalie sekta za jamii tumeona afya, tumeona elimu jinsi ya bajeti ilivyopangwa na mikakati ambayo imewekwa.

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa nijibu michango ya Waheshimiwa Wajumbe kwanza Mhe. Simai Mohamed Said na Mhe. Hassan Khamis Hafidh walizungumza kwa kina masuala mbali mbali ambayo nitayajibu. Kwanza lilizungumzwa suala la biashara na Bara kwamba biashara na Bara imepungua.

Ni kweli Mhe. Naibu Spika, sisi biashara na Bara Zanzibar kupeleka biashara Bara zimepungua, lakini biashara kutoka Bara zinaendelea vile vile kuwa nyingi, kuna kipindi hapo nyuma tulikuwa tumeweza kuwa na *balance* kati ya sisi na biashara za Bara. Sababu moja ya kwanza ni kwamba kulikuwa na vikwanzo vizivyoeleweka, vikwazo vya aina gani kwa mfano unaambiwa kwamba unatakiwa ufungue *argent* kule Bara kuna kampuni fulani mfano kampuni ya chai inapeleka chai wameambiwa hamna kupeleka chai mpaka mfungue *argent* na hiyo haimo katika kanuni na taratibu sheria na *regulation* za biashara. Lakini pia huo ni mfano mmoja.

Kuna mfano mwengine ni kwamba utawala wanavyosema, utawala wa kusimamia sekta za biashara na viwanda na uwekezaji ni tafauti. Sisi tunaweka sheria zetu na wao wanaweka sheria zao. Lakini nayo hiyo siyo sababu kwamba biashara zisivuke kutoka Zanzibar kwenda Bara nayo bahati mbaya inachukuliwa nayo ni sababu.

Lakini jengine ambalo linalochukuliwa kama ni sababu ni kubadilika kwa taratibu za kodi. Nilisikia mwaka jana kati kati hapa utaratibu wa kodi za *VAT* zilivyokuja nazo vile vile zikasababisha baadhi ya biashara zetu zilivyokwenda kule nazo zilizotoka kule kuja Unguja nazo zilipata matatizo. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, naomba niwatoe hofu Waheshimiwa Wajumbe kwamba suala hili serikali zote mbili zinalielewa na tumekubaliana sasa mwanzoni mwa mwezi unaokuja serikali yetu na Serikali ya Muungano zikae pamoja kuzungumzia vikwazo vinavyioitwa siyo vikwazo vya kodi ili kuona kutatua tatizo hili na vile vile tumepata mtaalamu sasa hivi ambaye yumo katika kamati, kuna kamati kule Serikali ya Muungano inayosimamia masuala ya kuondosha vikwazo visivyokuwa vya kodi. Kwa hivyo, tuna mtaalamu na ameshaanza semina mbali mbali kuwafahamisha wadau wote wafanyabiashara jinsi ya kuweza kutambua vikwazo hivi na vile vile kuweza kuviondosha.

Wito wangu nataka niseme kwamba Tanzania Mhe. Naibu Spika, ni moja na moja sababu ya Muungano ni kusababisha kuwe na urahisi wa biashara ili kukuza uchumi na kukuza maendeleo ya nchi yote Tanzania. Kwa hivyo, kama vikwazo hivi vitaendelea kwa kweli vitatuathiri sana sisi tulioko Zanzibar hata kunako sera zetu za kujenga uchumi na kujenga viwanda na zile sera zetu za kushajihisha wawekezaji. Kwa hivyo, lakini naelewa kwamba kuna vikao vya Muungano na safari hii baada ya kukaa sisi na wizara zinazohusika tutaweza kuwa na jawabu zuri la kuweza kuondosha vikwazo hivi. Kesi zimekuwa nyingi na ziko lakini matarajio yangu kwamba serikali ya Chama cha Mapinduzi sikivu itafikia mahali kuwa na utaratibu ambao rahisi na mzuri wa biashara kutoka Zanzibar ili ziende Bara bila ya kuwavunja moyo wawekezaji.

Jengine alilozungumza Mhe. Simai Mohamed Said ni kuhusu mpango wa kuanzisha viwanda. Niseme tu Mhe. Naibu Spika, kwenye bajeti yangu nilieleza lakini naomba nieleze tena katika mpango wa kuanzisha viwanda tunachofanya cha kwanza sasa hivi ni kupitia sheria ya viwanda naomba mkumbuke kwamba sheria ya viwanda ipo ya mwaka 1998. Maeneo mengi sana ya sheria hii hayakutekelezeka, kwa hiyo, tunapia sheria hii lakini tunapitia na sheria ya Ujasiri amali ya mwaka 2006 ambayo inazungumzia wenye viwanda wale wadogo wadogo, sheria hiyo imetoa pendekezo la kuanzisha Shirika la Viwanda Vidogo vidogo kama *SIDO* ambayo sheria yake itakuja kunako Baraza la Wawakilishi ili muijadili. Muhimu ni kwamba tunataka viwanda viendelezwe na viwe endelevu na viweze kuwapa tija wananchi wetu.

Pia tunapitia sera ya uuzaji wa bidhaa nje kwa sababu lengo kubwa ni kuongeza bidhaa zetu nje lakini tunauza zaidi bidhaa ambazo hazijategenezwa kwa mfano bidhaa za kilimo. Lakini kwa hii sera ya uuzaji bidhaa nje tunaipitia tena ili kutoa motisha na kutoa maelekezo na kuwasiadia wale ambao wanataka kuuza bidhaa zao nje ili waweze kuuza bidhaa zao nje kwa tija zaidi. Vile vile tunafanya mapitio ya utafiti wa maeneo *specially economic zone* au vile vile masuala mazima ya *free procesing zone* na masuala ya *EPZ* kwa sababu tunataka Zanzibar iwe kituo cha biashara kitakachoweza watu wote kuja kuweka biashara zao hapa na biashara zao ziweze kusambazwa katika maeneo mengine nje ya Zanzibar. Kwa hiyo, sera hiyo hizo zinatizamwa vile vile.

Lakini la mwisho kuhusu viwanda niseme tumeandaa mkakati na kuweka *priority* ku- *list* maeneo ya viwanda ambayo tunataka kipindi hichi Zanzibar yasimamie na haya ni maeneo ambayo yana tija kubwa. Kwanza tumesema viwanda vya vitu vya kilimo ambavyo Mhe. Waziri wa Kilimo amesema hapa *Agro Industry*. Viwanda vya pili ni viwanda vya vitu vya baharini

yaani *blue ecomonic* au *marine industry*. Eneo la tatu tumekubaliana kwamba liwe ni *light manufacturing*. Humu vitaingia vitu kwa mfano mambo yote ya viwanda vidogo vidogo ikiwemo madawa ikiwemo vyakula, ikiwemo vitu vya viungo na kadhalika.

Eneo la nne ni kwa upande wa viwanda vinavyotumia *TEHAMA* yaani vinavyotumia teknolojia ya Habari na mambo hayo yote yanayofanana na hayo. Huko, kuna tija kubwa sana Mhe. Naibu Spika, nchi za wengine sasa hivi vijana wanajiajiri kutegemea na mambo ya *TEHAMA* hapa Zanzibar tumeanzisha sasa hivi eneo la *incubation* tunawafundisha vijana wetu kupitia Afisi ya Wizara ya Wanawake na Watoto. Lakini pia tunahangaika zaidi kupata kituo kijiji kizima kwa ajili ya mambo ya *TEHAMA* na huo utaratibu juzi tu Baraza la Mapinduzi tumekubaliana kwamba ifanyike *concept paper* na itakapokuja baadae mwakani tutajua tunafikia wapi.

Mheshimiwa eneo la mwisho katika hiyo *priority* ya maeneo ya viwanda ni eneo la *Oil and Gas*. Kama mnavyojua tumo katika utaratibu wa kutafuta masuala hayo ya mafuta na gesi na hiyo ni sekta ambayo itatusaidia sana Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, alizungumzia pia kuhusu mambo ya *branding*. *Branding* ni jmabo ambalo hatuna neno la kiswahili bado lakini ni jambo ambalo tunatumia jina letu tunatumia vitu vyetu, tunatuma vitu ambavyo Mwenyezi Mungu ametuwezesha kama mfano karafuu ni jambo ambalo Mwenyezi Mungu ametupa. Lakini kuna mambo mengi ya utamaduni na mambo mengine mengine ambayo tukitaka tuyatumie haya kwa ajili ya kuendeleza viwanda kwa mfano kofia za Zanzibar, kanzu za Zanzibar masuala mazima ya kutumia *spice* hizi ambazo tunaweza tukafanya mambo ya *wellness* kwa watalii na kadhalika. Haya yote Mheshimiwa yanakuja katika suala zima la *branding.*

Niliulizwa Mheshimiwa kwamba je, Zanzibar ni *brand name*? Ukitaka kutumia *brand name* lazima ulisajili lile neno jina lenyewe ulisajili. Kwa hivyo, kuna mahoteli nje Zanzibar na kadhalika. Tunafanya utafiti kuona kwamba tunawezaje kusajili Zanzibar kwa ajili ya bidhaa zetu na hiyo *process* tutaianzisha kwa sababu tumeshafanya *branding* ya karafuu lakini tumeshauriwa tufanye *branding* kwa vitu vyote vya Zanzibar na kuifanya Zanzibar yenyewe kuwa ni *branding name* ambayo tutaitumia na mtu atakaeitumia vibaya atashitakiwa.

Mhe. Naibu Spika, vile vile kulikuwa na suala kuhusu mahusiano ya *private sectors* na serikali. Mimi naomba nikiri kwamba tuna mahusiano mazuri sana baina ya serikali na *private sectors*. Bahati mbaya sasa hivi *private sector* wana *chamber* wanavyombo vya *Chamber of Commerce* kwa sasa hivi *Chamber of Commerce* inapitia na wao vile vile mageuzi. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, unakuta kwamba bado hawajakaa vizuri.

Kuhusu Baraza la Biashara serikali imepitia mfumo mzima wa Baraza la Biashara na tumeona kwamba kuna haja ya kuboresha au kuufanya uwe mzuri zaidi. Kwa hivyo, sheria ya Baraza la Biashara tumeshaitayarisha na inakuja Baraza la Biashara pengine Baraza linalokuja Mwenyezi Mungu akipenda na katika sheria hii Mhe. Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ndiye Mwenyekiti wa Baraza la Biashara, na Katibu Mkuu Kiongozi ndiyo Katibu wa Bureau hii ya Baraza la Biashara na kuna wajumbe nusu kwa nusu ambao wa serikali na wanyabiashara ambao watakaa kujadiliana mambo yanayotakiwa.

Pia kumependekezwa kuwa na Mabaraza ya Mikoa kwa ajili ya kuwashirikisha wenzetu walioko Mikoani na Wilayani. Naomba hii niunganishe na dhana yetu kutoka katika *SMIDO* ya kutaka kwamba wilayani viwanda vielekezwe katika wilaya, kila wilaya wana uwezo wa kufanya baadhi ya mambo. Kuna wilaya kwa mfano Kaskazini wao wanaweza kuzalisha vitu mbali mbali kama bizani, manjano, tangawizi na kadhalika. Kwa hivyo, kila wilaya inatakiwa iwe na kiwanda kinachohusu kuanzia kulima mpaka kumalizia kuweza kutengeneza kitu na kuuza

Kwa hivyo, ni kweli Baraza la Biashara ni muhimu, lakini haliwezi kuhamishiwa Tume ya Mipango, kwa sababu utaratibu wake umeshapangwa na ushakubalika kwamba Baraza la Biashara libakie chini ya ofisi ya mwenyewe Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kwa hivyo, tutaendelea na utaratibu huu kwa sababu tumeona ni utaratibu ambao unatoa nguvu na unasimamia vizuri zaidi wafanyabiashara zile kero zao na matatizo yao yanapotokea, kunakuwa na serikali chini ya Mwenyekiti mwenyewe Rais wa Zanzibar ndiye ambaye anasimamia kwa kutuagiza mawaziri ili kutekeleza kuondosha zile kero zinazosababisha biashara zisiende vizuri.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo nadhani la mwisho lilizungumzwa na Mhe. Hassan Khamis *Diaspora* na hasa kuhusu masuala ya Tume ya Bei, na wengine wajumbe walizungumza kuhusu vyakula bei zimepanda na vile vile kulikuwa na hofu au tafrani iliyoingia nchini hapa kama kuna michele ya plastiki na kuna tambi za plastiki. Nataka nichukuwe dakika kama moja tu hapa nizungumze, kwamba utaratibu wa Tume ya Bei tumeondokana nao miaka mingi bali pale tulipokuwa tumesema serikali isifanye biashara, lakini tukaleta utaratibu mwengine wa mashirikiano kati ya wizara yangu vitengo vinavyoshughulikia masuala ya walaji na masuala ya biashara, ili kukaa na wafanyabiashara kujipangia bei.

Mhe. Naibu Spika, nina masikitiko sana niliposikia taarifa aliyosema Mhe. Hassan Khamis kwamba bei za vyakula vimepanda katika mwezi wa Ramadhani. Wafanyabiashara tunawapa *exemption* na mwaka huu *exemption* imetoka mapema sana. Waziri wa Fedha na Mipango alitoa *exemption* mapema kwa wakati na wafanyabiashara walionunua mali walipewa *exemption* hiyo mapema. Kilichotokea Mhe. Naibu Spika, bahati mbaya bandarini kuna meli zilizokuwa na vyakula zilichelewa kufika pale zinapotakiwa kushusha vile vyakula, na ndio maana wafanyabiashara wadogo wadogo wakachukua hili jambo wakalifanya kwa faida zao, kwa sababu hakukua na sababu wao bei wazipandishe. Kwa sababu kodi imeondoshwa na bidhaa zimeingia nchini tokea wiki iliyopita meli ilikaa kwenye gati ilishusha vyakula, ilishusha tende, unga wa ngano, sukari na imeshusha mchele. Hakuna sababu wafanyabiashara hawa kuweza kupandisha bei.

Mhe. Naibu Spika, mimi mwenyewe binafsi niliulizia kwa wale ambao ni waagiziaji wa vyakula wakanihakikishia kwamba wao hawakupandisha bei. Kwa hivyo, naomba nichukuwe nafasi hii kutoa onyo kali sana kwa wafanyabiashara hawa *retailers* ambao wamechukua nafasi hii kuwapa dhiki wananchi wetu kwa kuwapandishia vyakula michele, tende, unga ningewaomba waache mara moja tutawafuatilia na tukiona kuna watu wamefanya hivi basi tutawachukulia hatua kali, kwa sababu wamepewa *exemption* watu kwa ajili wananchi wetu wapate maslahi yao Ramadhani wafunge vizuri bila ya kuwa na bughudha ya bei, kwa sababu watu wetu Mhe. Naibu Spika, hawana uwezo.

Jengine Mhe. Naibu Spika, naomba nimtowe wasi wasi Mhe. Hassan Khamis kila tukikuwa Wizara yetu tutajipanga vizuri, kuhakikisha kwamba kutakuwa kuna mfatiliaji wa hali ya juu kuona kwamba hizi bei tunazokubaliana wafanyabiashara, basi bei zile zinasimamiwa vizuri ili zisipandishwe kiholela. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, jengine kuhusu vyakula hivi vya mchele, tambi za plastiki na vitu vya plastiki. Mhe. Naibu Spika, watu wamekuwa na *concern* sana, naomba niwatowe wasiwasi hakuna vyakula hivyo. Tume-*check* hata kule Bara. Bara wamefanya *inspection* kwa baadhi ya maduka, wakakuta kwamba hakuna vyakula vya plastiki si mchele wala tambi za plastiki. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, sisi pia tume-*check* taarifa niliyopewa leo asubuhi hakuna tambi za plastiki. Kwa hivyo, wananchi msiwe na wasi wasi vyombo vyetu vipo, chombo cha Wizara ya Afya cha vyakula na madawa kipo imara sana, chombo chetu cha *ZBS* kiko imara sana na sisi wafuatiliaji tukiona mara moja kama vyakula vilivyoletwa haviridhishi katika afya ya wananchi tunachukua hatua. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwa kusema naunga mkono bajeti hii. Lakini pia naomba nimpongeze sana Mhe. Rais na nasema sisi wote wajumbe wa Baraza lako na wananchi wa Zanzibar tumpongeze, kwa sababu ni Jemedari mzuri, maagizo anayotupa tunayafanyia kazi na ndio haya yametufikisha leo tumo katika trilioni. Niseme tu hakuna kiongozi mzuri yule mwenye imani na wananchi wake na mheshimiwa wetu ana imani sana na wananchi wake. Tunapewa maagizo mara kwa mara kuangalia hali halisi inavyokwenda ya taifa letu, kiuchumi, kibiashara, kiafya na kielimu. Kwa upande huo tuko tayari niseme na Wizara yangu Biashara, Viwanda na Masoko tuko tayari kuendelea. Kama nilivyosema pale mwanzo, bajeti mbili zilizobakia ni kujipa nguvu zaidi, kujitayarisha zaidi ili kuingia katika hilo deni tulilosema la mageuzi katika *vision* inayokuja ya 2020. Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko. Sasa nimkaribishe Mhe. Mahmoud Thabiti Kombo Waziri wa Afya ili na yeye aweze kujibu baadhi ya hoja. Mhe. Waziri karibu.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa mimi nimshukuru Rais wetu Dk. Ali Mohammed Shein. Katika Sekta ya Afya. Nataka nitowe uchanganuzi ambapo Waziri wa Fedha na Mipango alitoa katika maelezo yote. Katika uchanganuzi haijapata kutokezea asilimia kuongezeka katika bajeti ya serikali upande wa afya kama mwaka huu, katika historia ya Zanzibar, imeongezeka *almost* 20 *percent*. Nilieleza hapa wakati najibu mwaka jana tulikuwa bilioni 59, safari hii tuko 83. Tofauti na mama yangu hapa Bi Amina Salum Ali Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko. Yeye anazalisha zaidi, lakini anatumia kidogo. Sisi tunatumia zaidi, tunazalisha kidogo, kwa sababu tunatoa huduma kwa jamii moja kwa moja.

Lakini la pili sera. Mhe. Rais ameendelea kusimamia sera ya kutoa matibabu bure hapa Zanzibar na ndio maana kuongezeka kwa bajeti hii. Naomba wananchi wote walione hili walikubali na walipokee na wampongeze, kwa sababu sehemu nyingi sasa hivi duniani pamoja na wenzetu Tanzania Bara, baadhi ya huduma zinakuwa za malipo. Tunakwenda siku zote tunapata huduma

hizo tunaona, baadhi ya huduma zinakuwa za malipo, sisi hapa zote bado. Ile zile ambazo hazimo katika huduma muhimu mgonjwa huambiwa akatafute kwingine ama huchangiwa. Lakini hata wagonjwa wa nje pale inapokuwa huduma haipatikani hapa, wagonjwa wa nje tumekuwa sisi kama Wizara ya Afya tukiwapeleka moja kwa moja nchini India. Kwa mwaka jana *almost* Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa Dk. Ali Mohammed Shein imetumia bajeti ya takribani milioni mbili dola kuwapeleka wagonjwa nje ya nchi kutibiwa kwa yale matibabu yaliyokuwa hayapatikani hapa. Hao wamepelekwa bila ya ubaguzi wowote, kuna baadhi ya wajumbe walisema wanapelekwa kwa matabaka. Hawa walipelekwa bila ya ubaguzi wowote. Wamo wakulima ndani, wamo wakwezi, wamo wavuvi na wengine wote. Muhimu ufuate utaratibu wa kupitia kwenye bodi ambayo inathibitisha ili mgonjwa apelekwe nje.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba kuchukua fursa ya kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Fedha. Nilikuwa nimesimama na mchumi mmoja hapo nje leo na mimi nilikuwa nahitaji kuuliza kidogo maswali, ili na mimi niweze kushiba. Mimi ni *engineer by profession*, sasa ikiwa kuna swali la uchumi, basi lazima sisi ma-*engineer* huwa tunawauliza watu wa uchumi. Nilipomuuliza akaniambia hivi vitabu vya Mhe. Waziri cha kwanza, cha pili na kile cha tatu hii ni *PhD cases* ndio maana akaitwa Dk. Khalid jinsi ya vitabu hivi vilivyopangwa, nimekaa na mchumi. Akaniambia humu ndani kuna *results prosperity* Zanzibar yaani matokeo yale ya hali njema tunayokwenda nayo na tunayoendelea nayo.

Mhe. Naibu Spika, kuna *decentralization by devolution* ama *devolution by decentralization* yote mawili yanawezekana, tunakoelekea kwenye masuala ya ugatuzi kuna masuala ya petroli na gesi, kuna masuala yote ambayo yamepangiliwa vizuri. Yule mtaalamu wa uchumi alikuwa ananiambia baada ya hotuba ya Mhe. Rais aliyoitoa humu Barazani hii ya pili leo ambayo imepangika kwa mlolongo. Hotuba ya kwanza ni ya Mhe. Rais, kwa sababu ile ilitoa mpango wetu mzima tunaokwenda nao, basi hii pia imepangika naomba nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa kuja na kitu kama hiki kizuri. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mwelekeo uko *clear* sasa ni juu yetu sisi kutekeleza. Naomba niwapongeze sana Wizara ya Fedha na Mipango Baraza hili hili la Wawakilishi lilitoa kibali cha mkopo *almost 8 billion, to the tune of eight billion* ilitoa hapa, lakini waziri ameweza ku-*sustain* na uchumi, amekopa *only 24.5 percent*, katika ile *eight something billion* amekopa *only 24.5 percent* mimi nampongeza sana, maana kila ukikopa nao mzigo wa kulipa unazidi kuwa mkubwa, kwa hivyo uchumi umekuwa mzuri nashukuru sana. Naomba niwapongeze sana Mhe. Waziri na watendaji wake. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, pale kuna ma- *professor* wengine, kina *professor* Khamis Mussa wao ndio wanajua kuyapangilia haya na hata ya Wizara ya Afya tukikwama tunakwenda kwao wanatupangia vizuri, vipi tufanye vipi dawa tununue kwa muda na vipi zile dawa zisije tukaishiwa halafu tukaja kuwa hatuna. Kwa hivyo, tunajaribu kupanga mipangilio mizuri ya kununua kwa wakati ili tusiishiwe.

Mhe. Naibu Spika, baada ya pongezi hizo mimi naomba ni-*relate* leo afya na uchumi wa nchi. Mhe. Naibu Spika, wengi hawajui kama hiki kipindupindu chetu tulichokuwa nacho sasa hivi tunaendelea nacho tunakichukulia *very lightly* kinaweza kuathiri uchumi mzima wa nchi. Jana katika kupekua pekua nilikuwa napitia historia ya mwaka 1978 nikiwa mimi nina umri wa miaka

9 wakati huo. Katika historia ya mwaka 1978 Zanzibar iliathirika sana na kipindupindu na yote ilikuwa kwa sababu tulikuwa tumechukulia *very like* wakati huo.

Mhe. Naibu Spika, naomba nikuambie kipindupindu kikizidi hata wewe hutokuja hapa kwenye kiti hicho kukaa, Waziri wa Fedha na Mipango hatofanya kazi yake vizuri, watu wa *collection ZRB* na wengine hawatoweza ku-*collect* vizuri, mwaka 1978 hali hiyo ilikuwepo ya karantini nchi nzima. Mtu aliyekuwepo Kaskanzini haji Kati, aliyekuwepo Kati hendi Kusini na aliyekuwepo Kusini haji mjini. Kwa hivyo, naomba sana kwa kupitia Baraza lako tukufu na viongozi wote, pamoja na wawakilishi wa majimbo pamoja na wananchi wote ambao wanatusikiliza, sasa hivi kipindupindu tusikidharau kilichokuwepo nchini kwetu ni lazima tukifanyie kazi kwa pamoja. Lisionekane ni la Wizara ya Afya tu, hili ni jukumu letu sote kwa pamoja uchumi wetu unaweza kuathirika.

Mhe. Naibu Spika, mwaka jana Wizara ya Fedha na Mipango ilitumia bilioni 2. 2 kwa sababu ya kipindupindu tu, ambapo hizo bilioni 2.2 zingeweza kutumika katika mambo mengine mengi ambayo nchi yetu inahitaji. Mwaka huu halikadhalika wameshatoa fedha nyingi hatujajua tutafikia ngapi mpaka kipindupindu kitakapomalizika. Pale iliongelewa habari ya kambi za kipindupindu, wengine wanasema tuzihamishe, wengine wanasema tuzifunguwe mpya na wengine sijui tuzipeleke wapi, hatuwezi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutazama hali halisi na baada ya kutazama kwa mtazamo mpana tumeona pale Chumbuni ndio patakuwa kambi kuu ya kipindupindu. Kwa sababu mgonjwa wa kipindupindu kila ukim-*transfer* muda mrefu ama masafa marefu basi unazidisha *risk* ya *infection* njiani. Tumekaa na wataalamu wamekuja wataalamu wa dunia wa masuala ya kipindupindu wamesema hii iwe ndio *main camp*. Tumefungua kambi ndogo ndogo kama vile Gamba na kwengineko Makunduchi tulifungua, lakini zile ni *temporary*. *Temporary* zinafunguliwaa kwa sababu ya wingi wa wagonjwa na hiyo hiyo kuhofia kuwaleta kutoka pale mpaka kuja huku Chumbuni ikaja kutokea athari kubwa zaidi. Kwa hivyo, nawaomba wale Waheshimiwa Wajumbe waliochangia suala la mambo haya ya kambi watuvumilie kwa sasa hivi tutaendelea kuwa nayo.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu Kitengo cha Saratani. Kuna baadhi ya Waheshimiwa Wawakilishi, naomba niipongeze sana hotuba iliyosomwa na Mhe. Abdalla Ali Kombo kaka yangu, na yeye hotuba yake imepangika vizuri, maana ile kama ya Dk. Khalid *PhD* yake kama *Bachelors,* bado ana muda wa kufikia na yeye *PhD*. Lakini hotuba yao imepangika vizuri sana na mule pia walitaja kuhusiana na habari ya saratani.

Mhe. Naibu Spika, Kitengo cha Saratani tumekianzisha lakini bado hatujaanzisha wodi maalum. Hivi sasa tuko mbioni kulifanyia kazi, majengo yetu yakipata nafasi ya kutosha baada ya matengenezo makuu, basi na Kitengo cha Saratani. Hivi sasa tuna madaktari wawili kwa mara ya kwanza wazalendo ambao wako pale Mnazimmoja Hospitali, hawa wanapatikana pale Mnazi Mmoja tu, na katika bajeti nilisema kwamba kwa mara ya kwanza pia tumepata dawa za saratani ambazo zimeingizwa katika mfumo wa kutoa tiba ama kupunguza makali ya ugonjwa wa saratani Zanzibar. Haya tumeshaanzisha tunawaomba Waheshimiwa Wawakilishi watuvumilie watupe muda, tukishapata wodi maalum basi tutaanzisha wodi angalau vitanda 10 mpaka vitanda 15 kwa ajili ya wagonjwa hawa, wale ambao hawataweza kwenda kule *Ocean Road* ama wale

waliokuwa wamesharejeshwa kutoka *Ocean Road.* Sasa hivi wengi wanachanganyika na wagonjwa wengine katika wodi nyengine.

Mhe. Naibu Spika, kumezungumziwa suala la Binguni pia nimeshalitolea maelezo, hatua zilizokuwepo sasa hivi tumeshapata fedha za *feasibility study,* tutafanya *feasibility study* na wenzetu *Ardhi institute*. Tumekwenda kwa *Ardhi institute* wenzetu, kwa sababu *Ardhi Institute* wamefanya Hospitali ya kisasa ya Mloganzila.

Mhe. Naibu Spika, ikiwezekana naleta ombi kwako tuwaandalie wawakilishi kwa kupitia Baraza lako tukufu wakaione Hospitali ya Mloganzila, tunakwenda kwenye hizi *trip* za michezo za kirafiki na kadhalika. Lakini katika *trip* hizo moja wapo ikiunganishwa maana Mloganzila iko njiani kwenda Arusha, njiani kwenda Morogoro, njiani kwenda Dodoma. Tukiweza kusimama tukaweza kwenda kuangalia ni *State of the Art.* Sasa ndoto ya Dk. Ali Mohammed Shein ambayo ameitamka katika ilani na kuchukua ahadi kwa wananchi ni kujenga hospitali ya kisasa Binguni. Hospitali hiyo itafanana ama itakuwa nzuri zaidi kuliko hospitali ya wenzetu, tutashindana, kushindana kwa vitu vizuri sio vibaya ni vizuri. Ndio maana tumekwenda kwa *Ardhi Institute,* kwa sababu wale wameshafanya mambo yote na pale tunataka kuweka pia taasisi ya utafiti. *Medical Tourism Centerl* ya Zanzibar itakuwepo pale, kwa sababu ni pahala *green* na penye upepo mzuri. Sasa hivi watu wameshaanza kutoka Dubai na Kenya. Hapa hapa Mnazi mnapopasema Mnazi Mnazi, watu wanatoka nje ya Zanzibar kuja kutibiwa hapo hapo Mnazi. Patakapofunguliwa hapo Binguni watakuja watu kutoka Duniani wakati huo kuja kupata *Medical Tourism,* kuja kutibiwa wakati huo wanatalii. Kwa sababu mazingira yetu mazuri na hali ya hewa yetu nzuri na tuna kila kitu Mwenyezi Mungu katujaalia *Alhamdulillahi*.

Mhe. Naibu Spika, kuna baadhi ya wajumbe pia walichangia kuhusu upatikanaji wa dawa kwa wakati. Safari hii tumeunda utaratibu mzuri kama huu tunaokwenda nao, miezi sita iliyopita hii tumekwenda na utaratibu mzuri. Tunapata *Lump-sum* ya dawa kwa sababu wale Kampuni wanazotu-*supply* sisi dawa ni vyema kununua *Lump-sum,* zamani tulikuwa tunanunua kidogo kidogo ndio maana tunaishiwa, safari hii tunanunua *Lump-sum* pamoja na *buffer stock.* Kwa hivyo, kwa zile dawa mia muhimu *essential drug list* sidhani kama tutakuwa na tatizo, na pakitokezea tatizo la hapa na pale naamini hilo tutaweza kulitatua kwa mashirikiano yetu na umoja wetu.

Jengine kubwa zaidi lililoguswa Mhe. Naibu Spika, ni Bima ya Afya. Mimi naomba nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, naamini akimaliza tu bajeti yeye na Katibu Mkuu tutakaa pamoja tuanze mara moja, kwa sababu hizi fedha tayari zimeshatengwa katika bajeti yetu. Fedha za kuanzisha Mfuko wa Bima ya Afya tayari zimeshatengwa. Tayari tumeshazungumza na wataalamu mbali mbali, tayari tumeshazungumza na *stakeholders,* tayari tumeshafanyiwa *consultancy*, tayari *draft* ya awali ya sheria ipo. Tunatakiwa tukae mimi, Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, Makatibu Wakuu wetu, ili tupate ile *approval* ya mwisho ya serikali kwa ajili ya kuwasilisha hapa Mwenyezi Mungu akitujaalia sio mbali sana tutawasilisha sheria hii ya kuanzisha Mfuko wa Bima ya Afya. Mfuko wa Bima ya Afya utaanza na *Civil service*, wafanyakazi wa serikali kwanza.

Mhe. Naibu Spika, lakini huko *future* tunakokwenda Mfuko wa Bima ya Afya ndio utakuwa mkombozi wa Mzanzibari. Mfuko huu utakuwa wa aina yake kwa sababu tutasoma makosa ya

wenzetu wote wengine waliokuwa wamefanya katika mifuko yao mingine mbali mbali duniani. Tumeshasoma kutoka Mfuko wa Lebanon, tumesoma kutoka Mfuko wa Qatar, tumekwenda kusoma katika Mfuko wa *UAE* na tumesoma Mfuko wa wenzetu Tanzania Bara, Uganda na Kenya katika *East Africa Community*. Sasa wote tumeshaona matatizo yao naamini sheria ileitakapokuja Waheshimiwa Wawakilishi watapata fursa ya kutosha ya kuchangia, lakini naamini utakuwa ni mfuko wa aina yake.

Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Wajumbe wengi wamezungumzia kuhusu ile mashine ya *DNA*, na safari hii imo katika bajeti, lakini naomba nitowe indhari, maana baada ya kutoa matamko hapa kwenye *budget speech* kumekuwa na *drip* nyingi Mhe. Naibu Spika, zinazopigwa huko nje naomba nitoe indhar katika mashine ya *DNA* wajue kwamba mashind hii ya *DNA* inaletwa kwa kesi maalum za udhalilishaji haitokuwepo kwa mambo ya ndoa na kwenda kutazama watoto hayatakuwepo.

Mashine hii itakuwa chini ya sheria ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa hivyo itafuata kanuni zile zile zilizokuwemo katika sheria ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Mhe. Naibu Spika, si wewe wala mwengine atakayeweza kutoka tu na mtoto akapimwe pale haitowezekana, Sheria ya Mkemia Mkuu wa Serikali hivi sasa inasema mamlaka zitakazoruhusiwa kutoa amri mashine yoyote iliyopo pale kutumika pamoja na hizi zilizokuwepo leo wale wanapima vitu vingi sana, wanapima unga wa *Heroin* wanapima unga wa *Cocaine* wanapima unga wa kila aina pale wanapima damu ya binaadamu iliyokuwa na hivyo viashiria vya vilevi, wanapima mkojo wa binaadamu ama haja ndogo iliyokuwa na viashiria vyote. Lakini hawezi tu mtu akatoa haja yake ndogo akenda nayo pale akasema naomba unipimie Mkemia mkuu aaa masuala ya matibabu yanaishia huku huku Mnazimmoja kwenye *Laboratory* ya Mnazi Mmoja pale unakwenda uchunguzi maalum.

Kwa sheria iliyokuwepo hivi sasa na kanuni zilizopangwa atakayeruhusiwa wa kwanza kabisa ni uchunguzi unaotokana na amri ya *DPP Director of Public Prosecution* ndio maana mjumbe wa bodi pale sijui wengi kama wanajua hilo, yeye ni Mjumbe wa bodi pale bodi ya Mkemia Mkuu wa Serikali *DPP* ni mjumbe wa bodi. Kwa hivyo wa kwanza kabisa atakayeruhusiwa ni *DPP* wa pili uchunguzi unatokana na amri ya kimaandishi wa Polisi, kwa hivyo ukitaka kujua huyu mtoto wako au si wako inabidi uende huko kwanza kwa sababu ile mashine imekusudiwa zaidi katika udhalilishaji ndio tunaelekea huko. Ni amri ya polisi ya tatu itatokana na amri ya Mahakama kama kuna uchunguzi *Expert Opinion* kwa ile sheria tuliyopitisha juzi hapa sheria ya ushahidi kama kutahitajika *Expert Opinion* wa tatu atakuwa ni amri ya Mahakama, Mahakama inaamuru Mkemia Mkuu afanye uchunguzi zaidi wa kupata *Expert Opinion.*

Na wa mwisho kabisa ni uchunguzi utakaotokana na ukaguzi wowote wa kiserikali ambao umethibitika au umethibitishwa na *authority* yoyote nyengine lakini iwe imethibitishwa na Serikali kwamba *authority* hii inafanya uchunguzi huu iruhusiwe, kwa hivyo naomba niseme tena. Mashine hii inakuja mashine hii tuko katika mkakati tumeshapata *quotation*, tushapata mambo yote yameshapita tuko katika mkataba wa kuinunua. Lakini naomba niseme tena itatumika kwa mujibu wa sheria haitovunja nyumba za watu, haitovunja ndoa za watu na sisi hatutoruhusu mambo haya kufanyika nchini kwa sababu mashine hii hailetwi kwa makusudio ya kuangalia huyu ndie au sie au huyu wa nani au yule wa nani aaa. Mashine hii imekusudiwa

katika kutoa ushahidi wa *Expert Opinion* katika kesi za udhalilishaji wa watoto ambapo mtu akishapatikana hapo moja kwa moja hamna kurudi nyuma.

Mwisho kabisa Mhe. Naibu Spika, naomba kwa kumalizia kusema kwamba hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Fedha pamoja na michangio mbali mbali pamoja na kamati waliotoa hotuba yao na maoni yao yote kwa kweli iliyobakia sasa hivi ni sisi wenyewe kushirikiana, sisi tusiposhirikiana tukawa na umoja, tukawa na upendo wa kuitumikia nchi yetu hakuna mwengine atakayekuja kutumikia nchi yetu, ni sisi wenyewe lazima tushirikiane. Mimi nitawaomba sana Waheshimiwa Wawakilishi hasa katika sekta yangu inayonigusa mimi sekta ya Afya. Sekta hii ni moja wapo ya sekta nzito kwa sababu inatoa huduma kwa jamii moja kwa moja, sekta ya afya ni moja wapo ya sekta nzito leo unajua pale kuna kipindupindu, kipindupindu inatokana na hali ile kuna baadhi ya hali inabidi ufunge macho mwezi wa ramadhani uende kwa sababu unahofia itakapokuja kuzuka sikukuu kipindupindu kile kinaweza kuongezeka mara kumi na mbili zaidi.

Hali yetu tulivyo leo tuna wagonjwa 15 naomba nitamke wazi tuna wagonjwa 15 katika kambi ya kipindupindu ambao wana kipindupindu, wataalam wa maradhi haya wanatwambia kila mgonjwa mmoja aliyefika pale basi kaacha wengine ambao kashawaambukiza kwa aina moja au nyengine zaidi ya kumi, kwa hivyo nchini sasa hivi naweza kutamka wazi tunaweza kuwa na kesi 200 haraka haraka. Tokea kipindu pindu kianze mpaka hii leo tuko wagonjwa wote jumla 500 katika watu mia tano hao watoto wadogo 50 chini ya umri wa miaka 5.

Kwa hivyo mimi nakuombeni sana Waheshimiwa Wawakilishi tumuunge mkono Mhe. Waziri wa Fedha yeye ndio mkusanyaji wa yote, yeye ndio mbeba mzigo mzito, na tumpeni fursa wakati mwengine wa kubuni mambo mapya kwa sababu tunapombana sana anakuwa hana fursa ya kubuni masuala mapya, kwa sababu yeye inabidi abuni pia ndio huko mipango na kwengineko abuni fursa za kuongeza pato la taifa lazima, abuni mianya mbali mbali ya kuongezea. Kwa sababu sisi watumiaji wakubwa tuko huku hasa katika sekta ya afya, leo kipindu pindu kimezuka ghafla kesho keshokutwa tunatumia bilioni moja au bilioni mbili nje ya bajeti hatujapangilia katika bajeti yake kama mwaka huu tutakuwa na kipindu pindu kiasi fulani, lakini anahangaika kinapotokezea anahangaika pamoja na idara kuu ya maafa, maafa yoyote yanapotokezea nchini anahangaika yeye Waziri wa Fedha kutafuta zile fedha kuzileta ili tuzitumikie yameshatokea mengi.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana najua umeshawasha *Indicator* nakushukuru sana mimi naomba nimuunge mkono Mhe. Waziri wa Fedha kwa asilimia mia moja na tutaendelea kumuunga mkono katika utendaji wetu kwa mwaka huu mzima kutoa huduma bora, kufikia ndoto na ahadi alizotoa Mhe. Rais Dkt. Ali Mohammed Shein kwa wananchi wa Zanzibar ahsante sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana nakushukuru Mhe. Mahamoud Waziri wa Afya anayefuata atakuwa ni Mhe. Moudline Cyrus Castico ambae ameniomba dakika tano pamoja na Mhe. Riziki Pemba wote hao wameomba dakika tano tano na baada ya hapo ajitayarishe Mhe. Rashid Ali Mhe. Moudline karibu.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mheshimiwa kwa heshima na taadhima napenda nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza

kunipa nafasi hii na pia nipende tu kusema kwamba napenda nipongeze Baraza zima kwa ushirikiano wa pamoja ambao tumefanya kufikia mahali hapa, ambapo tupo katika suala hili zito la Wizara ya Fedha na hotuba ya bajeti kwa ajili ya Serikali. Pia nimshukuru tena sana Mhe. Spika, kwa kazi zake nzuri pamoja na watendaji wote na Wewe Naibu Spika, na wenyeviti wote katika kipindi chote ambacho tumekuwa nacho na ambacho tunaendelea kuwa nacho.

Mheshimiwa mimi nataka nijibu baadhi tu ya masuali ambayo yalikuwa yamejitokeza ambayo kidogo yanagusa Wizara yangu ili kumsadia kumpunguzia majibu Mhe. Waziri wetu wa Fedha. Ilikuwa kumeulizwa suala la ajira kuna swali linalosema inawezekana katika mawakala tulionao kuna mawakala feki wanaowasaidia watoto wanapokwenda kutafuta kazi au wanapokwenda kufanya shughuli mbali mbali nje ya nchi.

Napenda nimjibu tu kwamba Mheshimiwa ambae jina lake limenitoka lakini naomba anivumilie tu niseme kwamba kuna baadhi ya mawakala watu waliokuwa wanafanya udanganyifu katika kupeleka watu wanaotafuta ajira nje ya nchi kwa utaratibu usio salama na uangalizi wa karibu, na upungufu wa mikataba ya wazi. Lakini kwa sasa hivi kuna mawakala 8 ambao wameshapewa leseni na kusafirisha watu na wanaendelea kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizowekwa na wegine wameshindwa kutekeleza taratibu hizo. Utaratibu uliowekwa hasa kwa kada za majumbani lazima tupate mkataba wa muajiri hasa wanapopelekwa nchi za Kiarabu kama Oman na sehemu nyengine kunakuwa na udhibiti mkubwa kwa watu waliokuwa hawana leseni na iwapo watakiuka taratibu za kisheria zilizowekwa atachukuliwa hatua zinazostahiki mara moja, kwa sababu tumeshoshwa na hii tabia ya kuona watu wetu wanakwenda lakini wanarudishwa katika mazingira magumu ambayo hayatupi sisi amani.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu masuala ya wanawake na watoto Mhe. Khadija Kibano niseme tumeupokea ushauri wake unaohusu mawasiliano ya ofisi kuhusu Wilaya ambae anatakiwa atoke Wilayani na kuja Makao Makuu kwetu. Nataka niseme huo ndio utaratibu tunaoutumia lakini ni bahati mbaya tu kwamba mengine yanapoletwa inawezekana hayaletwi kwa jinsi inavyostahiki, lakini tunajipanga ipasavyo kuhakikisha kwamba masuala haya hayataendelea.

Lakini alieleza suala jengine pia kuhusiana na suala la taarifa ya mawio anasema kwamba tunapata taarifa nyingi kwenye mawio ambazo ukiangalia taarifa na data tunazotoa zinakuwa ni ndogo. Kwanza nichukue nafasi ya kuwapongeza kwa ushirikiano wao uliopo na vyombo vya habari lakini taarifa hizo zisipowasilishwa rasmi katika sekta husika kwa mfano kama polisi, hospitali na ofisi za mkono kwa mkono inakuwa sio halali kuzitumia katika taarifa hizo. Hata hivyo inaendelea kuomba wananchi kushirikiana nasi ili kadhia hii zikomeshwe katika jamii ili kina anayekuwa na tatizo asikae nalo apeleke na atoe taarifa zikishatolewa taarifa kwa kushirikiana na ngazi za chini kwa kupitia sekta zote kwa waratibu walioko sehemu zao na hata Mashehia tunazipata na tunazi-*record*.

Mhe. Asha Abdalla Mwakilishi wa Kiwengwa bahati nzuri sana kuwa ni Mjumbe ambae ni makini na bahati nzuri ni mzoefu na ni matunda ya ofisi ya Wizara yetu ya wanawake na watoto, ambae amekuwa akitoa mchango mwingi mara kwa mara nimependa kusema tu kwamba kwa uzoefu wake kuanzia ngazi za chini tunapokea ushauri wake na namuomba sana kwamba ofisi yetu iko wazi asingoje tu kuja kuzungumza hapa, aje atusaidie kwa sababu ameshawahi

kufanya kazi katika maeneo kwa muda mrefu kwa hivyo tunahitaji pia uzoefu wake na wengine tukiwa ni wageni inakuwa ni ngumu kidogo kupata uzoefu uliopo.

Lakini pia kuna Mhe. Shaib Said Ali tumepokea ushauri wako unaosema kwamba tuwe karibu sana na watu wa vijijini ili kupunguza kesi zinazojitokeza mara kwa mara ambazo ndio hizo ambazo haziripotiwi.

Suala jengine alizungumzia masuala ya ushirika anasema wajasiriamali wanawezeshwaje katika shughuli za mikopo masoko na kuwafuatilia shughuli zao ziko je, Mhe. Naibu Spika, naomba kujibu kwa kusema kwamba suala hili Wizara yangu kupitia Idara ya Uwekezaji, Uwezeshaji Ushirika na Mikopo zinawasaidia wajasiriamali katika maeneo matatu. La kwanza ni kuwahamasisha na kuwasaidisa kuunda vikundi vyao na kuvirasimisha kuwa vya ushirika. Ya pili ni baada ya kuvirasimisha vikundi hivyo vinapatiwa elimu ya uendeshaji wa vikundi vyao viongozi na mambo ya utawala bora pia wanafundishwa jinsi ya kuandaa maandiko ya miradi na waandishi wa vitabu vya hisabu pamoja na kuwaunganisha na taasisi za fedha zikiwemo mfuko wa uwezeshaji wa *Sacco's*, kwa kupitia mikopo. Pia kupitia vikundi vyao vya ushirika wanafuatiliwa wanafanyiwa ukaguzi wa kawaida juu ya uendeshaji wa biashara pamoja na kuwapatia ushauri wa kitaalam, pia kufuatana na Wizara ya Biashara wanakuwa karibu kutaka kutafutia masoko lakini pia watu wa kilimo wanakuwa karibu pia kutaka kutusaidia katika kuelimisha walioko katika sekta za kilimo.

Katika kuwawezesha wanapewa huduma zifuatazo, ujuzi wa kutengeneza bidhaa hizo bora huduma hizo zinapatikana kupitia vituo vyetu kwa mfano kama ameshasema Mhe. Waziri wa Biashara hapa Mhe. Amina Salum Ali alizungumza habari ya kusema kwamba tuna *Incubator* ambazo tunafundisha na tunaandaa wafanyabiashara ili waweze kufahamu watafanya nini, lakini pia tuna suala la *Daye Fruit Collage* ambacho ni kituo kizuri cha kuwafundisha akina mama katika suala zima la kutengeneza umeme wa jua, na wamesambaza katika maeneo mbali mbali katika sehemu hii ambayo iko Kibokwa. Kuwaunganisha na bodi ya utalii ambayo Waziri wa Habari anatusaidia pia, mikopo kupitia mfuko wa uwezeshaji pamoja na *Sacco's*, huduma za ushauri za kibiashara na maendeleo mengineyo yanayohitajika.

Mhe. Naibu Spika, kwenye suala la mikopo suali lilikuwa hivi, kuhusu suala la mikopo kwa wanawake kwamba haitoki kwa wakati. Napenda kujibu kama ifutavyo Mhe. Naibu Spika, suala la mkopo lina hatua kadhaa na utaratibu wake ni kuwa maombi ya mikopo hupitishwa kwa kamati maalum ya mikopo ambay hukaa kila baada ya miezi mitatu, baada ya maombi hupokelewa muombaji anapatiwa fomu ya kujaza mahitaji ya biashara yake na kiasi halisi cha mkopo unaohitajika, maombi yote kwa pamoja hupelekwa kwa kamati ya ya kuidhinisha mikopo na ikishapitishwa fedha hiyo hutolewa. Lakini pia muda unakuwa mkubwa kutokana na wingi wa wananchi waliotangulia kuomba hii yote tumefikia ili kuweza kudhibiti suala zima la kuweza kuwapa watu wasioweza na tukaishia kwamba tutakosa kabisa mapato ya kurudishwa kwa ajili ya mzunguko wa ukopaji.

Lakini pia napenda nichukue nafasi hii pekee ya kumpongeza sana Rais wetu Dkt. Ali Mohammed Shein kwa upendo wake kwa wananchi kuhusu ustawi wao, tumesikia jinsi tena alivyowawazia mema wastaafu wote kuongezwa kiwango cha pencheni zao mungu ataendelea kumlinda na kumbariki na kumpa umri mrefu yeye pamoja na familia yake na Zanzibar nzima,

nadhani jumuiya zote sasa hivi za wastaafu zimepata kufurahi na zisiache kumpongeza ili wajue kwamba na wao wanafurahi pale anapowafanyia yaliyokuwa mema. Kwani walikuwa wanakuja mara kwa mara ofisini kutaka kuona na wao wapate pencheni za kuongezwa kidogo, kwa sababu wengine wengi walipata pencheni katika viwango vidogo sana bahati nzuri Waziri wa fedha ametenga pesa maalum ambazo ziko katika bajeti yake. Kwa maana hiyo tukipitisha bajeti hizi mambo mengi mazuri kama walivyotangulia viongozi wenzangu mawaziri na nyie Waheshimiwa Wawakilishi mliochangia itakuwa ni wakati mzuri kuweza kuona kazi zinafanyika ipasavyo.

Lakini baada ya maelezo haya napenda kuunga mkono na kuwashauri wawakilishi wote kuunga mkono kwa asilimia mia moja ili itekeleze majukumu tuliyompangia Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango na nawatakieni afya njema ili mumalize salama Ramadhani ahsanteni na Mungu awabariki. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Uwezeshaji Wanawake, Vijana, Watoto Mhe. Moudline Cyrus Castico na Wazee vile vile, sasa nimpe nafasi Mhe. Riziki Pemba Juma Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia nami fursa hii kuweza kuchangia katika hotuba hii ya Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Naibu Spika, nianze kabisa kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu ambae ametujaalia uzima na afya njema kuweza kuwa hapa leo katika Baraza letu tukufu katika mwendelezo wa vikao vyetu vya Baraza la tisa, leo katika Mwezi 24 wa Ramadhani.

Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hii vile vile kumpongeza sana na kwa dhati kabisa Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein, nampongeza sana Mheshimiwa kwa juhudi zake ambazo anazifanya kwa kuendeleza Serikali yake lakini kwa kuleta maendeleo ndani ya taifa letu la Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ni miongoni mwa wizara ambazo imeongezewa bajeti yake ya Serikali kwa mwaka huu wa fedha 2017/2018 lengo ni kuimarisha utoaji wa elimu bora ndani ya mazingira ya Zanzibar, lakini hizi zote ni jitihada ambazo Mhe. Rais wetu anazichukua kwa kuona kwamba elimu inaimarika ndani ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, ningependa na mimi kuchangia katika baadhi ya maeneo ambayo Waheshimiwa Wajumbe wamegusia, suala zima la uimarishaji mazingira vituo vya amali, Mhe. Naibu Spika, tuseme kwamba tunaipongeza sana na tunaishukuru sana Wizara ya fedha kuhakikisha kwamba fedha za *SDL* za kuendeleza ujuzi fedha hizi zinaanza kupatikana katika bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018, hata Mhe. Jaku Hashim Ayoub alipochangia alipongeza juhudi hizi. Katika mikakati ya kuona kwamba mazingira ya vituo vya Amali imeimarika basi Serikali inachukua kila jitihada kuona kama vituo hivi vinakuwa katika mazingira mazuri vikiwemo na vifaa, njia moja wapo iliyotumika ni kuona kwamba pesa hizi zinapatikana katika vituo vyetu vya amali ili kuona kwamba lile lengo la Serikali la kuendeleza vituo hivi linaweza

kufikiwa na lengo ambalo litasaidia sana katika kupunguza tatizo la ajira kwa vijana wengi wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuona hilo linafanikiwa basi Serikali yetu kwa kusaidiana na wafadhili mbali mbali wanasaidia katika kutoa vifaa katika vituo vyetu vya mafunzo ya amali, kwa mfano katika kituoa cha Mkokotoni tulipokea vifaa kutoka kwa ndugu zetu wa Iran vifaa na mashine mbali mbali ambazo zinatumika katika kuona kwamba utoaji wa elimu katika vile vituo unakuwa ni mzuri, lakini vijana ambao wanakwenda pale basi wanapata elimu nzuri na elimu ambayo itaweza kuwasaidia wao kuweza kujiajiri baada ya kumaliza mafunzo yao.

Mhe. Naibu Spika, vile vile katika kuendeleza vituo hivi na kuona kwamba lengo la Serikali linafikiwa vituo vyetu tayari vimeanza kuongeza miradi ya uzalishaji kwa kupata mikopo katika vituo vyetu vitatu ambavyo mpaka sasa hivi vipo, ikiwemo kituo cha Mkokotoni, Mwanakwerekwe pamoja na Kituo cha Vitongoji kwa Pemba. Vituo vyote hivi vimepatiwa mikopo ili kuona kwamba inaongeza miradi yake ya uzalishaji mali na hii yote ni katika ile mikakati ya kuona kwamba vituo hivi vinaweza kuimarika vizuri ili viweze kutoa elimu iliyo nzuri na kusaidia suala zima la kuondosha tatizo la ajira kwa vijana wake.

Vile vile, Mhe. Naibu Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Elimu kupitia Idara ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali, inawapatia mafunzo walimu wa vituo hivi kwa kushirikiana na ndugu zetu wa Ujerumani sambamba na ndugu zetu wa India ambao tayari tumeshatiliana saini kuhusiana na masomo mapya ya kusarifu kwa mazao ya kilimo. Wataalamu wanaita *agro processing.*

Mhe. Naibu Spika, ni kwamba mafunzo hayo yatatolewa kwa walimu wetu, na tunaamini kwamba yatakapotolewa basi vijana wengi nao wataweza kufaidika na elimu hii ambayo itatolewa, lakini Mhe. Naibu Spika, vile vile katika kuimarisha vituo hivi, Serikali inatowa mikopo kwa wanafunzi ambao wanamaliza masomo yao. Mikopo hii inatolewa kwa lengo la kuona kwamba vijana wale na wao wanapata kujiendeleza kiuchumi, mpaka sasa tayari vikundi kumi vimeshapatiwa mikopo nafuu mikopo ambayo haina riba. Mikopo hii inatolewa chini ya usimamizi mzuri wa mamlaka na vijana hawa wanapatiwa elimu ya kutosha kutoka katika Idara ya vikundi vya Ushirika na wanapatiwa Elimu ya Ujasiri Amali pamoja na usimamizi wa fedha zao.

Kwa hivyo fedha ambazo zinapatikana kwa wanafunzi wale basi unazisimamia vizuri na tayari vijana wengi wameshaanza kujigomboa kutokana na ukitaka mafunzo ya amali. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika nigependa sana kuwambia Mhe. Wawakilishi kwamba Serikali inafanya kila jitihada kuona kwamba vituo vya mamlaka ya mafunzo ya Amali vinaimarika vizuri kwa kupeleka vifaa na zana nyengine mbali mbali, ila tunapenda sana tuendelee kuwaomba kwamba washajiishe vijana ndani ya majimbo yetu ili waweze kujiunga na vituo hivi. Kwa sababu vituo vina zana za kutosha na elimu inayotolewa pale ni nzuri kama ambapo mwisho unapata mikopo vijana wanapata kujiajiri. Kwa hivyo tatizo la mitaani kuwa vijana ambao hawana ajira basi vile vile, nalo litaweza kuondoka kwa hili tunaomba sana Mhe. Wawakilishi watuunge mkono.

Mhe. Naibu Spika vile vile, lilizungumziwa suala jengine la uongezwaji wa madawati uende sambamba na ongezeko la madarasa, tunashukuru kwa ombi ambalo na ushauri ambao

Waheshimiwa wameutoa na tuseme kwamba Serikali tayari inalizingatia suala hili, kama ambavyo tumeweza kujibu katika masuala mbali mbali yanayoulizwa ndani ya Baraza lako tukufu ni kwamba Serikali tayari itaanza na madarasa hayo 285 ambayo ni madarasa yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi hasa leo asubuhi Mhe. Naibu Waziri wakati anajibu vile vile alilichambua suala hili ambalo Mhe. Jaku Hashim lilikuwa ni suala lake la msingi.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, tuseme kwamba Serikali kwa kuona umuhimu wa hili imetenga fedha maalum za kuimarisha miundo mbinu bilioni mbili, fedha ambazo zitaingia katika ujenzi wa madarasa ukamilishaji wa madarasa hayo ya nguvu za wananchi vile vile, kuna bilioni mbili nyengine za Mfuko wa Elimu. Serikali kwa kuona kuna umuhimu mkubwa wakuona madarasa yanamaliza, madarasa ambayo wananchi wameyajenga, kwa kuengeza na bilioni mbili katika Mfuko wa Elimu, Mfuko ambao utakuwa endelevu kwa maana mfuko huu kila mwaka wa fedha utakuwa unaingiziwa fedha. Lakini Mfuko huu vile vile, utakuwa uko tayari kupokea fedha za wafadhili, wahisani wakiwemo na Waheshimiwa Wawakilishi kuona kwamba wanasaidia katika maendeleo ya elimu.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, fedha hizo zote zilizotengwa basi zitatumika kukamilisha madarasa ambayo wananchi wameanza kuyajenga na tunaamini kwamba, baada ya madarasa hayo kukamilika ile Kamati ya Mhe. Rais ya kukusanya madawati ya Kitaifa basi kasi hii itakwenda kwa sambamba kwa hiyo lengo litaweza kufikiwa vizuri.

Mhe. Naibu Spika vile vile, tulipata ushauri kwa Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Gando Mhe. Maryam Thani alisema kwamba tuendelee na ujenzi wa madarasa ya skuli za ghorofa, tuseme kwamba Mhe. Mwakilishi kwamba hili suala tayari Serikali imeanza kulifanyia kazi, na katika hizi skuli mpya ambazo zitajengwa skuli tisa basi zote zitakuwa ni skuli ya ghorofa, skuli ambazo zitajengwa katika maeneo ya Mkoa wa Mjini Magharibi pamoja na Skuli nne Pemba. Lakini vile vile, tayari kuna skuli ya Madungu, Kiembe Samaki, Mpendae pamoja na Faraja. Skuli hizi zote ni skuli za ghorofa na zimejengwa za ghorofa kwa kuona kwamba ili matumizi ya ardhi yatumike vizuri, na tutumie ardhi chache kwa kupata madarasa mengi basi Serikali tayari imeanza. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, napenda sana kumwambia Mheshimiwa kwamba jambo ni zuri ambalo umelisema lakini tayari Serikali yake ilikuwa imeshalianzia kazi hili suala na litaendelea kama ambavyo katika skuli zetu hizo tisa tutakazozijenga ambazo zitakuwa ni za ghorofa.

Mhe. Naibu Spika tuliambiwa vile vile suala zima la mapitio ya Sera yetu ya Wizara ya Elimu Mheshimiwa tumeshajibu sana suala hili na tungependa kuongezea kwamba tayari Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika mwaka huu wa fedha itapitia Sera yake ya 2006. Na sera hii itakapopitiwa itakusanya maoni kutoka kwa wadau mbali mbali wa kielimu wakiwemo wana siasa, wafanyabiashara, taasisi za binafsi NGO na Taasisi nyenginezo zitakusanywa maoni yao. Kwa hivyo tunaomba sana Waheshimiwa Wawakilishi basi tunakuja kufanya maoni watoe maoni ambayo yatakuwa endelevu, maoni ambayo yataimarisha na kujenga vizuri sera yetu ya Elimu ya Zanzibar kwa mustakbali wa maendeleo ya Elimu kwa watoto wetu.

Mhe. Naibu Spika suala jengine ambalo tayari limeshazungumzwa sana na limefafanuliwa sana hasa na Mhe. Naibu Waziri suala zima la ufaulu, ningependa kuengezea kitu kidogo katika suala hili ni kwamba Mhe. Naibu Spika, Skuli zetu za Zanzibar zilishika nafasi nzuri sana katika

matokeo ya Kitaifa ya mtihani wa Kidatu cha Nne kwa 2016. Kwa mfano katika Skuli ya Lumumba ilishika nafasi ya 44 kati ya Skuli 4228 za masomo ya Sayansi.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika hiyo nafasi ni kubwa sana maana yake tunasema hiyo, katika nafasi ambazo katika 50 bora za Tanzania nzima. Na ukiziangalia skuli ni 4228, Skuli ya Zanzibar itakuwa ni skuli ya 44 kwa kweli ni ufaulu ni nzuri sana, tunapenda sana kuwapongeza walimu wetu kwa kazi ambayo wanaifanya. Tunaomba sana wazidishe juhudi na Serikali yao iko pamoja nao katika kuona kwamba mazingira mazuri na maslahi ya walimu nayo yanazidi kuimarika kila ambapo Mhe. Rais anapofurahi kwa wafanyakazi wote, basi na walimu nao wanakuwa hawasahauliwi tunamshukuru sana Mhe. Rais kwa juhudi zake hizi na kuwapa moyo sana walimu wetu.

Lakini vile vile, Skuli ya Biashara ya Mombasa nayo imeshika nafasi 238, Skuli ya Chasasa Pemba 266 Kiponda ilichukua nafasi 272 na Vikokotoni imechukua nafasi 276. Mhe. Naibu Spika huu ni ufaulu ukubwa sana, kwa sababu nafasi ya 200 bado wamo kati kati 1000 hawajafika hata 500 haijafika. Tukiangalia skuli zote za Tanzania nzima, Zanzibar kushika nafasi hiyo ni jambo la kujivunia sana, na tunashukuru sana kwa hili na tunaishukuru Serikali kusimamia suala zima la elimu na kutoa yale mazingira mazuri mazuri kupitia Wizara ya Fedha.

La mwisho kabisa Mhe. Naibu Spika, tuliomba kwamba tuangalie sana Mkoa wa Mjini Magharibi kutokana na wingi wa wanafunzi ambao wako nao, ni kweli na tunakubali kwamba Mkoa wa Mjini Magharibi ina idadi kubwa sana ya wanafunzi ukilinganisha na Mikoa yote ya Zanzibar. Kati ya kuliona hili Serikali katika ujenzi wa Skuli tisa ambazo tano zinajengwa Unguja basi Skuli tano zinajengwa katika Mkoa wa Mjini Magharibi. Skuli hizi zinaenda katika maeneo ya Bububu, Muembe Shauri, Fuoni, Kinuni pamoja na Chumbuni zote ni katika Mkoa wa Mjini Magharibi.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuliona hili kwamba idadi kubwa ya wanafunzi iko katika Mkoa huu ndio maana skuli 5 hizi zimewekwa katika Mkoa huu. Lakini vile vile kuna Skuli mbili za kupitia *World Bank* nao watazijenga, moja itajengwa katika eneo la Mwanakwerekwe ambalo nalo bado katika Mkoa wa Mjini Magharibi, kwa hizi ni jitihada ambazo Serikali imeziona na inathamini sana kwa kuona kwamba vijana ambao wako katika Mkoa huu nao waweze kupata elimu ilio nzuri, katika mazingira mazuri.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo na mimi niseme kwamba nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia lakini vile vile, naomba sana kuunga mkono hoja ya Bajeti hii ya Serikali kwa mwaka huu fedha wa 2017/2018 na niombe sana Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu na wao tuunge mkono hoja hii Bajeti ya Serikali iweze kupita na Serikali iweze kutekeleza wajibu wake.

Mhe. Naibu Spika baada ya hayo ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana nakushukuru Mhe. Riziki Pembe Juma, Waziri wa Elimu sasa nimpe nafasi Mhe. Rashid Ali Juma na baadae mchangiaji wetu wa mwisho kabla ya kuja mwenyewe Mhe. Dkt. Khalid Salum atachangia Mhe. Mohamed Aboud Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Mhe. Rashid Waziri wa Habari, Utalii na Michezo karibu sana.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika na mimi sina budi kumshukuru *Allah Subhanahu Wataala* kutuwezesha kuingia katika hii kumi la mwisho na *inshaallah* atatupa uhai mrefu kwa sote na tuweze basi kumaliza Ramadhani hii, na tuweze kupeana Sikukuu iliyo njema *inshaallah*.

Mhe. Naibu Spika, vile vile sina budi kumshukuru sana sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa jitihada zake kubwa ambazo anazifanya kwa wananchi wake, kwa lengo tu la kutimiza azma yake, najua wazi hana kikubwa cha kuwalipa kwa kura nyingi walizomtia lakini bado ana moyo wa kuwatumikia na kuhakikisha kwamba wananchi wake wanapata maendeleo ya hali ya juu katika kipindi chake chote cha uongozi.

Lakini vile vile, nishukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Amani, kwa kuendelea kunipa imani na pamoja na kazi nyingi hizi zilizokuwamo Barazani lakini bado tu wananialika katika vikao vyote hususan vikao vya Kamati za Siasa za jimbo na vikao vyengine vyote muhimu ambavyo vinaweza kutuletea ushindi mwaka 2020.

Mhe. Naibu Spika, nataka nichangie hotuba hii ya Wizara ya Fedha inayohusu Mipango vile vile Hali ya Uchumi pamoja na Bajeti hii ya Serikali ya mwaka 2017/2018 kwa kuanza na suala zima la fedha zinazotengwa katika bajeti za Wizara zetu. Ni wazi kwamba bajeti hii zinajumuisha bajeti kuu na bajeti kuu ya Serikali inapopita ndio sisi sasa tunapaswa kwenda kuwajibika katika kuyatekeleza yale yote ambayo tumeyapanga katika Wizara zetu. Waheshimiwa Wajumbe wamechangia mengi kuhusiana na bajeti zetu, lakini leo wameendelea kuchangia mengi kwenye hii Hotuba ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango.

Katika yale mambo ambayo yamegusa katika Sekta yangu, kwenye Sekta ya Michezo walikugusa sana juu ya uhaba wa fedha ambazo zimetengwa katika kuendeleza suala zima la michezo. Mhe. Naibu Spika, nataka nikiri wazi kwamba fedha zilizotengwa hata zingetengwa kiasi gani, zingekuwa zinaonekana tu bado ndogo kwa sababu unaamini kwamba wengi wetu tunataka maendeleo yaje kwa wakati mmoja lakini maendeleo ni kitu kinachokuja kwa hatua baada ya hatua. Fedha zilizotengwa kwa ujenzi wa viwanja vya michezo nataka niwathibitishie Wajumbe kwamba, Wizara ya Fedha imefanya jitihata safari hii kuongeza kwa kiasi kikubwa fedha ambazo zitaleta marekebisho ya viwanja vya Amani, viwanja vya Gombani ujenzi wa viwanja vya *Mao tse Tung* vile vile, na ujenzi wa viwanja vitano vya wilaya.

Lakini bado kuna fursa ya kupata fedha ambazo zinaweza zikatumika kuvijenga viwanja vya ndani kama vile viwanja wa Malindi na viwanja vyenginevyo. Kubwa zaidi bajeti iliyotengwa hapa niishukuru sana Wizara ya Fedha, kwa sababu naamini wazi kwamba kwa fedha iliyotengwa ndani ya Wizara yetu basi ni wazi tutasimamia kuzipata hati za viwanja ambazo kwa muda mrefu hazikuweza kupatikana na viwanja vile vikaingia katika athari ya matumizi mengine baada yake matumizi yaliyokusudiwa.

Lakini kwa mashirikiano makubwa naamini kwa kushirikiana na Wizara yengine, Wizara yetu itashirikiana kuweza kuvilinda viwanja vilivyokuwemo mashule na viwanja vyengine, ambavyo vimo katika Taasisi za Serikali hivyo basi yale maoni ambayo yalikuwa yanaonekana na Wajumbe wengi kwamba ni vyema tungeziongeza fedha hizi, ni vizuri zaidi fedha hizi zimekuwa nyingi bado tunashukuru fedha zilizotengwa nataka niwajulishe kwamba kwa bajeti

hii sasa hivi tuungame basi na yale maneno ya hekma ya Mhe. Marehemu Mzee Abeid Aman Karume yaliyopita kwamba “Ni vyema tukawa na hicho kidogo tukagawana kidogo kidogo kuliko kuja kukipata kingi kabisa tukashindwa kuweza kugawana vyema”.

Naamini wazi kwamba tunaweza tukatumia, tukapewa bajeti kubwa sana, lakini kwa mwaka mmoja isitosheleze kuyafanya yote hayo, si rahisi Wizara kuweza kusimamia ikaweza kujenga viwanja vyote vitano vya wilaya kwa wakati mmoja. Viwanja vile vinajengwa kidogo kidogo sasa hivi tumeanza na viwanja vya Wilaya ya Kusini lakini naamini mwaka wa pili tutaendelea na viwanja vya vyengine, na hadi tutakapofika 2020, kama inavyosema ilani ya chama chetu basi tunaweza tukafanya mambo mageuzi mazito kabisa kwenye suala hili la michezo.

Lakini pia Mhe. Naibu Spika, ningeweza kuzungumzia hoja zilizoelezwa kuhusu Wizara yangu ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwenye Sekta ya Utamaduni, mambo mengi mazuri yamechangiwa na yamechangiwa kwa mfumo wa maoni na tunashukuru sana Wajumbe wote ambao wametoa michango hiyo, lakini michango hiyo mingi ilielekeza namna gani tunaweza kuukuza utamaduni wetu kuuendeleza utamaduni wetu na hatimaye ukaleta tija kubwa kabisa katika kustawisha utalii.

Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo ina amini wazi kwamba vivutio vingi vya Mji Mkongwe vimeanza kuonekana kwamba vinaharibika, nataka nitumie fursa hii kulieleza Baraza lako Tukufu kwamba ndani ya bajeti iliyopangwa ya Wizara ya Fedha ambayo inajumuisha Wizara zote, basi imezingatia vizuri sana juu ya suala zima la majengo yaliyokuwemo katika Mji Mkongwe ambayo nayo ni vivutio vikubwa kwa utalii. Miongoni ya mambo hayo yaliyozingatiwa ni moja katika ujenzi wa Beit el Ajaib ni jengo ambalo lilikuwa linaingiza fedha nyingi za mapato ya Serikali na kwa muda mrefu kivutio kile hivi sana hakitumiki, lakini ndani ya bajeti ya mwaka huu 2017/2018 bajeti ile imeweza kuzingatia vizuri matengenezo yale na Waheshimiwa Wajumbe wasiwe na wasiwasi, tumehamisha vitu vilivyokuwemo mle na wenzetu Serikali ya Oman wako tayari kutusaidia kulirejesha jengo lile kama vile livyokuwepo awali.

Nataka nithibitishe wazi kwamba jengo lile Serikali imeweza kujipangia ndani ya kipindi hichi cha 2017/2018 endapo msaada huo hautosimama kwa sababu ni msaada ambao ulikuwa unazungumziwa kwa siku nyingi, lakini jengo hilo sasa hivi endapo litakuwa litasimama Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha kwa kupitia bajeti hii ambayo tunaipitisha hii leo, basi tutalijenga lile jengo kwa fedha zetu wenyewe za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, basi ya ujenzi wa Beit el Ajaib bado kunaonekana kwamba vivutio vya ujenzi wa jengo la Ngome Kongwe nalo linaonekana kwamba limeoneka kuwa liko katika hali ya ambayo hairidhishi, jengo la Ngome Kongwe nakubali kwamba ni jengo ambalo linatumika katika Matamasha mengi hapa. Matamasha yote ya Kitaifa ambayo tunayafanya hapa Zanzibar, mengi yao basi yanafanyika pale katika uwanja wa Ngome Kongwe miongoni mwa Matamasha tunayofanya pale ni ZIFF, Sauti ya Busara hii tunafanya Matamasha ya Biashara, tunafanya Matamasha ya Kilimo, lengo letu ni kuona kwamba katika Bajeti hii ya mwaka 2017/2018 tunalitumia vyema jengo lile na Ngome Kongwe ili liweze kuwa-*acommodate* matamasha mengi zaidi ndani ya Mji Mkongwe.

Tunaelewa wazi kwamba unapotoka huko nje kuutangaza utalii kwenye matamasha basi wanaelewa neno *Stone Town* "Mji Mkongwe Mji Mkongwe" lakini unapofika Mji Mkongwe kivutio kizuri kwenye Matamasha basi ni jengo lile la Mji Mkongwe. Lile ni jengo la historia ni jengo la mwanzo ambalo limejengwa na Wareno na likaonesha kwamba ni jengo refu lao ndani ya Zanzibar, wakati huo lilipoanza kujengwa kwa hivyo ni wazi kwamba ndani ya bajeti ya mwaka huu tunashukuru sana Wizara ya Fedha kwa kutuzidishia Bajeti kidogo kwenye hili suala zima la Utamaduni na kwa mwaka huu basi tunaweza tukaimarisha vyema lile jengo letu lililokuwepo pale.

Kuhusu Utamaduni wa ukarimu wa Wazanzibari na kuimarisha lugha yetu na lugha zile za kigeni kumetoka michango mingi sana, moja katika michango hiyo ni kutizama namna gani vizazi, vivazi vyetu vinaweza vikatumia vizazi vyetu vinaweza kuvaa vivazi vile vya asili, utamaduni wa vivazi na utamaduni wa mitindo ya Ulaya ambayo inaingia nakuathiri utamaduni wetu. Ni wazi kwamba bajeti hii iliyokuwepo katika kipindi hichi cha mwaka 2017/18 ambayo siku chache zijazo itaanza kutumika basi imezingatia namna gani ya kutunza na kuulinda utamaduni wetu. Ni kweli kwamba Zanzibar imeanza kuathirika na utamaduni wa Kiulaya, utamaduni wa Kimagharibi, lakini bado kupitia matamasha yetu basi tunaweza tukaendeleza hii mitindo.

Kulikuwa kuna wazo na ushauri wa kutaka mitaala maalum itumike ya masomo kwa lugha za zigeni. Pamoja na jitihada za serikali za muda mrefu uliopita kwa kushirikiana na Wizara zetu za Elimu basi ni wazi kwamba tutafanya masuala haya ya mazungumzo katika kipindi hiki tuhakikishe kwamba lugha hizi za kigeni hususan zile nchi ambazo tunapata wageni wengi basi lugha zile za kigeni zifundishwe ndani ya mashule yetu.

Hapo zamani tulikuwa tunayo Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni imeonekana sasa hivi yote ile imeingia katika Chuo Kikuu. Lakini bado tunayo fursa hiyo kule katika Chuo cha Utalii. Chuo cha utalii nacho kimeingia katika Chuo Kikuu cha SUZA lakini bado kuna fursa zinazoweza kupatikana Chuo cha Uandishi wa Habari. Ndani ya Chuo cha Uandishi wa Habari sasa hivi tumekuwa tunafundisha lugha za kigeni ikiwemo lugha ya kichina.

Ulitoka mchango juzi hapa kwamba tunapata wageni wengi kutoka China lakini hatujui ile lugha. Nataka kuwathibitishia wananchi wa Zanzibar na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba Wazanzibar wengi wanazungumza Kichina tena wanazungumza *frequently* kabisa. Kutokana na jitihada hizo sasa utalii umeweka sasa hivi zaidi kuweza kuutangaza kwenye nchi za Asia pamoja na kufungua milango katika nchi za Bara Hindi basi tumeanza kufungua milango ndani ya Nchi ya Asia hususan kule China. Ndani ya nchi ya China kwa kujali sana utamaduni na wenzetu jinsi walivyofanikiwa kuukuza utalii kwa kutumia utamaduni wao tumeona sasa tushirikiane katika nyanja ya habari, tushirikiane na nyanja ya utalii.

Mhe. Naibu Spika, havi karibuni katika bajeti iliyopita 2016/17 tumetembelewa na waandishi wa habari, kutoka China wapatao 100 kuja kuchukua vivutio vyetu, kuja kuchukua utamaduni wetu hapa na kuutangaza ndani ya televisheni za China. Zaidi ya watalii wasiopungua milioni 5 wenye kutizama televisheni za Anhui zilizokuwepo China waandishi wale wamekuja kuchukua vitu vyetu vya utalii na tunatarajia ndani ya bajeti ijayo vivutio vile vya utalii vitaonyeshwa katika Bara la China. Tegemeo letu zile hoja zilizotoka hapa kwamba wageni wanaoingia ni laki 360

bado wanaonekana kidogo sana. Soko hili la China litakapofumuka basi tunaamini wazi kwamba idadi iliyokisiwa ya wageni laki 500 ndani ya mwaka wa 2020 inaweza kufikiwa kabla ya wakati huo.

Mhe. Naibu Spika, niendelee kupongeza jitihada na ahadi za serikali kupitia mipango yake na dhamira za kukuza uchumi kwa kuwatumikia wananchi wetu katika hotuba zake alizozitoa Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango. Ni kweli katika bajeti kuu yake ya serikali imezingatia sana muelekeo huu wa utalii. Ukiitizama bajeti yake kwa kirefu sana kurasa nyingi sehemu ya 22, 25, 43, 68 ilijaa muelekeo mzima wa kukuza utalii kwa kupitia utamaduni. Ni vyema kuwashauri Wajumbe wenzangu tuweze kuvisoma vizuri sana vitabu hivi tulivyopewa, hususan kile kitabu kinachoonesha mapendekezo ya bajeti ya serikali basi kimeelezea vizuri sana juu ya uti huu wa mgongo wa utalii.

Katika kukuza hicho basi niwambie wananchi wote kwa ujumla, niwashauri wananchi wetu wa Zanzibar wengi sana utalii wanauwona tu kwamba utalii ni utalii ambao umeanzishwa na serikali lakini wananchi hawaufanyii kazi ipasavyo. Wananchi ambapo watapata muamko mzuri na tutumie fursa hii ya kuwaamsha wananchi wetu kuwa na muamko mwema juu ya utalii, basi suala hili la Zanzibar kuwa utalii ni uti wa mgongo linaweza likafikiwa na halina mjadala juu ya suala hili.

Lakini wananchi wetu na wao napaswa kabisa kwamba kuwa makini na kupata ari ya kujua kwamba utalii unaweza ukawapatia ajira za aina nyingi, utalii unaweza ukawapatia pato wao wenyewe kwa wenyewe na utalii ndiyo unaweza sasa hivi kushika sekta kubwa ya mapato katika vyanzo vingi ambavyo vinafanyika kwa sekta mbali mbali zinazogusa huo utalii. Ni vyema tena tukakumbuka sana maneno ya hekima yaliyotolewa na Mzee wetu Marehemu bwana Abeid Amani Karume, alipenda sana tukiwa na chetu tukitukuze. Utalii ni wetu, utamaduni ni wetu. Sisi tuna jukumu la kuwasaidia wananchi wetu kuhakikisha tunaulinda utamaduni wetu, kwa hivyo tutukuze kilicho chetu mpaka tusahau kile cha wenzetu. Kwa wenzetu kuna utalii, kwa wenzetu kuna mengi, lakini utalii wetu ni wa aina yake endapo tutausimamia vizuri sana basi ni wazi kwamba utalii wetu utakuwa na haiba kubwa na utakuwa na tija kubwa na mafanikio makubwa katika uchumi huu wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, niendelee kabla ya mwisho kabisa nitoe ule mchango ambao Wajumbe wengi walichangia kuhusu Sekta ya Habari. Sekta ya Habari kama inavyoonekana niendelee kuzidi kumpongeza tena Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein katika kuleta mageuzi makubwa ya vyombo vya habari. Wajumbe wengi walikuwa hawana kimeme katika kulisema hili kwamba televisheni zetu, redio zetu za Zanzibar zimeanzishwa mwanzo lakini zimekuwa za mwisho katika kuonekana katika kupeleka habari kwa wananchi wake.

Nataka niwathibitishie wazi kwamba mageuzi makubwa yamepita katika bajeti iliyopita ya mwaka 2016/17, lakini na mageuzi makubwa yatafanywa ndani ya bajeti hii ya mwaka 2017/18. Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein, yeye mwenyewe yupo mstari wa mbele naamini wazi kwamba na Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo na mimi niko mstari wa mbele, lakini nampongeza sana Dkt. Khalid Salum Mohammed na yeye kabisa kuweza kusimamia bajeti yake na kuisaidia Wizara ya Habari kuhakikisha kwamba redio zetu na televisheni zetu za serikali zinasimama. Nataka kuwathibitishia baada ya kumaliza bajeti ya mwaka 2017/18 hakutakuwa na

redio ya *private* wala hakutokuwa na televishen ya *private* ambayo itakuwa mshindani zaidi ya kuleta ushindani wa vyombo hivi vyetu vya serikali.

Mhe. Naibu Spika, na mimi nataka nichukue fursa hii kuwaambia wajumbe wote waliokuwemo humu ndani ya Baraza la Wawakilishi, tunawakaribisha kuja kuzitizama *studio* zetu mpya, kuja kutizama matengenezo. Unaweza ukapita pale nje kwa mfano *studio* za *radio* ukaliona jengo nje halivutii halina rangi lakini ukweli tubakie na maneno ya kasa, nje hachezi ndani kuko vyengine. Studio zetu zipo za aina nyengine karibuni Waheshimiwa mje pale ku-*record* yale mambo yenu ambayo mnayafanya mazuri kwenye redio.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa una dakika tatu kumalizia, naomba umalizie.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo: Namalizia kabisa Mheshimiwa mwisho kabisa nilikuwa nataka nielezee suala la utalii. Mwisho kabisa nataka nielezee hoja ya Mhe. Machano Othman Said, alitueleza wazi kwamba Maofisa wa Mikoani hawajui takwimu. Tunajua wazi kwamba suala la takwimu katika utalii ni changamoto kubwa. Hii ni changamoto siyo kwa sekta ya utalii tu takwimu zote ndani ya serikali zetu bado hazijapata msimamo kamili kabisa wa kupata takwimu ambazo zina uwiano mmoja. Hivyo kwa kufanya mashirikiano makubwa na taasisi nyengine tunaamini wazi tutashirikiana na taasisi ikiwemo Uhamiaji na taasisi nyengine kuhakikisha kwamba maafisa wetu wanapata takwimu kamili hususan pale wanapoingia katika Mikoa yao.

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa niunge mkono hoja kwa asilimia zote asilimia mia, bajeti hii tuipitishe kwa muda mfupi. Nashukuru sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Rashid Ali Juma Waziri wa Habari, Utalii na Michezo sasa nimwite Mhe. Mohammed Aboud Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais Mheshimiwa karibu sana.

Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Aidha namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia na kutuwezesha kuendelea kufanya shughuli zetu katika mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani na kuweza kutekeleza vyema funga zetu, nawatakia Waislamu wenzangu wote Mwenyezi Mungu atujaalie atukubalie funga zetu na atuafikishie kufikia kumaliza funga hii kwa salama na furaha *Inshaallah*.

Mhe. Naibu Spika, nami nichukue fursa hii nimpongeze Mhe. Waziri wa Fedha, Katibu Mkuu, Katibu Mtendaji, Tume ya Mipango, Naibu Katibu Mkuu, Watendaji na wafanyakazi wote wa Wizara ya Fedha kwa namna walivyoshirikiana kutuletea kwanza hotuba nzuri ya bajeti lakini kutuletea bajeti nzuri sana, bajeti yenye upeo yenye muelekeo mkubwa kwa maslahi ya nchi yetu na watu wake. Nawashukuruni sana Mhe. Waziri na Watendaji wote na wafanyakazi wa Wizara ya Fedha.

Mhe. Naibu Spika, aidha niwashukuru Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi wale waliochangia na wale ambao hawakupata nafasi ya kuchangia, lakini naelewa imani yao juu ya bajeti hii, kwa hivyo niwapongeze na niwashukuru sana wajumbe wote. Shukurani maalum

ziende kwa Kamati ya Bajeti kuanzia Mwenyekiti na Wajumbe wote kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa kushirikiana na Wizara yetu ya fedha na serikali kwa jumla katika kutimiza kazi hii ngumu na nzito lakini kuitimiza vizuri sana, nawashukuru na kuwapongeza sana.

Vile vile tuwapongeze wananchi wetu wa Zanzibar Unguja na Pemba kwa imani yao kubwa kwa kuiunga mkono serikali yao na kutokana kuunga mkono huko kumetuwezesha kufanya mambo yetu vizuri na kuyatekeleza vyema kama yalivyopangwa. Tuwatakie kila la kheri wananchi na mafanikio makubwa katika kuendeleza nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, vile vile niruhusu nitoe shukurani maalum kwa Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein kutokana na umakini wake, uadilifu, busara zake na hekma zake ambazo zimesaidia sana katika kuiweka nchi yetu katika hali ya amani, utulivu na umoja kutokana na busara hizo tumeweza kupita hatua kubwa na ndiyo maana wananchi wameweza kufanya shughuli zao za kawaida, wafanyabiashara kufanya shughuli zao za kibiashara na kila mmoja wetu kutekeleza wajibu wake kama alivyojipangia kutokana na kwamba nchi yetu ipo katika hali ya amani na utulivu mkubwa. Kwa hivyo nipeleke shukurani maalum kwake yeye na familia yake kwa namna ambavyo wameisaidia nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, bajeti hii ni bajeti ya mfano ni bajeti ambayo wenzangu walionitangulia wameyaeleza kwa kina mambo mbali mbali, lakini moja ambalo kubwa katika bajeti hii ni bajeti ambayo zaidi ya asilimia 45 ya bajeti hii itakwenda kwenye mipango ya maendeleo ya nchi yetu ni ya mfano sana kwa miaka mingi haijawahi kutokea kufikia kwa asilimia hii kubwa. Kwa hivyo inatoa muelekeo mzuri wa maendeleo ya nchi yetu. Wenzangu waliotangulia walieleza namna ambavyo tumepunguza utegemezi, tumeshusha sana utegemezi na matokeo yake sasa utegemezi umekwenda kwenye wastani wa asilimia 7.3 ni jambo kubwa sana na kwa sababu Mhe. Hamad Rashid alilieleza vizuri sina haja ya kulirudia.

Mhe. Naibu Spika, niseme tu kwamba bajeti hii imelenga kuzitumia vilivyo rasilimali zetu za ndani ili ziweze kutusaidia katika kuimarisha uchumi wetu na kupunguza umasikini unaotukabili. Kwa hivyo ni bajeti ambayo imemuelekeza mwananchi kusaidia wananchi wetu, kusaidia nchi yetu, kuimarika kiuchumi, kuzisaidia sekta binafsi ziweze kufanya wajibu wake, kuvutia uwekezaji na kuhakikisha kwamba sekta zote za kiuchumi zinafanya wajibu wake pamoja na sekta za kijamii. Kwa msingi huo tuipongeze sana sana bajeti hii kwa namna ilivyoelekea kutusaidia na kutuondoa hapa tulipo ili kupiga hatua kubwa sana.

Pia bajeti hii imezidi kuendeleza jitihada zetu za sekta ile ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia, imeweka utaratibu maalum ili sasa serikali ianze jitihada ya kutafuta mafuta na gesi asilia. Jambo ambalo naamini sote mafanikio yake yataleta pato kubwa kwa nchi yetu na kuongeza uwezo wa kutoa huduma mbali mbali. Kwa ufupi niseme bajeti hii ni bajeti ya wananchi wa Zanzibar, ni bajeti yao inayoelekeza kuondoa mambo mbali mbali ambayo yanawakabili.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo kabla ya kueleza mengi ambayo nakusudia kuyasema yaliyofanywa na serikali yetu, niende moja kwa moja kwenye suala la kujibu hoja ambazo zimejitokeza kwa upande wa serikali.

Mhe. Naibu Spika, hoja ya kwanza inahusu namna tunavyofanya kazi kati yetu na chombo hiki kikubwa cha Baraza la Wawakilishi. Nataka niwahakikishie Wajumbe na wananchi kwa jumla waelewe kwamba serikali yetu ina dhamira na siku zote imekuwa ikifanya hivyo kufanya kazi kwa karibu sana na Baraza lako hili tukufu. Tunaamini kwamba Serikali na Baraza tukufu la Wawakilishi ni watoto pacha ambao wanahitaji kufanya kazi kwa pamoja. Lakini pia tunaheshimu Kamati zote za kudumu za Baraza hili mipango yake na taratibu zake ili tuweze kufanya kazi kwa pamoja. Tunaelewa umuhimu wa Kamati hii ya Bajeti ambayo imeanzishwa.

Mhe. Naibu Spika, lazima tukubali katika chombo hichi cha Kidemokrasia maoni ya kila mmoja wetu ni halali. Maoni ya Wajumbe wasiokuwemo ndani ya serikali na wajume waliyokuwemo ndani ya serikali maoni yao yote ni sawa cha msingi ni kupima nguvu na uwezo wa hoja yenyewe. Nia na dhamira kwa wajumbe waliotoka serikalini na wasiotoka serikalini dhamira yetu ni kuhakikisha tunawahudumia vyema wananchi wetu. Cha msingi hapa ni hoja yenyewe na hata siku moja serikali haiweze kuwa hoja yake dhamira ni kukwamisha utendaji wa Kamati au utendaji mzuri wa Baraza, bali hoja zetu ni kusaidia utekelezaji utakaosaidia Baraza letu na Kamati zetu kufanya kazi vizuri. Mimi naomba jambo hili tuelewane kwa pamoja, dhamira hapa ni kufanya kazi kwa pamoja.

Mhe. Naibu Spika, suala la usimamizi wa matumizi ya serikali. Ni nia ya serikali kuhakikisha kwamba matumizi ya serikali yanatumika vizuri kwa kufuata taratibu na sheria zilizowekwa. Waheshimiwa Wawakilishi wamelizungumiza sana jambo hili. Nataka niwahakikishie kwamba dhamira za seirikali ni kufanya jitihada zote kuhakikisha kwamba matumizi ya fedha za umma zinatumika kwa malengo na utaratibu uliokusudiwa ili kutoa tija na ufanisi katika utekelezaji huo. Taasisi mbali mbali zimeanzishwa na nyengine kuimarishwa na serikali msingi wake ni kuhakikisha nidhamu na matumizi bora.

Mhe. Spika, kwa mfano ofisi ya *CAG*, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imeimarishwa zaidi kwa msingi wa kusimamia shughuli za matumizi ya fedha za serikali kwa ukamilifu wake. Halikadhalika kimeanzishwa chombo maalum cha kupambana na rushwa msingi wake ni kuangalia kila pale ambapo pana rushwa hatua zichukuliwe. Lakini vile vile serikali imeweka utaratibu ya kukutana kati ya serikali na Wizara husika kwa maana ya Rais kukaa na wizara zake kila baada ya miezi mitatu ili kuona namna ya matumizi ya serikali, mafanikio kutokana na kile kilichopatika na kwa msingi huu kwa kiasi kikubwa sana kimepigwa hatua kubwa katika matumizi ya Serikali, na jitihada hizo zitandelea kuendelezwa ili kuhakikisha kwamba matumizi ya Serikali yanatumika vizuri.

Vile vile kwenye suala la ujenzi wa bandari ya Mwangapwani Mhe. Naibu Spika, uamuzi wa kujenga bandari Mwangapwani umeshafanywa na Serikali na Mwangapwani serikali imeamua ijengwe bandari ya mafuta na gesi na eneo la Mpigaduri serikali imefanya uamuzi ijenge bandari ya mzigo. Tathmini yote imefanywa katika vikao mbali mbali na wataalamu mbali mbali kuhakikisha bandari ya Mpigaduri inajengwa na ijengwe kwa kuleta tija siyo kwa kuleta athari yoyote katika uchumi wetu. Kwa hivyo tunaamini uamuzi huu ni wa msingi na una manufaa makubwa katika kwa nchi yetu na ni matarajio yetu baada ya kukamilika bandari ya Mpigaduri, bandari ya malindi itumike zaidi kwa ajili ya bandari ya abiria wetu sehemu ya kushusha na kupakia abiria.

Kwa huo uamuzi umefanywa na serikali imejua umuhimu wa kufanya bandari ya Mwangapwani kwa maana ya bandari ya gesi na mafuta katika eneo la Mwangapwani. Kwa hivyo Waheshimiwa Wajumbe huu ulikuwa ni uamuzi wa Serikali na ulifanywa kwa makusudi kwa kuelewa kwamba italeta tija katika shughuli za serikali.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa wizara yangu lilikuwepo suala linalohusiana na moja kuhusu Uwakala wa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na lilikuja kama shauri kuwa Mhe. Rashid Makame Shamsi alitaka kwamba fedha tunazopewa za mtaji wa bilioni 1.5 zitumike vizuri, nataka nimuhakikishie kwamba tunasimamia ili malengo yaliokusudiwa yafatwe na zitekelezwe kama ambavyo jambo hili limekusudiwa kwa nia ya kukiboresha kiwanda chetu, kwa nia ya kutoa huduma bora zaidi na naamini nyote wajumbe mtakubaliana nami kwamba kazi nzuri imeanza ya kiwanda. Vitabu vyetu vya bajeti hivi sasa ukiviona unaona ni vitabu vilipigwa kitaaluma vya kisasa vinavyokidhi haja, tutaendelea kufanya hivyo ili tutoe huduma bora zaidi.

Aidha kulikuwa na hoja kuhusu gharama za ujenzi wa jengo la ushauri nasaha la Kidimni. Waheshimiwa Wajumbe ni kweli jengo lile sisi tumerithi kutoka iliyokuwa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na tumekwenda mara nyingi kuona uhalisia wa thamani ya jengo lenyewe. Nataka niseme kwamba jengo lenyewe katika kutolewa tenda lilifuata utaratibu wote uliotakiwa kwa mujibu wa sheria ile na aliyechaguliwa kufanya kazi ile ilikuwa ni Kampuni ya Al-Hilal na walifanya kutokana na mikataba walokatibiana nao.

Jengo lile sio jengo dogo sana ni jengo ambalo linatarajiwa kuwa la ghorofa tatu kwa hivyo *foundation* yake lazima itakuwa na gharama na vile vile katika kufunika kwake kwa zege ya juu kwa maana ya paa kwa sasa lazima itakuwa ya gharama, ina vyumba mule ndani karibu vyumba ishirini vya shughuli mbali mbali ni eneo linotumika zaidi ya *square metre* 1,200 pamoja na kuanza *foundation* ya uzio na kuweka mazingira ya eneo yale katika hali nzuri. Lakini pia kuna maeneo yaliyojengwa kwa ajili ya kuweka lifti mbili na vile vile kuwa na ngazi mbili za kupandia kwenda juu.

Kwa hivyo kwa hesabu za haraka haraka sisi tulivyoona tumejiridhisha kwamba inaweze kufikia thamani halisi. Lakini kwa sababu ya ushauri iliyotolewa na Baraza lako Tukufu Mhe. Naibu Spika, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ataunda kamati maalumu kufuatilia kwa kina zaidi kuona uhalisia wa gharama za matumizi ya jengo lile. Mhe. Naibu Spika, tutafanya kila liwezekanalo ili kuhakikisha fedha za serikali zinatumika vizuri.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine ambalo ningependa niliseme ni suala zima la mafanikio yetu chini ya uongozi wa Dk. Ali Mohamed Shein. Mhe. Naibu Spika, mcheza kwao hutunzwa kazi kubwa imefanyika ya maendeleo ya nchi yetu na moja katika mambo ambayo Mhe. Rais wetu amefanya ni kuhakikisha Amani na Utulivu wa nchi yetu kuimarika sana. Lakini pia ameendelea kuyaimarisha Mapinduzi yetu matufuku ya mwaka 1964 na sera zake za msingi, ameimarisha muungano wetu na umoja wetu katika nchi yetu, ametekeleza vyema yeye na Serikali yake Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini, na matokeo yake Mhe. Naibu Spika, ni haya Mhe. Waziri wa Fedha aliyaeleza.

Pato la Taifa limeongezeka, pato la mtu mmoja mmoja limeongezeka, mfumko wa bei umethibitiwa vizuri na sasa umebaki kwenye tarakimu moja, makusanyo ya mwezi

yameongezeka na kila mwezi sasa tunakusanya zaidi ya bilioni 50,000,000,000 kutoka bilioni 15,000,000,000 mwaka 2010. Kwa hivyo ziko jitihada kubwa ambazo zimefanyika katika kuimarisha uchumi wetu na kuongeza mapato ya nchi kwa nia ya kutoa huduma zaidi kwa wananchi wetu.

Lakini Mhe. Rais ameendelea sana kujali sana wafanyakazi katika kada mbali mbali kila wakati ameshughulikia kwa kina sana kuongeza mishahara na hivi karibuni sote tumesikia kimeongezwa kima cha chini kutoka 150,000 mpaka 300,000 ameendelea kutowa *pension* kwa wazee, ameweka utaratibu mzuri wa Utumishi wa Umma ambao sote unatufaa. Lakini ameongeza kasi katika upatikanaji wa elimu kwa kujenga madarasa mapya ya shule pamoja na vifaa vya skuli, kuondoa michango kwa wazazi katika elimu ya msingi pamoja na kugharimia mitihani katika skuli za *primary* na *secondary* na kuanzisha mfuko wa elimu nia na dhamira kuendelea kuimarisha huduma za elimu nchini. Ameendelea kuimarisha miundo mbinu Usafirishaji na Mawasiliano na Nishati na hivi leo tunaona namna ya huduma tunavyozipata kwa urahisi zaidi.

Mhe. Naibu Spika, huko nyuma ilikuwa ukitaka kusafiri kwenda Pemba inakuchukua mwezi mzima kufanya *booking* ya ndege kwenda Pemba, lakini leo hapa unachukua mkoba wako unaingia kwenye ndege unasafiri na jioni unarudi na kwenda Dar es Salaam na kadhilika na kadhalika. Kwa hivyo urahisi kwa safari zetu umetokana na kazi kubwa iliyofanywa na uongozi wa Rais wetu na utelelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapunduzi. Mafanikio yote haya Mhe. Naibu Spika yametokana na jitihada kubwa wengi hapa tumezungumizia suala la *Terminal II* nataka niwahakikishe Mhe. Naibu Spika na Baraza lako tukufu kwamba jitihada kubwa zimefanywa kuhakikisha jengo lile kupata muafaka na kuendelea kumalizika mapema iwezekanavyo, Serikali imechukua hatua mbali mbali na muda usiokuwa mrefu jengo litamalizika tutalitumia vizuri kwa manufaa yetu sote.

Mhe. Naibu Spika, Rais wetu alichukua jitihada mahsusi za kuimarisha zao la karafuu kwanza kwa kuongeza bei lakini pia kwa kuongeza uzalishaji kabla ya mwaka 2010 uzalishaji ulikuwa chini ya tani elfu 3,000 leo hii tunazaidi ya tani elfu 5,000 kwa mwaka tunazalisha kwa karafuu, na bei naamini wananchi wetu wanaridhika kutokana na bei nzuri inayotolewa na Serikali kwenye suala la karafuu.

Kwa hivyo yuako mambo mbali mbali ambayo yamefanikiwa katika huduma za afya Mhe. Waziri wa Afya amelieleza mambo haya kwa kina na mimi naamini sote tunaona jitihada ya serikali. Lakini niseme moja kubwa sana, ujenzi wa bohari ya kisasa ya madawa ambayo ni mfano katika Afrika yote haya yamefanywa katika kipindi hiki cha Dk. Ali Mohamed Shein, kwa hivyo tuna kila sababu ya kuiunga mkono bajeti hii ili izidi kuleta mafanikio makubwa zaidi.

Uanzishwaji wa miji mipya ya kisasa kama Fumba na kwengineko na hivi sasa mji wa Zanzibar unapangwa uwe mji wa kibiashara na wenye maendeleo makubwa zaidi na dhamira njema ipo na mambo yameanza nataka niwahakikishie wajumbe wa Baraza letu Tufuku na wananchi wa Zanzibar katika muda usio mrefu tutaiona Zanzibar ni kitofu cha mji wa biashara katika ukanda huu wa Afrika ya Mashariki, hizi zote ni jitihada ya serikali yetu. Kwa hiyo tunayo kila sababu wajumbe wenzangu kuiunga mkono bajeti hii.

Mimi nina ushauri Mhe. Naibu Spika ningeomba sote kwa pamoja tukubaliane nayo katika suala zima la maendeleo ya nchi yetu tuhitaji sana kuondoa tofauti zetu za kisiasa. Mhe. Naibu Spika, ukitizama tofauti zetu za kisiasa hazitusaidii sana zaidi ya kutugawa na kuturudisha nyuma tunapoungana tukawa watu wamoja tukafanya kazi pamoja mafanikio yetu yanakuwa makubwa sana, kwa hivyo niwaombe wananchi wote wa Zanzibar kwanza waiunge mkono Serikali yao washirikiane nayo ili tufanye kazi kwa pamoja kwa maslahi ya nchi yetu ili tuweze kuondoka hapa tulipo na kupiga hatua kubwa zaidi kwa maslahi yetu sote.

Mhe. Naibu Spika, dhamira ya Mapinduzi matukufu ya mwaka 1964 yalikuwa ni kuleta umoja katika nchi yetu, kuleta upendo na kupiga hatua kubwa zaidi ya kimaendeleo na kuondoa aina yoyote ya dhuluma na kuondoa aina yoyote ya ubaguzi maana ubaguzi Mhe. Naibu Spika ndio sumu ya maendeleo, ndio sumu ya amani, ndio sumu ya umoja wetu. Kwa hivyo jambo la msingi kabisa tuendelee kuimarisha umoja wetu kupambana na kila ambalo litaleta athari katika kubaguana wenyewe kwa wenyewe. Tuache kubaguana kwa rangi, tuwache kubaguana kwa dini, tunawache kubaguana kwa sababu ya itikadi za kisiasa, tuache kubaguana kwa sababu ya eneo mtu analotoka na sote tushirikiane tujenge nchi yetu na yoyote yule anayehatarisha amani ya nchi yetu huyo sote tumuone kama si mwenzetu na tumuweke kando kabisa, suala la msingi tukae kwa umoja, tukae kwa amani, tupendane, tuvumiliane tujenge nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, na Waheshimiwa Wajumbe wakati umefika kwa kuona hapa tulipo tunahitaji kufanya mabadiliko makubwa zaidi kwa maendeleo yetu, kwa hiyo naomba sana sana sote kwa pamoja ili kupata faida kubwa za bajeti hii tusimpe tabu Waziri wa Fedha atakapokuja hapa baada ya kutoa majibu yake tushirikiane naye tuiunge mkono bajeti hii ili tuanze na safari mpya ya kuleta maendeleo makubwa katika nchi yetu.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, napenda niseme naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na niwaombe wenzangu sote tuunge mkono hoja hii kwa mafanikio ya kuleta maendeleo makubwa katika nchi yetu.

Baada ya haya nakushukuru sana Naibu Spika na ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana tunakushukuru Mhe. Waziri sasa nimpishe mwenye hoja Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango Dk. Khalid. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, sina budi kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutujalia afya na uzima na kutuwezesha kutekeleza majukumu yetu tukiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu Baraza la Wawakilishi.

Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa amani na utulivu tulionao katika nchi yetu lakini pia namshukuru Mhe. Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein kwa hekima na busara zake na mapenzi yake kwa wananchi wote jambo ambalo linachangia sana kujenga mshikamano na amani na utulivu katika nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba pongezi zote zililotolewa katika hotuba yangu zinamstahiki Mhe. Rais wetu Dk. Ali Mohamed Shein, mafanikio tunayoendelea kuyapata katika nchi yetu

yanatokana na juhudi zake, hekma na busara na maelekezo anayotupatia siku hadi siku. Mimi binafsi namshukuru sana Mhe. Rais kwa muongozo na maelekezo yake kwangu na kwa wizara yangu jambo ambalo linatufanya tuweze kutekeleza majukumu yetu makubwa tuliyopewa na Serikali hii kwa ufanisi na wepesi sana.

Mhe. Naibu Spika, nachukua fursa hii pia kumshukuru sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais Balozi Seif Ali Iddi ambaye ndiye Kiongozi wetu Mkuu wa Shughuli za Serikali hapa Barazani ambaye naye amekuwa msaidizi makini wa Mhe. Rais na amekuwa akitupatia muongozo na maelekezao yake mazuri ambayo yanasaidia sana kufanikisha utekelezaji wa shughuli za wizara yetu.

Mhe. Naibu Spika, shukurani za pekee nazitoa kwa Mhe. Spika kwako wewe Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Wenyeviti kwa kuongoza mijadala ya Baraza letu kwa umakini na busara na hekima kubwa.

Mhe. Naibu Spika, aidha namshukuru sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti Mhe. Mohamed Said Mohamed Dimwa na wajumbe wote wa kamati hii kwa mashirikiano mazuri maoni na maelekezo ya kamati. Nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza wote kwa mashirikiano mazuri kwa wizara yetu na nawashukuru wote waliopata fursa ya kuchangia aidha kwa kusema moja kwa moja au wale waliotoa maoni yao kwa maandishi.

Mhe. Naibu Spika, wizara yetu imepata bahati kubwa ya kuchangiwa Waheshimiwa Wajumbe wengi jumla ya wajumbe hamsini na nne (54) wamechangia hotuba ya wizara yangu, wajumbe 47 walichangia kwa kusema moja kwa moja na wajumbe saba (7) walichangia kwa maandishi.

Waliopata fursa ya kuchangia ni kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Abdalla Ali Kombo - Mwakilishi wa Jimbo la Mwanakwerekwe ambaye alisoma hotuba ya Kamati kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti Mhe. Mohamed Said Mohamed Mwakilishi wa Jimbo la Mpendae.

2. Mhe. Shehe Hamad Mattar
3. Mhe. Ali Suleiman Ali
4. Mhe. Hassan Khamis Hafidh
5. Mhe. Abdalla Maulid Diwani
6. Mhe. Dk. Mwinyihaji Makame
7. Mhe. Miraji Khamis Mussa
8. Mhe. Panya Ali Abdalla
9. Mhe. Omar Seif Abeid
10. Mhe. Said Omar Said
11. Mhe. Saada Ramadhan Mwenda
12. Mhe. Tatu Mohammed Ussi
13. Mhe. Yussuf Hassan Iddi
14. Mhe. Ame Haji Ali
15. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil
16. Mhe. Suleiman Makame Ali

17. Mhe. Nassor Salim Ali
18. Mhe. Ali Khamis Bakar
19. Mhe. Shaib Said Ali
20. Mhe. Hidaya Ali Makame
21. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis
22. Mhe. Suleiman Sarahan Said
23. Mhe. Asha Abdalla Mussa
24. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa
25. Mhe. Viwe Khamis Abdalla
26. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma
27. Mhe. Rashid Makame Shamsi
28. Mhe. Hamad Abdalla Rashid
29. Mhe. Simai Mohammed Said
30. Mhe. Bahati Khamis Kombo
31. Mhe. Maryam Thani Juma
32. Mhe. Machano Othman Said
33. Mhe. Hamza Hassan Juma
34. Mhe. Khadija Omar Kibano
35. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
36. Mhe. Mussa Ali Mussa
37. Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira
38. Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
39. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais
40. Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko
41. Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji
42. Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)
43. Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi
44. Mhe. Waziri wa Afya
45. Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto
46. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali na
47. Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo.

Mhe. Naibu Spika, waliopata fursa ya kuchangia kwa maandishi wengine wamerudia wamechangia moja kwa moja na kwa maandishi.

1. Mhe. Asha Abdalla Mussa
2. Mhe. Bahati Khamis Kombo
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar
4. Mhe. Tatu Mohammed Ussi
5. Mhe. Masoud Abrahman Masoud
6. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf
7. Mhe. Suleiman Sarahan Said
8. Mhe. Mohamed Mgaza Jecha
9. Mhe. Omar Seif Abeid
10. Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto
11. Mhe. Mgeni Hassan Juma

12. Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo
13. Mhe. Zulfa Mmaka Omar
14. Mhe. Waziri wa Afya

Mhe. Naibu Spika, kwa ujumla michango yote yalikuwa ni mizuri na niseme tumeipokea michango yote kwa moyo mkunjufu. Nitajitahidi kutoa maelezo katika yale maeneo ambayo bado hayajatolewa ufafanuzi lakini naomba sana Mhe. Naibu Spika uniruhusu kuwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri wote na Naibu Mawaziri waliopata fursa ya kutoa ufafanuzi katika maeneo mbali mbali yanayohusu wizara yao, lakini pia yanayohusu bajeti ya serikali na mpango wa maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, pia naomba nichukue fursa hii kuwashukuru sana watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango na taasisi zake zote wakiongozwa na Katibu Mkuu, ndugu Khamis Mussa Omar, Naibu Katibu Mkuu, ndugu Ali Khamis Juma, Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango, Afisa Mdhamini, ndugu Ibrahim Saleh Juma.

Baada ya utangulizi huo Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako sasa naomba kutoa ufafanuzi na maelezo kwa baadhi ya michango ambayo nahisi bado haijaguswa na Waheshimiwa Mawaziri na Waheshimiwa Manaibu Mawaziri ambao wamesaidia kutoa ufafanuzi katika hutuba yangu.

La mwanzo ambalo nahisi nilitolee ufafanuzi mheshimiwa liliulizwa sana na Waheshimiwa Wajumbe wengi, lakini hasa liliulizwa na Kamati ya Bajeti ni suala la thamani ya shilingi na mfumko wa bei. Katika hili hasa hoja yao kubwa ilikuwa Benki Kuu waandae mipango ya hali ya uchumi pamoja na sera za kifedha wakishirikiana kwa karibu sana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika mpango na maamuzi hayo ili kuhakikisha sarafu yetu haizidi kupungua thamani. Hiyo ndio hoja iliyokuwa ya Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati, na niseme tu kwamba tumekuwa tukishirikiana sana na Benki Kuu hasa katika suala la sera za fedha ambapo uandaaji wake huzingatia mwenendo wa uchumi wa Zanzibar. Hata hivyo, Benki Kuu ina mamlaka na uhuru juu ya jukumu lake hilo la msingi. Aidha, suala la utulivu wa sarafu kimsingi linahitaji pia kuongezeka kwa udhalishaji wa ndani na usafirishaji, kwa maana ya *export* na kupunguza uagiziaji ili kupata urari mzuri wa biashara na kupunguza pengo kubwa baina ya mahitaji na upatikanaji wa fedha za kigeni.

Lakini pia kamati ilikuwa na hoja ya ushirikishwaji wa sekta binafsi ya Zanzibar katika maamuzi yanayowagusa. Hili Mhe. Naibu Spika, niseme kwa ujumla serikali inathamini sana mchango wa sekta binafsi na kwa kiasi kikubwa sana sekta binafsi inashirikishwa katika mapitio na mageuzi ya mfumo wa kodi na mashirikiano yataimarishwa katika maeneo mengine.

Hoja nyengine ilikuwa ni mfumko wa bei, kama nilivyosema na serikali ilitakiwa kuweka mikakati madhubuti kuhakikisha uzalishaji wa ndani wa chakula unaongezeka.

Mhe. Naibu Spika, suala hili lilizungumzwa vizuri sana na Mhe. Waziri anayehusika na sekta ya kilimo na hasa alipogusia mradi mkubwa ambao unatarajiwa kutekelezwa hivi karibuni kutokana na fedha za mkopo nafuu kutoka *Exim Bank* ya Korea ya Kusini. Alieleza jinsi gani kilimo cha umwagiliaji maji kitakavyoendelezwa kupitia mradi huo mkubwa.

Mhe. Naibu Spika, katika hili nipongeze sana juhudi ambazo zinafanywa na sekta binafsi, wakulima wenyewe lakini pia na *NGO's* hasa *NGO* ya TAHA ambazo zimekuwa zikisaidia sana wakulima wetu kwa kuwapatia *green houses* na pia wanasaidia katika utoaji wa pembejeo za kilimo. Naomba pia *NGO* nyengine hata sekta binafsi nao ishiriki kikamilifu katika kuendeleza sekta ya kilimo, hoja yetu ikiwa kuongeza uzalishaji na kuweza ku-*stabilize* uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo lilizungumzwa na kamati ni serikali iangalie uwezekano wa kuishauri Benki ya Maendeleo ya Kilimo iliyopo Tanzania Bara kufungua tawi lake hapa Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, wazo hili ni zuri na niseme tu kwamba tunalipokea, hata hivyo ni vizuri kuelewa kwamba benki ipo katika hatua za awali baada ya kuanzishwa na zimo katika hatua za matayarisho. Lakini hili tulichukue na tutawasiliana nao na kuwaomba kufikiria kuwa na tawi la benki hiyo kwa hapa Zanzibar.

Pia lilizungumzwa suala na kamati serikali iwezeshe wakulima wadogo wadogo kwa kuongeza fungu la uwezeshaji kwa vijana (*guarantee fund*). Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba kwa sasa *guarantee fund* ipo chini ya wizara inayoshughulikia masuala ya uwezeshaji na inahusu zaidi masuala ya kusaidia vijana. Mfuko huo pia unaonesha una changamoto za uendeshaji hasa gharama kubwa za uendeshaji. Wizara inadhamiria kutatua changamoto hizo lakini vile vile inadhamiria kukutana na uongozi wa Benki ya *CRDB* inayodhamini ili kuzungumzia changamoto hizo. Tutaangalia uwezekano wa kuhusisha mfuko huo na wakulima wadogo wadogo baada ya kuondokana na changamoto zilizopo.

Masuala ya sekta ya ardhi namshukuru sana waziri anayehusika na sekta ya ardhi aliyazungumza vizuri sina haja ya kuyarudia. Lakini pia kulikuwa na suala zima la Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini MKUZA III na kamati iliitaka wizara au serikali ichukue hatua na jitihada za makusudi katika kuwaelimisha na kuwashirikisha wananchi wakati wa kuandaa na kutekeleza mipango ya kimataifa.

Mhe. Naibu Spika, hatua zote zinazochukuliwa katika uandaaji wa mipango ya kitaifa na hasa MKUZA tokea hatua ya MKUZA I, MKUZA II na sasa MKUZA III wananchi wamekuwa wakishirikishwa kikamilifu kwa kutumia njia mbali mbali. Hata katika uzinduzi wake Mhe. Naibu Spika basi utazinduliwa na Waheshimiwa Wajumbe hapa watapata mwaliko, lakini utazinduliwa na wananchi wote watashirikishwa katika uzinduzi huo, kwa sababu tunaamini kabisa hatua za mwanzo zianzie katika uandaaji lakini pia katika utekelezaji, ufatiliaji na kuufanyia tathmini mpango huo.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo lilizungumzwa na Kamati ya Bajeti ni Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi (*ZIPA*), na hili pia lilizungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe baadhi yao waliligusia na walisema kwamba umefika wakati wa kuifanyia mapitio yakinifu sheria yetu ya *ZIPA* ambayo imepitwa na wakati. Lakini pia wanazungumzia kwamba baadhi ya wananchi wazalendo hawanufaiki sana na utaratibu uliopo sasa hivi wa uwekezaji.

Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba mapitio ya sheria ya *ZIPA* yanaendelea, tayari tuna rasimu ya sheria mpya ya *ZIPA* na mswada wa sheria mpya unatarajiwa kuwasilishwa katika mwaka wa fedha 2017/2018.

Hoja nyengine ilikuwa ni serikali kukamilisha haraka mchakato wa kuripoti au wa kupitia ripoti ya kamati kuhusu kuwa na mfumo wa *one stop center*. Mhe. Naibu Spika, nieleze tena nimeshalieleza hili katika Baraza hili tukufu lakini nirudie kwa kusema kwamba kamati maalum iliyoundwa kupitia mfumo huu wa *one stop center* na kupendekeza namna ya kuimarisha imewasilishwa ripoti yake serikalini, na serikali ilitoa maoni na maelekezo kwa kamati hiyo ambayo sasa kamati inayafanyia kazi maelekezo ya serikali. Hivi karibuni tunatarajia watarudisha ripoti hiyo serikalini na serikali itatoa maelekezo yake.

Mhe. Naibu Spika, hoja nyengine ni serikali iwasilishe katika Baraza kwenye kipindi kifupi kijacho mikakati iliyopanga kuendeleza uwekezaji wa ndani.

Mhe. Naibu Spika, kwa utaratibu uliopo sasa serikali haiwasilishi Barazani miongozo ya kazi na mikakati ya aina hii. Mikakati hii itawasilishwa kupitia Kamati ya Kudumu ya Fedha, Biashara na Kilimo wakati wa utekelezaji wa kazi zake. Tunaamini kamati nayo itawasilisha taarifa yake na kutoa maoni na ushauri wake juu ya mkakati huo. Lakini kama nilivyosema mwanzo mipango na mikakati Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanaalikwa kushiriki katika uandaaji wa mipango hiyo, lakini vile vile katika kuifanyia tathmini mipango hiyo, ila utaratibu wa kuwasilisha hapa Barazani kwa sasa haujakuwepo.

Mhe. Naibu Spika, kuna hoja nyengine ambayo ilitolewa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili na hasa ilihusiana na sekta ya afya na hasa kwenye suala zima la ununuzi wa kifaa cha *DNA*. Namshukuru sana Waziri wa Afya amelitolea ufafanuzi vizuri sana suala hilo.

Mhe. Naibu Spika, lipo suala jengine ambalo lilizungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Bajeti utekelezaji wa miradi mikubwa na hoja yao ilikuwa serikali kuwa makini wakati inapoanzisha miradi kwa kufanya upembuzi yakinifu kwa maana *feasibility study* na kuwa na uhakika, lakini pia kuwa na usimamizi mzuri na kuwachukulia hatua watakaobainika kufanya uzembe au kukamishwa ufanisi katika utekelezaji wa miradi ya serikali.

Mhe. Naibu Spika, tunakubaliana na maoni ya kamati miradi ya maendeleo inatumia fedha nyingi za wananchi, hivyo uandaaji na utekelezaji wake unahitaji umakini mkubwa kuhakikisha tija ya fedha zinazotumika inapatikana. Kupitia Tume ya Mipango kwa sasa miradi yote inalazimika kuwa na upembuzi yakinifu. Aidha, idara maalum ya ufatiliaji na tathmini imeanzishwa chini ya Tume ya Mipango. Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pia nao huifanyia ukaguzi miradi hiyo ya maendeleo, mambo haya yakitekelezwa na kusimamiwa vyema tatizo lilobainika litaondoka kabisa. Kwa hivyo, hapa tusisitize utaratibu ambao hivi sasa tunao, na utaratibu wetu ni kwamba miradi mikubwa kama nilivyosema inawashirikisha pia wananchi kupata maoni yao, lakini vile vile tuna idara maalum inayoshughulikia suala zima la ufuatiliaji, lakini pia na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali naye anakuwa anafatilia miradi hiyo kuona *value for money* kwa zile shughuli ambazo zinatekelezwa.

Mhe. Naibu Spika, hoja nyengine ya kamati ilikuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kulifanyia kazi suala la Bima ya Kiislamu na miamala mengine ili wananchi wetu wafaidike na fursa zinazopatikana huko. Mhe. Naibu Spika, serikali inatambua haja ya kupanua huduma za

fedha zikiwemo zile za bima na hasa huduma za Kiislamu ambazo zinaonekana kuwa na soko kubwa hapa nchini. Tutaendelea kufatilia kupatikana kwa kanuni za uendeshaji za kuendesha biashara hiyo kutoka *TIRA* ili na sisi tufaidike nayo.

Mhe. Naibu Spika, vile vile Kamati ya Bajeti ilikuwa na maoni kwamba ni kheri kuwa na bajeti ndogo, lakini yenye kutekelezeka na uhalisia wa upatikanaji wa fedha kuliko kuwa na bajeti kubwa ambayo inaishia kulipa mishahara na matumizi mengine ya uendeshaji wa ofisi (*O/C*).

Mhe. Naibu Spika, suala la upatikanaji wa fedha za kutekelezea bajeti linaathiriwa na mambo mengi, makisio, makadirio yanafanywa kwa kuzingatia mwelekeo wa uchumi na mapato ya ndani na pia ahadi za Washirika wa Maendeleo. Pale chanzo cha mapato kisipoweza kufanikiwa kama ilivyokadiriwa haiwezi kuwa sababu ya kusema kwamba inaathiri bajeti yetu au mwenendo mzima wa kiuchumi, nayo pia haina uhakika wa kuipata fedha kamili. Tukubaliane kuwa jambo hili ni muhimu na tunahitaji sisi sote kushirikiana kuhakikisha kwamba mapato ya serikali yanapatikana, lakini pia Wizara yetu ya Fedha na Mipango itaendelea kuwafatilia wale wote walioahidi kuchangia bajeti yetu ili kuona kwamba fedha hizo walizoahidi zinapatikana na kutoleta athari katika utekelezaji wa bajeti ya serikali.

Mhe. Naibu Spika, hoja nyengine ilikuwa vyanzo vya mapato viwekewe mazingira mazuri kwa kuimarisha miundombinu na kuweka mifumo rasmi ya kisasa ya ukusanyaji wa mapato. Jibu la hoja hii Mhe. Naibu Spika, ni kwamba serikali inakubaliana na ushauri wa kamati kwani unaendana na dhamira yake na dhamira ya serikali ya kuhakikisha kuwa ukusanyaji wa mapato yote ya ndani unatumia mifumo ya kisasa ya kiteknolojia. Kwa mapato yasiyo ya kodi tayari Mfumo wa *IFMS* umetumika kwa majaribio kwa wizara tano na utarajiwa kutumika kwa serikali nzima katika mwaka wa fedha ujao. Aidha, Mradi wa *E-Tax* nao unatarajiwa kuimarisha zaidi mifumo ya ukusanyaji sambamba na matumizi ya *EFD* ambayo pia yanatarajiwa kuanza katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Naibu Spika, jana tulizungumza sana na kulikuwa na mada maalum inayohusiana na masuala ya *EFD*, na nadhani Waheshimiwa Wajumbe wamepata uelewa mkubwa wa jinsi gani matumizi ya mashine hizi za *EFD* zitakavyoweza kusaidia katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo vya ndani.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine lilikuwa ni vipaumbele vya taifa na kamati iliitaka serikali ivipitie upya vipaumbele vya bajeti kwa lengo la kuvifanya kuwa mahsusi zaidi.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya bajeti serikali inatambua haja ya kuwa na vipaumbele vichache. Tatizo ni hali yetu ya sasa ya maendeleo inayofanya haja ya kuelekeza fedha katika sekta nyingi kwa wakati mmoja, hali hii itabadilika pindi tutakapokuwa tumepiga hatua kubwa katika maeneo mengine. Nasema hili nalo pia litachangiwa pale tutakapoweza kukusanya na kudhibiti mapato kutoka vyanzo vyetu vya ndani. Na naamini kabisa Waheshimiwa Wajumbe na wananchi sote tutashirikiana katika kuhakikisha katika mwaka wa fedha 2017/2018 basi mapato yetu yanaimarika zaidi.

Mhe. Naibu Spika, hoja nyengine ni mwelekeo wa mapato na wakasema kwamba imefikia wakati sasa *ZRB* na *TRA* zipangiwe malengo kitaalamu badala ya utaratibu wa kujipangia wenyewe malengo hayo.

Mhe. Naibu Spika, malengo ya mapato ya *TRA* na *ZRB* yanapangwa na serikali kwa kuzingatia mwelekeo wa uchumi, utendaji wa sekta kwa kipindi kilichopita. Mambo mapya yanayotarajiwa kutekelezwa kwa kipindi kinachokuja ikiwemo marekebisho ya sheria na mageuzi mengine yanayoidhinishwa. Kuna mfumo maalum wa kukadiria kodi unaotumiwa kupanga malengo ya vyanzo tofauti.

Mhe. Naibu Spika, hoja nyengine ilikuwa kuwepo kwa vyanzo halali vya mapato ambavyo havikusanywi kodi na kupelekea serikali kukosa sehemu ya mapato halali ya mapato yake ya ndani pamoja na mapitio ya mapato yanayokusanywa na Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Naibu Spika, tunashukuru sana maoni ya kamati juu ya suala hili, dhamira ya serikali ni kuhakikisha kuwa mapato yake yote kutoka vyanzo vyote yanakusanywa kwa wakati na ukamilifu. Tutayaangalia na kuyachukulia hatua katika mwaka ujao wa fedha maeneo yote saba yaliyobainishwa na kamati na mapato yanayokusanywa na Idara Maalum na maeneo mengine kama ilivyoelezwa.

Suala jengine nidhamu katika matumizi ya fedha za umma na kamati ilitaka kuwepo na mashirikiano na mawasiliano ya karibu baina ya mawaziri wa fedha kwa mapato ya Muungano au yale yenye athari kwa pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano. Hili nalo ni jambo jengine muhimu ambalo serikali inakubaliana nalo na jitihada kubwa zimefanywa na upande wa SMZ kuhakikisha mashirikiano hayo yanaimarika. Tutaendeleza zaidi jitihada zetu kuhakikisha kwamba tunafanya kazi vizuri zaidi na kwa karibu zaidi baina ya wizara zetu zinazohusika na masuala ya fedha katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kuhusiana na hoja nyengine ya Kamati ya Bajeti Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Bajeti walisema, hatua kali zichukuliwe kwa mujibu wa sheria kwa wote wanaohusika na upotevu wa fedha za umma na serikali iongeze nguvu au iongezee nguvu Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mhe. Naibu Spika, hii ni kauli inayotia moyo sana inayotoka kwenye Kamati yetu ya Bajeti, kama ilivyoanza kudhihirisha serikali haitosita kuchukua hatua au kumchukulia hatua mtendaji yeyote atakayebainika kuhusika na upotevu wa fedha za umma na hatua hizi zitachukuliwa kwa umakini bila ya kumuonea mtu wala kuwa na sindikizo la upande wowote ule.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala lilizungumzwa na kamati pia linalohusiana na ugatuzi wa madaraka, lakni nalo hili lilizungumzwa pia na Mhe. Mwantatu Mbaraka na kamati hii ilionesha wasiwasi wa uhalisia na ulazima wa mpango wa ugatuzi kwa hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, suala hili ni la kikatiba na hivyo tusipolitekeleza tutakuwa tunakiuka katiba yetu wenyewe ambayo tumeitunga katika nchi hii. Aidha, pamoja na udogo wa kisiwa chetu kijiografia bado tuna mfumo wa ngazi tatu ambapo mfumo wa serikali, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali Kuu kwa maana ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, lakini

vile vile Serikali za Mitaa. Mfumo huu unahitaji mgawanyo bayana wa madaraka baina ya ngazi hizo na uamuzi wa sasa wa serikali ni kupeleka baadhi ya majukumu kusimamiwa kweye ngazi iliyo karibu zaidi na wananchi ambayo ni ngazi ya Serikali za Mitaa.

Kuna hoja pia ya watendaji watakaohusika na mpango huo wajengewe uwezo na pia asasi za kiraia zishirikishwe mapema. Nimhakikishie Mheshimiwa, niihakikishie kamati na Waheshimiwa Wajumbe kwamba masuala haya yote ni muhimu sana na kama ilivyoshauriwa na kamati yote haya tunayachukua na yatatekelezwa na serikali kupitia taasisi zake zinazohusika.

Mhe. Naibu Spika, kamati pia ilionesha wasiwasi wake juu ya ongezeko la mishahara kwa watumishi na walizungumzia suala zima la athari ya kuongezeka kwa mishahara hiyo katika uchumi wetu. Niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe lakini pia niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati kwamba, serikali imekuwa ikizingatia mambo mbali mbali wakati wa marekebisho ya mishahara, tunaangalia ndani ya serikali yale masuala chanya lakini vile vile tunaangalia nyongeza stahiki ambazo zinahitaji kwenda kwa wafanyakazi, lakini na matokeo yake tunayoyatarajia katika uchumi wetu. Kwa hivyo, hayo yote yanazingatiwa na Waheshimiwa Wajumbe wasiwe na wasiwasi katika suala hili.

Mhe. Naibu Spika, kuna hoja nyengine iliyozungumzwa inayohusiana na misamaha ya kodi hasa katika kipindi cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Ni suala ambalo hata Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko ameshalizungumza kwa kina kabisa na walitaka kwamba mamlaka husika ziandae utaratibu wa kuwadhibiti wale wafanyabiashara ambao wanakiuka masharti ya kupewa msamaha huo.

Mhe. Waziri amelizungumza vizuri na amesema kwamba serikali italifuatilia na wale wote wanaohusika kwamba wanapewa msamaha, lakini bado wanang'ang'aniza kuwakandamiza wananchi basi hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa dhidi yao.

Mhe. Naibu Spika, kulikuwa na hoja za Waheshimiwa Wajumbe mmoja mmoja na wa mwanzo alikuwa ni Mhe. Shehe Hamad Mattar ambaye alizungumzia suala la gawio la *BoT*, alitaka kujua mapato halisi ya gawio la *BoT* na alisema kwamba hayakuonekana katika bajeti ni kiasi gani kimepatikana.

Mhe. Naibu Spika, kwenye bajeti ya mwaka 2016/2017 makadirio ilikuwa ni kupokea jumla ya shilingi bilioni nne, lakini katika robo ya nne ambapo kwa bahati mbaya sana robo ya nne huwa hatuiingizi katika kitabu. Fedha zilizopokelewa ni shilingi 14 bilioni sawa na asilimia 350 ya matarajio. Lakini Mheshimiwa ni muhimu na ni vyema kuwajuilisha Waheshimiwa Wajumbe kwamba Benki Kuu haipo kufanya biashara. Kwa hiyo, kupata faida si miongoni mwa malengo ya msingi ya Benki Kuu, lakini pale inapotokezea kuwa na faida kutokana na shughuli zake mbali mbali ikiwemo ukodishaji wa majengo yake faida ile ndio tunayogawana kwa uwiano ule ambao tumekubaliana baina ya pande mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani alizungumzia suala la wanunuzi kuhojiwa na kutozwa kodi ya *VAT* wanaposafirisha bidhaa zao kwenda Tanzania Bara au kutoka Bara kuja navyo hapa Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, nieleze kwamba wafanyabiashara hao wanachoulizwa na wale wafanyabiashara au watu wanapokutwa na bidhaa huwa wanaulizwa kutoa risiti za bidhaa hizo.

Lengo ni kuhakikisha uhalali wa umiliki wa bidhaa hizo na iwapo muuzaji amekusanya kodi ya serikali kwa mnunuzi kutokana na mauzo hayo. Utaratibu huu ni kwa mujibu wa matakwa ya kisheria na bila shaka pia unawasaidia wanunuzi kuwa ni kielelezo cha umiliki na pia kuwa na kumbukumbui sahihi za biashara hizo. Niseme tu Mhe. Naibu Spika, kwamba katika mwaka wa fedha wa 2017/2018 tutaweka mkazo sana katika suala zima la wafanyabiashara kutoa risiti lakini vile vile na wananchi pia wanaponunua bidhaa zinazostahiki kupata risiti basi wadai risiti. Ni kinyume cha sheria mtu kwenda kununua bidhaa halafu asiwe na risiti atakapokumbana na wahusika basi atakuwa na hatia ya kujibu. Kwa hiyo, hilo ni suala ambalo sisi sote Waheshimiwa Wawakilishi tujenge muamko huo kwa wananchi wetu ili wahakikishe kwamba wanadai risiti wanaponunua bidhaa na kuweza kusaidia katika kuchangia mapato serikali.

Pia Mhe. Abdalla Maulid Diwani alizungumzia suala la wanunuzi kutozwa kodi mara mbili pindi wanaposafirisha bidhaa kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara au kinyume chake. Ni kweli kuwa marekebisho ya sheria ya *VAT* yaliyofanywa na sheria ya fedha Tanzania Bara mwaka 2016 yameleta matatizo ya biashara baina ya pande mbili za Jamhuri ya Muungano likiwemo suala la kutozwa kodi hiyo mara mbili kwa wanunuzi wanaonunua bidhaa zinazotengenezwa nchini kutoka madukani na baadae kuzisafirisha kuja hapa Zanzibar. Ni wanunuzi wa bidhaa kutoka viwandani tu pale Tanzania Bara ambao wamesajaliwa na *VAT* Zanzibar ndio kiujumla hawaathiriki na tatizo hili. Tunaelewa kuwa hawa wafanyabiashara wakubwa wanaonunua vitu viwandani sio wengi ukilinganisha na wanaonunua bidhaa madukani. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imechukua jitihada maalum na itaendelea kuwasiliana na wenzetu wa Hazina SMT kuiona athari inayotokea baina ya pande zetu mbili katika masuala mazima ya kibiashara ili tuweze kwa pamoja kufikiria jinsi gani tunaweza kuondoa changamoto na kasoro hizi. Kwa hivyo, niwaahidi Waheshimiwa Wajumbe kwamba hili suala sisi bado hatujachoka nalo tunaendelea kulifuatilia na tutaendelea kulizungumza na wenzetu ili nao waone katika mtizamo ule ule ambao na sisi tunauona katika athari inayotokana na mabadiliko ya sheria ya fedha yaliyofanyika mwaka 2016.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Miraji Khamis Mussa, Mhe. Hamad Abdalla Rashid, Mhe. Tatu Mohamed Ussi, Mhe. Maryam Thani Juma, Mhe. Panya Ali Abdalla na Mhe. Omar Seif Abeid. Wao walizungumzia hoja moja ya kuwa na mfumo mmoja wa kitaifa wa kusimamia mapato na Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza awali matumizi yaliyoanza ya kutumia mfumo wa *IFMS* kukusanyia maduhuli ya serikali na matarajio ya kuanza kutumia mfumo wa *E-Tax* inatuelekeza katika kuelekea huko kwenye mfumo mmoja. Lengo la baadae ni kuwa na mfumo unaogusa maeneo yote ya mapato tokea uzalishaji, uagiziaji biashara za ndani hadi kodi za mapato kutokana na faida ya uwekezaji au ajira. Kwa hivyo, lengo letu ni kwenda kwenye mifumo hii kuimarisha mifumo na tumesema katika hotuba ya bajeti kwamba mwaka wa fedha 2017/2018 tunakusudia kuufanyia mapitio mfumo mzima wa ukusanyaji wa kodi nchini ili kuhakikisha kwamba tunaweka mfumo bora utakaotuhakikishia tunakusanya mapato kwa wakati na kwa ukamilifu wake.

Waheshimiwa hawa pia walizungumzia kuhusiana na mkakati upi madhubuti uliowekwa na serikali katika matumizi ya *EFD.* Kama nilivyoeleza hatua za kuanza matumizi ya *EFD* ...

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri nakuomba kidogo. Waheshimiwa Wajumbe kwa kuwa waziri bado anaendelea kujibu hoja zetu na kwa kuwa muda wetu unakaribia kwisha ningemuomba

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais atuongezee muda ili tuweze kumaliza bajeti yetu leo hii kama ratiba inavyoelekeza. Kwa hiyo, Mhe. Waziri karibu sana.

KUONGEZA MUDA WA BARAZA

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa muda ulio mbele yetu haumtoshi Mhe. Waziri kufanya majumuisho na kumalizia suala zima la bajeti yetu hii kubwa ya nchi, hivyo niliombe Baraza lako tukufu litengue kanuni ya muda iweke kando ili tumpe nafasi Mhe. Waziri na hatua yengine zinazofuata ili tupate kufanyika kwa utaratibu mzuri mpaka hapo tutapomaliza shughuli zetu ndio tuweze kumaliza kazi iliyo mbele yetu.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa tuendelee.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza kwamba Waheshimiwa wengi na nimewataja wamezungumzia juu ya suala la mkakati upi madhubuti uliowekwa na serikali katika matumizi ya mashine za *EFD*. Kama nilivyoeleza hatua za kuanza matumizi ya *EFD* ziko katika hatua za mwisho tunatarajia kwamba mashine hizi zitaanza kutumika katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha wa 2017/2018. Niseme hapa jana tulikuwa na semina lakini juhudi kubwa tunafanya kwa kushirikiana baina ya wizara zetu mbili, Wizara ya Fedha na Mipango na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko katika kuhakikisha ndani ya robo ya kwanza basi mashine za *EFD* zinakuwepo nchini na zinaanza kutumika.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Yussuf Hassan Iddi na Mhe. Machano Othman Said walizungumzia suala la kupanda kwa mapato ya *PAYE* na kama iwapo kupanda huko kumezngatia kupungua kwa asilimia ya makato kutoka asilimia 13 hadi asilimia 9.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kuwa katika kuimarisha kipato cha wafanyakazi wa kipato cha chini kuanzia mwezi Aprili mwaka huu serikali ilipunguza kiwango cha kodi *PAYE* kinachotozwa katika ngazi ya chini kabisa kutoka asilimia 13 hadi asilimia 9. Na ni kweli pia kuwa pamoja na kupungua huko, malengo ya ukusanyaji mwaka 2017/2018 yameongezeka. Naomba niseme kuwa upangaji wa malengo hayo umezingatia kupungua huko kwa kiwango cha kutozea kodi kwa ngazi hiyo moja. Ongezeko la mapato linategemewa kwamba aidha limetokana na kuongezeka kwa mishahara lakini pili kuongezeka kwa walipa kodi, kwani sasa kiasi cha kipato kwa mwezi kilichosamehewa kodi kimepandishwa kutoka shilingi 150,000 hadi shilingi

180,000. Kwa utaratibu huu sasa wafanyakazi wote wa serikali watakuwa wanalipa kodi tafauti na awali ambapo wale wa kipato cha chini cha shilingi 150,000 tu walikuwa wamesamehewa.

Pia walizungumzia suala la misamaha ya kodi ni kiasi gani. Mhe. Naibu Spika, niseme kwmaba jumla ya misamaha ya kodi iliyotolewa baina ya mwezi Julai, 2016 na mwezi Mei, 2017 ni shilingi 30.3 bilioni ambapo kupitia *TRA* ilikuwa shilingi 13.9 bilioni na *ZRB* ni shilingi 16.4 bilioni na hizi takwimu ni hadi mwezi Mei, 2017.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia kulikuwa na suala zima walilozungumzia suala la vifungu kwenye kodi mahasusi ya tija na alivitaja vifungu 1111004 na vifungu 1151007. Hili suala lilizungumzwa nadhani na Mhe. Yussuf Hassan Iddi na alizungumzia kwamba hivi ni vifungu vimoja na kwa nini mwaka huu kumewekwa *zero*.

Mhe. Naibu Spika, mabadiliko haya yamefanyika kurekebisha makosa yaliyojitokeza mwaka jana ambapo makisio hayo kwa *TRA* yalioneshwa chini ya Idara ya Kodi za Ndani badala ya idara sahihi ambayo ni Idara ya Forodha. Kwa mwaka 2017/2018 yameondoshwa Idara ya Kodi za Ndani na kuhamishiwa Idara ya Forodha.

Pia kulikuwa na hoja kwa nini kodi za nyumba za serikali hazionekani kwenye bajeti ya mwaka 2017/2018, nayo hii pia ilizungumzwa na Mhe. Yussuf Hassan na aliulizia je, kodi hiyo imesamehewa? Mhe. Naibu Spika, ni kweli kuwa zamani mapato yanayotokana na ukodishwaji wa nyumba za serikali yalikuwa ni moja wapo ya mapato yanayoingia Mfuko Mkuu wa Serikali. Kwa sasa serikali imeanzisha Shirika la Nyumba na kuzikabidhi kwake nyumba hizo zilizokuwa zikikodishwa na serikali, kwa kuwa sasa zinaonekana kana ni mali za shirika mapato yake yanaingia kwenye hesabu za shirika badala ya kuonekana kama mapato ya serikali moja kwa moja na hivyo tumeondokana na makadirio yake kwenye bajeti ya serikali.

Mhe. Rashid Makame Shamsi na Mhe. Omar Seif Abeid walizungumzia kuhusiana na suala la gawio la Mashirika ya SMZ na kuonesha kutoridhika na matokeo yanayopatikana kwa maana ya gawio linalotokana na mashirika hayo na wakahoji kama wakala nao pia wanahusika na kutoa huduma feki.

Mhe. Naibu Spika, Mashirika ya Serikali ni mkono wa kibiashara wa serikali ambayo yanatarajiwa yajiendeshe kibiashara na kwa faida. Kwa kuwa serikali ndio mmiliki pekee, inatarajia pia kuwa mashirika hayo yaipatie gawio serikali kutokana na faida wanayoifanya. Nimwambie Mhe. Rashid Makame na Mhe. Omar Seif Abeid kwamba wizara itafuatilia zaidi iwapo faida kwa baadhi ya mashirika na hivyo kuangalia kwamba kwa nini gawio linalostahiki kutolewa kwa serikali halitolewi kama inavyostahiki. Kwa hivyo, hili ni suala ambalo Mheshimiwa tunaahidi kulichukua na tutalifuatilia kwa mashirika yetu yote.

Mhe. Ali Suleiman Shihata ametoa ushauri pamoja na Waheshimiwa wengine Mhe. Ali Khamis Bakari (Doholo), Mhe. Shaib Said Ali, Dkt. Mwinyihaji Makame, Ame Haji Ali na Mhe. Suleiman Sarahan Said. Hawa wametoa ushauri na maoni mbali mbali yanayyohusu uimarishaji wa ukusanyaji mapato ikiwemo mianya inayosababisha kuvuja mapato ya serikali. Lakini vile vile maoni kama haya yalitolewa na Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Maryam Thani Juma, Mhe. Bahati Khamis Kombo na Mhe. Asha Abdalla Mussa.

Kwanza niseme kwamba tunashukuru sana Waheshimiwa wote hawa kwa kutupa maoni haya, lakini pia tunawashukuru kwa kutambua umuhimu wa kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani, lakini pia kutambua jitihada kubwa ya serikali zinazochukuliwa kwa azma hiyo na tatu kwa kuisaidia serikali kwa kuonesha maeneo ambayo yakishughulikiwa yatasaidia zaidi kuimarisha mapato. Naahidi kabisa tutashirikiana na Waheshimiwa Wajumbe na wananchi wote wenye nia njema kabisa kwa nchi yetu katika kuainisha vyanzo vyengine vya mapato, lakini pia watakaotusaidia katika kuainisha upotevu wa mapato kutokana na vyanzo hivyo. Sisi tunaahidi kuyachukulia hatua kikamilifu ili kuimarisha mapato ya serikali.

Mhe. Naibu Spika, kulikuwa na suala la taarifa nafikiri hizi zimeshatolewa maelezo, lakini nikiri tu kwamba kwa bahati mbaya sana kulitokea tatizo la takwimu baina ya kitabu cha hutuba ya Mpango wa Maendeleo na ile iliyotolewa hutuba ya wizara inayohusika na Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto katika masuala mazima ya udhalilishaji wa kijinsia. Nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wakubali kwamba taarifa ile iliyotolewa na wizara husika tuichukue kama ndio taarifa sahihi na tatizo lililojitokeza ni kwamba, wakati Tume ya Mipango walipopata taarifa ya mwanzo watu wa sekta kwa sababu wanaendelea na ukusanyaji wa taarifa walikuwa tayari wameshaongeza na kubadilisha taarifa ile na kwa bahati mbaya sana si jambo ambalo linatokea mara nyingi ni jambo ambalo linatokea kwa bahati mbaya sana taarifa ile haikuweza kuwasilishwa moja kwa moja kwenye Tume ya Mipango na yakatokezea hayo yaliyotokezea ya kuwepo na utofauti wa takwimu hizo. Lakini kama nilivyosema naomba sana Waheshimiwa Wajumbe wachukue takwimu zilizotolewa na wizara inayohusika kwamba ni takwimu sahihi.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala liliuliziwa kuhusiana na matatizo ya kibenki za biashara na hili lilizungumzwa na Mhe. Abdalla Maulid Diwani lakini pia liligusiwa na Mhe. Tatu Mohammed Ussi na hapa hasa lilizungumziwa suala la wizi kwenye Banki ya *NBC* na nimueleze Mhe. Abdalla Maulid Diwani kwamba tumepokea taarifa hii. Kwanza napenda kuwapa pole wateja wote waliopatwa na fadhaa na matatizo kutokana na mkasa huo na kwa kuwa wizi umetokana ndani ya benki kupitia wafanyakazi wasio waaminifu naamini benki husika inapaswa kubeba jukumu la kuhakikisha kila mteja anapata hali yake kama alivyoiweka.

Lakini kwa upande wetu ili kutafuta ufumbuzi muafaka tutawasiliana rasmi na benki hiyo. Lakini pia ikibidi basi tutafanya mawasiliano na msimamizi wa mabenki ambayo ni Benki Kuu ili kuona kadhia hii inapata ufumbuzi haraka iwezekanavyo.

Ipo hoja nyengine Mhe. Naibu Spika, ya kufutwa kwa leseni ya Benki ya *FBME* na Waheshimiwa waliuliza ni vipi wateja watapata haki yao. Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba ni kweli kwa Benki kuu imefuta leseni la Benki ya *FBME* na hivyo mchakato wa kuifilisi umeanza rasmi.

Naomba pia nitumie fursa hii kuwa pole wananchi wote walioathirika na hatua hiyo iliyolenga kuhami wateja na mfumo wa sekta ya fedha kutokana na *FBME* kutiwa hatiani nchini Marekani kwa tuhuma za kushiriki katika utakatishaji wa fedha haramu. Kwa sasa mchakato wa kufilisi umeanza chini ya Taasisi ya Bodi ya Bima za Amana kwa maana *adiposities insurance board*. Pamoja na mambo mengine bodi hii itakuwa na jukumu la kutambua wateja wote wenye hesabu

katika benki hiyo, mali na madeni ya benki na hatimae kuweza kuwalipa wenye amana zao kwa mujibu wa sheria ziliopo.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame na Mhe. Omar Seif Abeid walizungumzia pia suala la uwekezaji kupitia *ZIPA* na walisema kwamba miradi mipya ya uwekezaji imepungua sana kwa mwaka 2016/17. Mhe. Naibu Spika, ni kweli idadi ya miradi na kiasi cha uwekezaji kimepungua sana mwaka huo ukilinganisha na mwaka 2015/16.

Serikali inafanya mapitio ya sheria ya *ZIPA* kama nilivyosema mwanzo, lakini pia tunaandaa vigezo maalum vya wawekezaji wakubwa wenye hadhi maalum kwa maana *Strategic investment* na kuchukuwa jitihada za kufungua maeneo zaidi ya uwekezaji kama vile uvuvi wa bahari kuu na viwanda baada ya kutegemea uwekezaji katika sekta ya utalii pekee ambayo ndio imeanza kupungua uwekezaji mpya. Jitahda hizi zitakwenda sambamba na uimarishaji wa utendaji wa *ZIPA* yenyewe na utaratibu wake katika kusimamia miradi ya uwekezaji nchini.

Kuna suala lilizungumzwa la Bandari ya Mpigaduri naamini hili limetolewa maelezo mazuri na Mhe. Naibu Waziri anaehusika na Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. Sina haja ya kulieleza hilo. Lakini kulikuwa na hoja ilikuwa inazungumzia muingiliano wa miradi mikubwa na katika hili niseme tu hakutakuwa na mwingiliano wa miradi mikubwa kwa vile kumeshafanyika mpango wa matumizi wa eneo hasa katika eneo la kitalii la Maruhubi. Pale kumefanyika mpango wa matumizi wa lile eneo na kwa namna hiyo mradi wa ujenzi wa Bandari wa Mpigaduri hautaathiri miradi mingine iliyoko pale ikiwemo hifadhi ya Maruhubi yenyewe lakini pia Chuo cha Utalii na shughuli nyengine za kihoteli zinazoendelea katika eneo lile.

Lakini Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame alizungumzia hatma ya wananchi kwenye miradi ya uwekezaji katika eneo la Fumba. Mhe. Naibu Spika, kama ilivyo kwa maeneo mengine wananchi wa maeneo ya Fumba wanahitaji kupewa mazingatio maalum ili waweze kuishi wao na vizazi vyao vijavyo bila ya kuathiriwa na uwekezaji. Kwa sasa serikali imeidhinisha uwekezaji katika eneo huru la uchumi lililotangazwa toka mwaka 1992. Hata hivyo, baadhi ya watu ikiwemo wananchi nao wamekuwa wakiuza maeneo nje ya eneo huru kwa ajili ya uwekezaji na ujenzi wa nyumba za kuishi. Kilio cha Mheshimiwa Mwakilishi tutaendelea kukisikiliza na serikali itakuwa makini kuweza maendeleo ya uwekezaji bila ya kuwaumiza wananchi wake.

Mhe. Naibu Spika, kuna hoja inayosema tuna wawekezaji wengi ila wamehodhi ardhi kubwa ambazo hawazitumii na wengine kuzikodisha. Mhe. Naibu Spika, kuna ukweli katika jambo hili na pamoja na hatua zinazochukuliwa na serikali za kufuta mikataba ya ukodishaji ardhi bado Wizara yangu ya Fedha na Mipango itashirikiana na taasisi na wizara nyengine zinazohusika katika kulifuatilia suala hili ili kuhakikisha kwamba linapatiwa ufumbuzi wa haraka na kuona wale wanaohodhi maeneo kwa muda mrefu bila ya kuendeleza basi wanachukuliwa hatua ipasavyo kwa mujibu wa sheria za nchi yetu.

Mhe. Yussuf Hassan Idd alizungumzia suala la deni la tiafa na alizungumza je, deni letu la taifa ni himilivu kwa maana *sustainable*. Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba kila nchi inayokopa huhitaji kuhakikisha kuwa kiwango cha deni lake ni himilivu kwa kuzingatia uchumia wake, mapato ya serikali na usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi. Kwa Tanzania upeo wa mikopo dhidi ya pato la taifa umewekewa ukomo wa uwiano wa asilimia 50% na kwa Zanzibar kama nilivyoeleza

katika hotuba ya bajeti uwiano wa deni kwa pato la taifa ni chini ya asilimia 15% na ndio maana nikasema kuwa deni letu ni himilivu na bado linaonesha fursa kubwa ya kuweza kukopa lakini pia tuna uwezo wa kulipa deni hilo.

Lakini niseme tu kwamba huwa kunafanyika utafiti maalum katika suala zima la uhimili wa madeni yetu na kwa Tanzania utafiti huo ulifanyika mwaka 2016 na unafanywa na vyombo vya kimataifa vya fedha kwa maana ya Benki ya Dunia *IDA.* Lakini vile vile na chombo chengine cha fedha cha kimataifa *International Monitoring Fund*. Utafiti huo ulifanyika mwaka 2016 na umeonesha kwamba bado serikali yetu kwa maana Jamhuri ya Muungano wa Tanzania madeni yetu yako himilivu kwa maana yako *sustainable* na kwa hapa Zanzibar hali yetu iko vizuri zaidi tunaweza kukopa zaidi na tuna uwezo wa kurudisha mikopo ambayo tunaikiopa.

Kuna suala ambalo lilizungumzwa kwamba linachukua muda gani deni letu kuwiva na kiwango cha riba kwa mwaka ni kiasi gani. Mhe. Naibu Spika, tuna madeni ambayo yanamalizika muda wake katika vipindi tafauti yako ambayo yanaanza sasa kuiva katika mwaka 2018, lakini mengine yatakwenda mpaka mwaka 2050 yako yatakayokwenda mpaka mwaka 2058 inategemea siku mkopo ule ulivyochukuliwa, lakini vile vile inategemea na masharti ya mkopo huo. Lakini inategeme kwamba ni muda mfupi au mrefu au muda wa kati, lakini vile vile katika makubaliano kiwango cha riba kilichokubalika kilikuwa ni kasi gani.

Marekebisho mbali mbali kwenye vifungu vya Bajeti Mhe. Yussuf Hassan Iddi alitoa hoja kwamba wizara ijitahidi kuongeza bajeti ya Utalii, Afya na Viwanda, bajeti ya afya ifanane na ya elimu. Lakini hili pia lilizungumzwa sana na Mhe. Viwe Khamis Abdalla na niseme tu kwa mwaka 2017/18 bajeti za wizara zote zimeongezeka japo kwa ukuaji tafauti na kwa kawaida karibu nchini zote zinazoendelea hususan Kusini mwa Jangwa la Sahara Bajeti ya Elimu inakuwa kubwa kuliko ya Afya. Hii inatokana na idadi kubwa ya watoto wanaohitaji elimu kwa muda wote na wakati mmoja. Ni kwa msingi huu ndio maazimio ya kimataifa yanaelekeza kuwa elimu ipatiwe karibu robo ya bajeti na wakati sekta ya afya ikiombewa asilimia 15%.

Lakini hapa niseme kwa sababu liko suala jengine liliulizwa ni kwamba katika mwaka wa fedha 2016/17 serikali yetu imejitahidi sana na tushukuru sana uongozi wa Mhe. Dr. Ali Mohd Shein kwa udhibiti wake katika masuala mazima ya ukusanyaji mapato, takribani wizara zote hakuna wizara iliyopata chini ya asilimia 90% ya bajeti yake. Lakini vile vile ziko wizara ambazo zimezidi asilimia 100% na ilitokea kutokana na mahitaji maalum yaliolekezwa katika wizara hizo. Tuombe Mwenyezi Mungu na tushirikiane kwa pamoja kuhakikisha kwamba makusanyo hayo yanaweza kuwa mazuri zaidi katika mwaka 2017/18 na tunataka tuwe na mpango madhubuti zaidi wa kuhakikisha kwamba wizara zote zinapata fedha zao kwa mujibu wa bajeti zao, lakini vile vile zipatikane kwa wakati.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala zima la kupungua kwa jumla ya bajeti ya michezo na mazingira kwa mazingatio ya muhtasari wa bajeti. Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba bajeti kwa ujumla kuna baadhi ya maeneo ambayo ikilinganishwa na mwaka jana bajeti imepungua. Hali hii aghalabu hutokea kutokana na kukamilika kwa miradi ya maendeleo na hivyo fedha zake kutowekwa tena katika bajeti inayofuata ikiwemo kutokana na zile fedha zinazotolewa na washirika wa maendeleo. Takrabani maeneo yote hayo yamepata bajeti kubwa zaidi kutokana na fedha za ndani kulinganisha na mwaka uliopita kama nilivyokwisha kueleza.

Mhe. Naibu Spika, suala la pencheni ya jamii hili limeshatolewa ufafanuzi na zaidi ilikuwa ni pongezi ambazo tunazichukuwa pongezi hizo na kama nilivyosema mwanzo pongezi hizo hasa zinamstahiki mwenyewe Mhe. Rais Dr. Ali Mohd Shein. (*Makofi*)

Kuna suala jengine lilizungumziwa na Dr. Mwinyihaji Makame suala la kuwazungusha wahasibu na washika fedha. Nimuhakikishie tu kwamba kazi hii inafanyika hata katika kipindi hichi cha karibuni tumewazungusha wahasibu na washika fedha na kazi hiyo itaendelea kadri itakavyoonekana kuna haja ya kufanya hivyo.

Mhe. Naibu Spika, lipo suala ambalo lilizungumzwa na Mhe. Mussa Ali Mussa na alilizungumzia sana suala la Jengo la Tibirinzi jengo la Wizara ya Fedha na alitaka kwamba tuwe tunafatilia mikataba na tunawafatilia wakandarasi hasa wa miradi mikubwa na kusema kwamba jengo lile pale liondolewe. Niwambie kwamba wizara imefanya juhudi kubwa sana suala hili au shauri hili lilipelekwa mahakamani na hukumu imetoka. Lakini mkandarasi huyu kwa bahati mbaya sana hayupo nchini hivi sasa kwa taarifa tulizonazo anaishi Mombasa nchini Kenya na kwa bahati mbaya nyengine kwamba hakuwa na mali hapa ambayo sisi tungeweza kuishika. Kwa hivyo, bado tunaendelea na juhudi za kuhakikisha kwamba huko aliko tunamfikia na anafikiwa na vyombo vya sheria ili tuweze kukaza hukumu.

Lakini vile vile alizungumzia suala la Jengo la Soko la Wete nikubaliane nae kwamba jengo hili tayari limeshazinduliwa raasmi na amelizindua Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Ali Mohammed Shein na kama anavyosema kumetokea kasoro niahidi kwamba tutafatilia kasoro hizo. Lakini kwa sababu jengo hili liko katika muda ambao mkandarasi anatakiwa kufanya marekebisho ya matokeo yote yatakayotokea ya uharibifu basi ile *liability period* tutamtaka mkandarasi huyo aweze kufanya marekebisho yanayostahiki.

Jengo la Unguja Ukuu kwa waathirika wa dawa za kulevya na yeye amesema liko chini ya kiwango. Lakini nimwambie tu kwamba na hilo tutalifuatilia kwa kushirikiana na wizara inayohusika na kama yapo mambo ambayo yanastahiki kufanywa na mkandarasi basi mkandarasi huyo nae atafatiliwa na kuweza kufanya marekebisho hayo. Lakini kubwa zaidi ni kuzidisha umakini katika uandaaji wa mikataba lakini pia ufungaji wa mikataba na katika suala zima la usimamiaji wa utekelezaji wa mikataba hiyo.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mussa Ali Mussa pia alizungumzia suala la fidia za barabara za Ole-Kengeja na nimuhakikishie Mhe. Mussa Ali Mussa kwamba kama nilivyomwambia wakati siku moja nikijibu suali lake katika Baraza hapa, kwamba suala hili tutalifuatilia na litafanyiwa uhakiki kwa wale wote wanaostahiki kupata malipo yao ya fidia basi watapata malipo yao na serikali mara zote haiwakandamizi wananchi wake wala haiwadhulumu wananchi wake. Kwa hivyo, suala hili tutalifanyia kazi kwa kushirikiana na wizara husika.

Lakini pia nimueleze tu kwamba suala la fidia hii halikuwekwa katika bajeti ya mwaka 2017/18 kwa sababu dhamira yetu na mpaka sasa ndio tuna dhamira hiyo fidia hii imalizike kabla ya julai 2017. Kwa hivyo, tunataka imalizike ndani ya mwezi wa Juni na pia nimfahamishe Mhe. Mussa Ali Mussa hadi Machi 2017 jumla ya shilingi milioni mia tatu hamsini na nane nukta nane

zimeshalipwa na bado tumetenga shilingi bilioni 1.5 kukamilisha fidia ya nyumba na vipando ndani ya mwezi huu wa Juni. (*Makofi*)

Mhe. Jaku Hashim Ayoub yeye alizungumzia je, bajeti hii inaendana na vipambele vilivyowekwa. Tayari nimetoa maelezo kuhusu serikali ilivyojipanga na inavyodhamiria katika kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato na nimwambie kwamba vipambele vyote tulivyoviweka basi vinaendana na bajeti tuliyoizingatia. Pale inapotokea bahati mbaya inakuwa bahati mbaya na tutaitolewa taarifa. Lakini vipaumbele hivi vimewekwa kwa mujibu wa matarajio yetu ya mapato ya ndani na mapato ya nje. Kwa hivyo, hilo Mhe. Jaku Hashim Ayoub asiwe na wasi wasi nalo walioandaa hii wataalamu makini sana na wanataratibu maalum wanazozifuata katika kueka vigezo lakini pia katika kuweka makadirio ya mapato yatakayoweza kukusanywa katika mwaka wa fedha unaohusika.

Lakini pia alizungumzia suala la kuingizwa fedha na akataka kwamba fedha za Wizara ya Afya ziwe zinaingizwa kwa wakati na hili nimeshalieleza kwamba wizara zote kwa mwaka wa fedha 2016/17 zimeingizwa fedha za kutosha na tulijitahidi sana fedha hizo ziwe zinaingizwa kwa wakati. Kwa upande wa Wizara ya Afya walikuwa an bahati ya kipekee kwa sababu ni katika miongoni mwa wizara chache ambazo zimefikia asilimia mia moja bajeti yao ya mwaka 2016/2017 ilikuwa bilioni 11.9 na wamepata zote bilioni 11.9 sawa na asilimia 100%. Lakini hii si kwa wizara hii tu kwa wizara nyingi zilipata asilimia 100% nyengine zilizidi lengo aliekosa chini basi hakukosa chini ya asilimia 90% na tutaendelea na ari hiyo hiyo na tunawaomba watendaji wetu wote waielewe kasi ambayo Rais Dr Ali Mohammedd Shein ameiweka katika kuhakikisha kwamba yale yote yanayopangwa na serikali hii basi yanatekelezwa katika kipindi hichi. (*Makofi*)

Suala la Hoteli ya Bwawani nayo hii nimjulishe Mhe. Jaku Hashim kwamba hoteli hii imekodishwa kwa kampuni ya *Quality group* na kinachoendelea hivi sasa ni kwamba ametakiwa kwa mujibu wa sheria za nchi yetu kwanza kufanya *heritage impact assessment.* Lakini vile vile afanye *Environmental impact assessment* na kazi hiyo sasa hivi inafanywa, kwa sababu hawezi kuendeleza eneo lile kabla hajapata kibali cha *UNESCO* na haya ni mambo ambayo sisi wenyewe tumejipangia kwa kuuweka mji wetu kuwa ni Mji wa Urithi wa Kimataifa. Kwa hiyo, ni masuala ambayo yanafata utaratibu wa kisheria lakini pia nimjulishe tu kwamba jengo la Hoteli ya Bwawani ukarabati unaendelea ulisimama kidogo lakini sasa hatua za ukarabati wa jengo hilo zinaendelezwa.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema mwanzo niwashukuru kwa mara nyengine tena Waheshimiwa Mawaziri wa Wizara mbali mbali wamesaidia sana kujibu hoja nyingi. Kwa hivyo sina haja ya kuzirudia hoja zile niwashukuru wao niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe waliouliza maswala na waliotaka ufafanuzi katika maeneo mbali mbali.

Lakini nirudie kuwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa mashirikiano makubwa wanayonipa mimi ndio yalioniwezesha kusimama hapa na kutoa ufafanuzi wa hoja hizi.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, sasa naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Waziri ametoa hoja. Sasa niwahoji, wanaokubaliana na hoja hiyo, wanyooshe mikono, wanaokataa hakuna, wanaokubali wameshinda. Waheshimiwa hoja imekubalika kwa asilimia 100% hongereni sana. (*Makofi*)

Mhe. Waziri tunakupongeza sana na tunakushukuru sana kwa kazi nzuri ambayo umeifanya basi tukutakie kila la kheri, uweze kutimiza malengo yako pamoja na serikali yetu.

Lakini niwapongeze zaidi Waheshimiwa Wajumbe vile vile kwa michango yao mizuri kabisa pamoja na mawaziri kwa kuweza kusaidia kujenga hoja na niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe wakati tunachangia hapa wengi walikuwa wanaielekezea serikali kwamba kusimamia masuala ya fedha tumeipa jukumu serikali.

Lakini Waheshimiwa Wajumbe na sisi tunajukumu hilo kusaidiana na serikali ili kuweza kutimiza malengo yetu. Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe tusisahau hilo pia na sisi ni kazi yetu kusimamia serikali. Kwa hiyo, sote kwa pamoja tukishirikiana tutaweza kufika katika yale ambayo tumeyakusudia.(*Makofi*)

Nawashukuru sana kwa utulivu wenu na sasa ninaakhirisha kikao hadi kesho tukijaaliwa saa 3.00 asubuhi.

(Saa 9:20 jioni Baraza liliakhirishwa mpaka
tarehe 20 /06/2017 saa 3:00 asubuhi)